**CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**SHULE YA SANAA NA SAYANSI ZA JAMII**

**IDARA YA KISWAHILI**

# DHIMA ZA HURAFA KATIKA FASIHI YA WATOTO

**NA**

**AGNES MAKANDI NGITI**

**TASNIFU LA UTAFITI LILILOWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA**

**MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA 2019**

**UNGAMO**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa katika chuo kingine chochote.

Sahihi Agnes Tarehe 27/11/2019

Agnes Makandi Ngiti

C 50/CE/26045/2011

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini ya wasimamizi wafuatao kwa niaba ya chuo kikuu cha Kenyatta.

Sahihi ________ Tarehe 27/11/2019

Profesa Catherine Ndungo

Idara ya Kiswahili

Sahihi ________ Tarehe 27/11/2019

Dkt. Miriam Osore

Idara ya Kiswahili

## TABARUKU

Kwa mama yangu Esther Mwarania, dada zangu Evylin Wanja na Florence Kanyiri.

## SHUKRANI

Nashukuru Maulana kwa kunipa siha ya kuandika kazi hii hadi mwisho. Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Profesa Catherine Ndungo na Dkt. Miriam Osore, waliojitolea kwa njia zozote zile kuniongoza kwa hekima na ukakamavu. Pia natoa shukrani kwa wahadhiri wangu Dkt. Wafula, Dkt. Mwihaki, Dkt. Ngugi, mwalimu Mudhune, Dkt. Kingei, Dkt. Gakuo, Dkt. Masinde na wengine wa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta walionisaidia na kunielekeza nilipokuwa nikitafiti. Kwa watoto wangu Dan, Muriu, Mutwi na mume wangu Athinya walionivumilia nilipokuwa naishughulikia kazi hii, shukrani nyingi ziwafikie.

Nawashukuru wenzangu Milka, Musila, Karimi, Njeri, Mugure, Kamba, Kamanja na Kaaria walionitia motisha kuendelea na kazi hii. Sitasahau kuwashukuru wanafunzi wengine wote tulioshiriki katika masomo ya shahada ya uzamili. Kongole zangu za dhati kwa mwalimu Mwirebua na wengine walioniwia radhi na kunielewa wakati nilipokuwa naishughulikia kazi hii.

Nawashukuru wote wale ambao sijawataja na walinisaidia kufanikiza kazi hii.

# IKISIRI

Utafiti huu umechunguza dhima za hurafa katika fasihi ya watoto. Malengo matatu ya utafiti ni kubainisha dhima katika hurafa kwa watoto, kuchunguza maudhui katika hurafa kwa watoto na kudhihirisha mbinu zilizotumika kuwasilisha dhima na maudhui kwa watoto.Data ya utafiti imedondolewa katika vitabu teule ambavyo ni *Ngiri Mganga* (2010) cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Mayega. Vitabu hivi vimeteuliwa kwa makusudi kwa sababu vinasawiri dhima, maudhui na mbinu tofauti katika hurafa. Nadharia mbili zimeongoza utafiti huu nadharia ya semeotiki na nadharia ya naratolojia. Nadharia ya semeotiki iliyoasisiwa na Pierce (1977) inaongoza swali la jinsi wasomaji wa hadithi wanavyohakiki kazi ya fasihi na kuipa maana. Mwasisi wa nadharia ya naratolojia ni Prince (2003). Kulingana na Prince (2003) nadharia ya naratolojia huchanganua usimulizi au uandishi wa hurafa kama mbinu zilizotumiwa kuchangia watoto kuelewa ujumbe unaowasilishwa. Dhima na maudhui yaliyobainishwa huhimiza ujumbe unaokuwa muhimu kwa watoto. Mahali pa utafiti ni maktabani. Data na matokeo ya utafiti yamewasilishwa kimaelezo. Utafiti huu una manufaa kwa wahakiki, wandishi wa vitabu vya watoto na wanafunzi wa vyuo vikuu. Pia wakuza mitaala ya elimu watafaidika kuthibitisha dhima za hurafa katika fasihi ya watoto.

## ABSTRACT

This study is about the role of fables in children's literature. Its main objectives are to evaluate the role, themes and literal devices used in fables to make them significant to children. It was a descriptive research done in the library. Purposeful sampling was used to select three fables. These were: *Ngiri Mganga* (2010) by Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) by Nyakeri and *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) by Mayega. Data was collected and analyzed according to research questions and objectives. The research was guided by two theories; semiotic and narratology, whose scholars are Pierce (1977) and Prince (2003) respectively. The Semiotic theory analyzes the meaning of the fables to children. It depicts the roles they play in educating chidren. Fables are themed to relay specific lessons to children. The narratology theory describes the style used by the writer. Writters ensure fables are written in a manner that enables childern to understand them easily. The role of animal characters in children's literature is explained. The findings were described and summarized. The importance of fables to children is explained. The research is beneficial to authors, university students and any one else interested in children's literature.

## ISTILAHI MUHIMU

**Dhima**: Wajibu mkubwa au uwezo wa kufanya jambo.

**Hurafa**: Hurafa ni aina ya ngano ambazo wahusika wake ni wanyama. Utafiti umezingatia wanyama kama sungura, tembo, mbwa, sisimizi, ngiri, bundi, tumbili na fisi.

**Fasihi ya Watoto**: Aina ya fasihi iliyoandikwa kwa kuzingatia watoto kama hadhira lengwa.

**Mtoto**: Dhana mtoto ina utata katika kuieleza kwa sababu inaweza kuwa na maana mbalimbali. Katika utafiti huu mtoto ni binadamu ambaye akili na mwili wake haujakomaa. Muktadha wa utafiti huu umeonyesha ya kwamba mtoto anayelengwa ni wa umri wa miaka sita (7) hadi kumi na mitatu (13). Tucker (1981) ameeleza ya kwamba mtoto ni binadamu ambaye ana umri kati ya miaka saba aanzapo masomo katika shule ya msingi na miaka kumi na mitatu anapobaleghe.

## VIFUPISHO

**Eds**: Education

**uk.**: Ukurasa

**Ltd**: Limited

**Kur**: Kurasa

**MA**: Master of Art

**PhD**: Doctor of Philosophy

# YALIYOMO

UNGAMO .......... I
TABARUKU .......... II
SHUKRANI .......... III
IKISIRI .......... IV
ABSTRACT .......... V
ISTILAHI MUHIMU .......... VI
VIFUPISHO .......... VII
YALIYOMO .......... VIII
SURA YA KWANZA .......... 1
UTANGULIZI .......... 1
1.0 Usuli .......... 1
1.1 Suala la Utafiti .......... 5
1.2 Maswali ya Utafiti .......... 6
1.3 Malengo ya Utafiti .......... 6
1.4 Sababu za Kuchagua Mada .......... 6
1.5 Upeo na Mipaka .......... 9
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada .......... 10
1.7 Misingi ya Nadharia .......... 13
1.7.1 Nadharia ya Semeotiki .......... 13
1.7.2 Nadharia ya Naratolojia .......... 16
1.7.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Naratolojia .......... 17
1.8 Mbinu za utafiti .......... 18
1.8.1 Muundo wa utafiti .......... 18
1.8.2 Mahali pa Utafiti .......... 18
1.8.3 Sampuli Lengwa .......... 19
1.8.4 Ukusanyaji Data .......... 19
1.8.5 Uchanganuzi wa Data .......... 20
1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo .......... 20
1.9 Hitimisho .......... 20
SURA YA PILI .......... 22
DHIMA KATIKA HURAFA KWA WATOTO .......... 22
2.0 Utangulizi .......... 22

2.1 Dhima za Hurafa kwa Watoto ........ 22
2.1.1 Kuelimisha Maadili ........ 23
2.1.2 Kuonya ........ 26
2.1.3 Kuburudisha ........ 28
2.1.4 Kuelekeza ........ 33
2.2 Hitimisho ........ 34
SURA YA TATU ........ 36
MAUDHUI KATIKA HURAFA KWA WATOTO ........ 36
3.0 Utangulizi ........ 36
3.1 Maudhui ........ 36
3.1.1 Tamaa ........ 36
3.1.2 wizi ........ 39
3.1.3 Uzembe ........ 40
3.1.4 Umaskini ........ 41
3.1.5 Utamaduni ........ 42
3.1.6 Dhuluma ........ 44
3.2 Hitimisho ........ 46
SURA YA NNE ........ 47
MBINU ZILIZOTUMIKA KUWASILISHA DHIMA NA MAUDHUI ........ 47
4.0 Utangulizi ........ 47
4.1 Mbinu ........ 47
4.1.1 Mbinu ya Taharuki katika Hurafa ........ 48
4.1.2 Matumizi ya Methali katika Fasihi ya Watoto ........ 51
4.1.3 Matumizi ya Nahau katika Fasihi ya Watoto ........ 56
4.1.4 Ukariri ........ 58
4.1.5 Tanakali za Sauti ........ 59
4.1.6 Matumizi ya Tashbihi katika Hurafa ........ 61
4.1.7 Matumizi ya Taswira katika Hurafa ........ 63
4.1.8 Ukuzaji wa Lugha ........ 65
4.1.9 Nyimbo katika Hurafa ........ 67
4.1.10 Matumizi ya Picha katika Hurafa kwa Watoto ........ 71
4.1.11 Lakabu katika Hurafa kwa Watoto ........ 76
3.1.12 Mianzo na Miishio ya Hurafa kwa Watoto ........ 77

4.1.12.1 Mianzo ya Hurafa katika Fasihi ya Watoto ........ 78
4.1.12.2 Miishio ya Hurafa katika Fasihi ya Watoto ........ 78
4.1.13 Matumizi ya Usemi Halisi katika Fasihi ya Watoto ........ 80
4.1.14 Sauti ya Msimulizi katika Fasihi ya Watoto ........ 82
4.2 Hitimisho ........ 85
SURA YA TANO ........ 87
MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO ........ 87
5.0 Utangulizi ........ 87
5.1 Muhtasari wa Matokeo ........ 87
5.2 Mahitimisho ........ 92
5.3 Mapendekezo kwa Tafiti zijazo ........ 93
MAREJELEO ........ 94
VIAMBATANISHO ........ 98

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Usuli

Dhana ya mtoto ina utata katika kuieleza. Inaweza kufafanuliwa kwa kutegemea mwega wa mtoa maana hiyo. Utata unatokana na ukweli ya kwamba dhana mtoto inaweza kuwa na maana mbalimbali kutegemea sheria, dini, biolojia na mila. Mbiti (2011) anasema mtoto ni yule ambaye hajapashwa tohara kulingana na mila za Afrika. Kulingana na sheria ya Kenya, mtoto ni yule hajafikisha miaka kumi na minane. Kwa mujibu wa Tucker (1981) mtoto ni binadamu ambaye ana umri wa kati ya miaka saba aanzapo masomo katika shule ya msingi na miaka kumi na mitatu anapobaleghe. Utafiti umezingatia mtazamo wa Tucker (1981) unaoeleza ya kwamba mtoto ni yule anayesoma fasihi ya watoto katika shule ya msingi.

Kulingana na Akoleit (1990) na Mpesha (1995), fasihi ya watoto iliendelezwa kabla ya majalio ya wazungu. Hii ni fasihi ambayo ilipitishwa kwa njia ya masimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine na kuhifadhiwa katika kumbukizi za wanajamii. Kupitia fasihi hii watoto walifunzwa mengi kama vile maadili ya jamii, walielimishwa kuwa na bidii miongoni mwa mambo mengine. Hurafa zilisimuliwa watoto jioni na babu zao kabla ya kula chajio. Jambo ambalo liliwafanya watoto wasilale kabla ya chakula cha jioni kutayarishwa. Davies (1973) anasema fasihi ya watoto ni kazi ya kifasihi iliyokusudiwa hadhira ya watoto. Ngugi (2011) anakiri kwamba fasihi ya watoto nchini Kenya imekua na kushamiri katika miaka ya hivi karibuni. Umaarufu na kukua kwa fasihi hii kumesaidiwa kwa uandishi kama vile 'British Council' na 'Agha Khan Foundations'. Mradi mwingine uliosaidia kukua kwa fasihi ya watoto ni ule wa 'Tusome Vitabu' uliofadhiliwa na 'Care International' kwa kusaidia baadhi ya shule kufungua maktaba za vitabu

vya watoto. Maelezo haya yanaeleza fasihi ya watoto ni changa na inahitajika kukuzwa kiuandishi na kiuchambuzi.

Fasihi ya watoto huandikwa kwa kuzingatia majukumu mbalimbali. Haya ni kama kuadili, kuelimisha na kuonya. Majukumu hayo hulenga kuelekeza watoto kuhusu mienendo bora na kukashifu mienendo mibaya. Watoto huelimishwa kupitia kizazi kimoja hadi kingine, hurekebishwa tabia, huonywa na huongeza upeo na mafikira yao. Davies (1973) anasema ya kwamba, majukumu ya fasihi ya watoto sharti yapanue upeo na fikira ya mtoto kuhusu ulimwengu na jinsi ya kuishi kwa amani katika jamii. Kwa hivyo, kuhakiki hurafa kama kipera cha ngano katika fasihi ya watoto kutachangia kuwasaidia watoto.

Fasihi ya watoto ni fasihi maalum inayoandikwa kwa ajili ya watoto inaweza kuwa hadithi, ushairi, visa kale na maigizo. Fasihi simulizi ya watoto ni aina ya fasihi iliyoandikwa kwa kuzingatia watoto kama hadhira lengwa. Fasihi hii ya watoto ilikuwapo hata kabla ya kufika kwa wazungu Afrika, kama mali ya jamii, iliyopitishwa kwa masimulizi kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa mujibu wa Mpesha (1995) fasihi hiyo, ilihifadhiwa katika kumbukizi za fanani. Fasihi hii ilijumuisha nyimbo, mashairi, methali, vitendawili na ngano miongoni mwa tanzu za fasihi simulizi. Kupitia kwa fasihi hii watoto walifunzwa mambo mengi kama vile, maadili ya jamii na kuwa na bidii. Hunt (1994) anasema vitabu vya watoto huandikwa kwa sentensi sahili zile watoto wanaweza kuelewa.

Hurafa ni aina ya ngano ambazo wahusika wake ni Wanyama. Hurafa ni maarufu na hupendwa sana miongoni mwa hadhira changa kama watoto na vijana. Mbinu zinazotumiwa na wandishi wa hurafa huvutia watoto na huwapa motisha wa kuendelea kuzisoma. Kama vile mbinu ya taharuki na nyimbo. Finnegan (1970) anasema kwamba hurafa nyingi huhusu sungura, kobe,

buibui na wanyama wengine wakubwa kama tembo na husimuliwa na wanajamii wengi Afrika. Jamii hizo ni kama Wamasai, Wakikuyu, Wakisii, Wameru, Waluo na wengine. Kipury (1983) anasema miongoni mwa Wamasai hurafa huwa na wahusika wanyama wanaoishi miongoni mwa wanajamii kama mbwa, paka, ng'ombe, kondoo na wengine. Wanyama hawa wanajulikana kwa wanajamii. Bukenya (1997) amesema hurafa yoyote huipa jamii mwelekeo na ni kioo cha kuelekeza jamii kuzingatia maadili bora kama kuwa mwaminifu, mkarimu, mwenye busara na mwenye matumaini.

Hurafa kama kipera cha ngano katika fasihi simulizi huainishwa kama hadithi za kubuni na kufikiria kisa fulani. Kwa mujibu wa Wamitila (2006) ubunifu unaohusika hapa ni wa kijamii yaani kisa fulani kinatungwa na kupokezanwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hadithi hizi zinaitwa za mapokeo za kibunifu. Zamani zilihifadhiwa akilini mwa msimulizi lakini sasa zi naweza kuandikwa kwa tarakilishi au vitabuni.

Mifano mingine ya hadithi za kupokezanwa au kibunifu ni hekaya, istiara na visasili. Katika kazi hii hurafa zinazolengwa ni hurafa kuhusu wanyama kama tembo, sungura na wengine bali si wahusika mazimwi au majitu ambao ni viumbe wanaokuwa na sifa ambazo haziko kwa binandamu wa kawaida. Viumbe hawa huogopwa na watoto.

Wanyama wanaotumika kama wahusika huchukua nafasi ya mhusika binandamu. Kwa mujibu wa Ngure (2011) wanyama hawa wanatenda kama binandamu na hata hutoa sauti kama za binandamu. Umuhimu wa mnyama ni jinsi anavyoweza kuaibishwa anaporekebishwa na kuelekezwa. Jina la mnyama litatajwa hata ingawa anayeelekezwa ni binadamu. Hadhira hufurahia jambo hili na huchangamsha watoto sana. Jambo hili huvuta watoto kupenda na kufurahia hurafa. Ngure (2011) amesema katika hurafa nyingi, fisi ni kiwakilishi cha ulafi,

upumbavu, ubinafsi na kutowajibika, vilevile sungura ni kielelezo cha werevu na busara, ingawaje sungura anadanganya tunajitambulisha naye kwa sababu anafanya hivyo kwa busara na kwa hekima kubwa kiasi cha kuwapiku wanyama wakubwa. Jambo linalowapa watoto moyo wanaposhindana na watu wakubwa.

Hurafa husawiri aina mbalimbali za maudhui. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (2011) maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi ya fasihi. Katika hurafa maudhui yanayojitokeza ni ya tamaa, maadili, wizi, uzembe, kuburudisha, umaskini, dhuluma na uozo wa jamii. Maudhui ya kijamii hutambua matendo na tabia za wahusika wanyama zinazozingatia maadili na kuelekeza na kufunza tabia hizo. Tabia na matendo yanayoenda kinyume na maadili hukashifiwa, Kwa mfano, bidii kazini ilisifiwa na uzembe kukashifiwa. Kulingana na Ngure (2011) sifa kuu ya hurafa ni kumwezesha fanani na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida yangekuwa aibu kuyatamka hadharani. Hurafa humwezesha fanani kuongea kuhusu tabia za binadamu bila kumuudhi au kuonekana kama anamkashifu mmoja kati ya hadhira yake kwa mfano, katika hali halisi hakuna mtu angependa kuambiwa, “Wewe ni mjinga”, anapotaka kutoa ujumbe huu kwa watoto, yule fanani anaweza kutumia hurafa iliyo na mhusika mjinga kama “kondoo”. Ngure (2011) ameendelea kueleza ya kwamba matumizi ya wanyama humwezesha fanani kupigia chuku mambo yanavyotokea katika ulimwengu halisi wa wanaume na wanawake, nayo hadhira hufurahia chuku hiyo. Jambo ambalo linawavutia watu wazima na watoto.

Maudhui ya kuhifadhi utamaduni pia husawiriwa katika hurafa. Tamaduni za jamii zinahifadhiwa na kuendeleza utamaduni. Maudhui ya dhuluma husawiriwa katika hurafa. Unyanyasaji na utawala mbaya unajidhihirisha katika hadithi za watoto, pale ambapo wanahitaji

kutafuta mbinu za kuurekebisha uongozi mbaya pamoja na unyanyasaji. Mara nyingi wahusika wadogo kama Sisimizi katika hurafa hutumia busara kuurekebisha uongozi mbaya.

Dhima ya hurafa ni majukumu muhimu yanayotokana na hadithi za watoto. Kusimulia au kusoma kwa hadhithi huelezea kunakoambatana na utendaji. Sanaa ya utendaji huibuliwa kutoka katika bongo za watu na kutolewa katika miktadha maalumu. Sanaa hii hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Dhima kuu ya hurafa ni kuelimisha, kuelekeza na kuweka bayana mambo yanayothaminiwa na jamii. Farsi (1979) anasema wazee walikuwa na wajibu wa kuelimisha kizazi kipya. Kwa wakati huu kizazi cha wazee kinatokweka kwa kasi mno hivi kwamba imani na amali za jamii zilizosheheni katika hurafa zinasahaulika na kutoweka.

**1.1 Suala la Utafiti**

Utafiti huu umechunguza dhima za hurafa katika fasihi ya watoto. Uchunguzi umefanywa kubainisha dhima, maudhui na mbinu katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Uchunguzi ulichanganua hurafa katika vitabu teule vitatu. *Ngiri Mganga* (2010) cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Nyakeri. Kutokana na hadithi za watoto utafiti unalenga kuchunguza kama hurafa zina majukumu muhimu kwa watoto. Majukumu yale yamebainishwa ni ya kuelimisha, kuonya, kuburudisha na uadilifu. Maudhui ya hurafa huelekeza dhima kwa watoto. Mbinu hutumiwa ili kumwezesha mwandishi wa hadithi kuwasilisha ujumbe unaoeleweka na watoto. Uchunguzi wa mbinu muhimu kwa watoto katika hurafa zimechanganuliwa. Suala la utafiti limelenga kuthibitisha utendakazi wa hurafa kwa watoto. Uchanganuzi umeangalia dhima, maudhui na mbinu katika hurafa ambazo ni muhimu kwa watoto.

### 1.2 Maswali ya Utafiti

1. Ni dhima zipi zimebainishwa katika hurafa kwa watoto kupitia vitabu teule?
2. Ni maudhui yapi yamedhihirishwa kwa watoto katika vitabu teule?
3. Ni mbinu zipi zimetumiwa kuwasilisha dhima na maudhui kwa watoto katika vitabu teule?

### 1.3 Malengo ya Utafiti

1. Kubainisha dhima katika hurafa kwa watoto kupitia vitabu teule.
2. Kudhihirisha maudhui katika hurafa kwa watoto kupitia vitabu teule.
3. Kuchunguza mbinu katika hurafa zinazowasilishia watoto dhima na maudhui katika vitabu teule.

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti mwingi umefanywa kuhusu fasihi ya watoto. Akoleit (1990) na Weche (2000) wamefanya utafiti juu ya vitabu vinavyosomwa na watoto kwa jumla. Wengine kama Alembi (1991) na Okhoba (1995) wameshughulikia tanzu za ushairi wa watoto. Ngugi (2011) amechunguza ufundishaji wa fasihi ya watoto katika shule za msingi nchini Kenya. Fasihi ya watoto imeshughulikiwa lakini umuhimu wa hurafa kwa watoto wa umri wa miaka saba hadi kumi na nne bado haujafanywa. Kwa hivyo utafiti umechunguza wajibu mkubwa katika hurafa kwa watoto kwa kubainisha dhima, maudhui na mbinu zilizotumika.

Fasihi ya watoto ina tanzu nyingi kama bembelezi, vitendawili, na maigizo lakini utafiti huu umejikita katika kuchunguza dhima, maudhui na mbinu zilizotumika. Hurafa zilitumika kuelimisha watoto zamani. Watoto ni viongozi wa siku za usoni njia moja ya kutayarisha viongozi wa kesho wenye maadili ni kuwaelimisha. Majukumu yanayotekelezwa kwa watoto

katika hurafa ni muhimu kuchunguzwa kama yanaelimisha ili vitabu kuhusu hurafa vitumiwa kwa wingi katika shule za msingi.

Hurafa ni muhimu kwa sababu ya kutosahaulika kwa maudhui na ujumbe wake. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (2011) mara nyingi hurafa huwa na ujumbe katika nyimbo ambazo huimbwa na msimulizi pamoja na wasikilizaji wake na aidha huweza kupatikana katika methali hasa mwisho wa hadithi, zilizolengwa kuzitolea muhtasari hurafa nyingi. Hurafa hizo huwa muhimu kwa sababu zina maudhui maudhui na ujumbe unaoelekeza hadhira yake kuhusu maadili, maendeleo, kuhifadhi utamaduni na hatari ya dhuluma. Njogu na chimerah (2011) wameeleza hurafa huwa muhimu kwa sababu maudhui yanayoelezwa watoto huwa si mengi katika hadithi. Hii ni sababu mojawapo muhimu ya kutosahaulika kwa ujumbe katika hurafa. Kwa hiyvo dhima muhimu za hurafa hazitasahaulika kwa urahisi na watoto. Jambo ambalo limemfanya mtafiti kuchunguza umuhimu wa ujumbe wa maudhui na dhima za hurafa kwa watoto.

Njogu na Chimerah (2011) wamesema hurafa huwa maarufu miongoni mwa hadhira changa. Wanaeleza, zinakuwa maarufu kwa sababu zinasimuliwa kwa kutegemea chuku, nyimbo na vichekesho. Mbinu hizo hufurahisha. Haya madoido huwa gundi katika mabongo ya hasa wasikilizaji watendaji wanajijumuisha moja kwa moja katika utendaji wa baadhi ya vipochopocho hivi, basi vinaganda katika bongo zao, na kila mara wakivikumbuka, wanakumbuka mafunzo ya hurafa.

Hurafa ni muhimu katika kuelekeza na kurekebisha mienendo ya hadhira changa. Kinoti katika Nyaga (1997) amesema watoto wa kisasa hawazingatii maadili kama waliozingatia zamani. Anaendelea kueleza kwamba utovu wa maadili siku hizi umeongezeka miongoni mwa vijana. Nyaga anasema utovu huo wa maadili unasababishwa na athari ya vyombo vya habari, wazazi

kutoajibika na dini kuchukua nafasi ya kufunza badala ya fasihi simulizi. Kwa hivyo hurafa kama kipera cha fasihi simulizi ni mada muhimu.

Hurafa ni muhimu kwa sababu zimesawiri maudhui mbalimbali kama ya utamaduni, maadili ya wanajamii, dhuluma, utajiri na umaskini, tamaa na wizi. Bukenya na Gachanja, (1997) wamesema hurafa yeyote huipa jamii mwelekeo na ni kioo cha kuelekeza jamii kuzingatia maadili bora kama kuwa mwaminifu, ukarimu, busara na kutokosa matumaini.

Kwa mujibu wa Ngure (2011) hurafa zimedhihirisha majukumu muhimu katika kuelekeza dhima kama ushirikiano, maadili bora, ucheshi kwa watoto, kuonya watoto dhidi ya uozo wa jamii kuelekeza watoto kuhifadhi mila na desturi za jamii, watoto kuzingatia ukweli haki, na zingine. Hurafa zinaposimuliwa au kusomewa hadhira lengwa zinatahadharisha kujiepusha na matapeli, walaghai na wezi walio katika jamii. Hurafa ni muhimu kwa sababu humwezesha fanani na hadhira yake kusema mambo ambayo kwa kawaida yangekuwa muhali au aibu kuyatamka hadharani. Ngure (2011) amehimiza hurafa ni maarufu na hupendwa sana miongoni mwa hadhira changa au vijana.

Kulingana na M’Ngaruthi (2008) hurafa ni muhimu kwa sababu katika fasihi ya watoto hadithi za watoto zimeandikwa zikiwa na wahusika wanyama. Wahusika hawa wamepewa aghalabu sifa na uwezo wa kutenda mambo kama binadamu. wanyama hawa huwakilisha binadamu na hutumiwa kutolea funzo kuhusu binadamu walio na tabia sawa na wanyama hawa. Mafunzo kwa watoto ambao wanatakiwa kuelekezwa kuhusu maadili yanayotarajiwa katika jamii ni muhimu. Kwa hivyo hurafa ni muhimu katika fasihi ya watoto.

M’Ngaruthi (2008) ameeleza zaidi ya kwamba hurafa kama kipera za fasihi simulizi ni maalumu kushutumu na kukejeli waliokosa kwa jamii. Njia mwafaka ni muhimu kuchunguza ya kukashifu

mienendo isiyofaa miongoni mwa watoto. Watoto wakirekebishwa mapema kizazi kijacho kitazingatia uadilifu na amani. Kwa hivyo mada ya utafiti inafaa ili kuchunguza umuhimu wa hurafa katika kukashifu, kukejeli na kushutumu watoto wanaokosa.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Kuna vitabu vingi kuhusu hadithi za watoto juu ya hurafa vile vingetumika kama sampuli katika utafiti huu. Vitabu vile vimechaguliwa ni *Ngiri Mganga* cha Kariuki (2010), *Sungura na Mbwa* cha Nyakeri (2011) na *Sisimizi Amuua Tembo* cha Mayega (2004). Vitabu hivi vimechaguliwa kwa sababu vinalenga kuelimisha watoto majukumu mbalimbali. Hayo ni kama maadili bora, kuonya, kuburudisha na kuadili.

Fasihi ya watoto ina tanzu nyingi ambazo pia zina vipera mbalimbali. Kuna ngano za kihalisia na kifantasia. Hurafa ni utanzu wa ngano za kihalisia. Kuna viwango mbalimbali vya elimu nchini kenya. Katika shule za msingi kiwango cha chini zaidi ni chekechea. Pia kuna darasa la kwanza hadi la tatu. Watoto wa darasa la nne hadi nane wako katika kiwango cha shule ya msingi. Baada ya kiwango kinachofuata ni shule ya upili. Utafiti huu umechunguza jinsi hurafa zinavyofaidi watoto wa miaka saba hadi kumi na nne katika shule ya msingi. Hawa ni watoto katika darasa la kwanza hadi la nane.

Kuna vitabu vingi vya fasihi ya watoto. Vile vimetumika vimehusu hurafa ambavyo ni *Ngiri Mganga* (2010) cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Nyakeri. Maswala mengi yangeshughulikiwa lakini maswali ya utafiti yamehusu uchunguzi wa dhima, maudhui na mbimu zilizotumika katika vitabu teule vya watoto.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Cass (1967) amechunguza kuhusu umuhimu wa matumizi ya picha na michoro katika vitabu vya watoto. Ameeleza ya kwamba michoro na vielelezo vinafaa vitumiwe kwa njia ambayo itachangia mtoto kuelewa ujumbe wa hadithi anayosoma. Rangi zinazopakwa picha zinatakiwa kuvutia watoto. Kuelewa kwa mtoto kuhusu picha na vielelezo kunategemea umri wa mtoto. Uchunguzi wa Cass (1967) umeangalia picha na vielelezo katika vitabu vya watoto bali wetu umechunguza picha kama mbinu moja iliyotumika na wandishi wa hurafa ili kuwasilisha ujumbe wa maudhui kwa watoto. Malengo ya utafiti wetu ni kuchunguza dhima, maudhui na mbinu katika hurafa tofauti na ya Cass (1967).

Holder (1981) amechunguza hurafa za Aesops. Ameeleza hurafa za Aesops zilikuwa maarufu miongoni mwa Wafaransa na ndiyo sababu zimetafsiriwa kwa Kiingereza. Hurafa hizo zilihusu wanyama wanaojulikana na jamii na wanapendwa na watoto. Usimulizi wa Aesops kulingana na Holder ulilenga kuburudisha watoto na kuwaongoza kuhusu maadili. Alikuwa na matokeo kwamba hurafa *Sungura na kobe* ilibainisha maadili ya utaratibu. Hurafa ya *Punda na Panzi*, inasisitiza nyama ya mtu mmoja inaweza kuwa sumu ya mtu mwingine. Hurafa za Aesops ni muhimu katika jamii ya Ufaransa miongoni mwa watoto. Utafiti dhima za hurafa katika fasihi ya watoto umelingana na uchunguzi wa Holder (1981) lakini mazingira ya utafiti wetu ni tofauti si ya Wafaransa.

Benton na Fox (1985) wamechunguza upokezi wa watoto katika tanzu za hadithi na ushairi. Matokeo ya uchunguzi wao ni kwamba watoto hupenda kujinasibisha na watu wakubwa kuliko wao. Pia wanaeleza upokezi wa watoto hutegemea tajriba, umri, uzoefu na mazingira yake. Utafiti unalingana na huu kwa sababu umeshughulikia hadithi katika fasihi ya watoto. Tofauti ni

kwamba hauchunguzi dhima za hurafa katika fasihi ya watoto. Mazingira ya utafiti wao si wa Kenya lakini ni ya Kiafrika nchini Kenya.

Gituku (1990) ametafiti kuhusu fasihi ya watoto. Alichunguza maigizo ya kienyeji ya watoto. Alibainisha jinsi watoto wanavyoigiza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi. Katika uchunguzi wake alitaka kutathmini ni utanzu upi wa fasihi simulizi uliwavutia watoto kuliko tanzu zingine. Nadharia iliyoongoza utafiti wake ni ya utendakazi. Alilinganisha jinsi watoto wa miaka mitano hadi kumi na mitatu walivyoigiza tanzu kama vitendawili, utambaji ngano, ukariri wa mashairi na uigizaji wa nyimbo. Alipochanganua uigizaji uliofanywa na wengi, aligundua vikundi vingi vya watoto viliigiza vitendawili kuliko tanzu zingine. Utafiti huu wa Gituku unalenga tanzu zote za fasihi simulizi bali utafiti wetu umelenga kuchunguza jinsi hurafa zinavyowasilisha dhima na maudhui kupitia mbinu mbalimbali kwa watoto.

Alembi (1991) ametafiti kuhusu mashairi na nyimbo katika fasihi ya watoto. Amechunguza tanzu za nyimbo na mashairi ili kubainisha umuhimu wa tanzu hizo katika kuelimisha watoto maadili yanayokubaliwa katika jamii. Utafiti wake umeangalia nyimbo na mashairi ya Wanyore, mojawapo ya lahaja za Kiluhya tofauti na utafiti wetu unaochunguza dhima za hurafa za Kiswahili kwa watoto.

Okhoba (1995) ametafiti maudhui ya kujiburudisha kwa watoto katika mashairi. Amechambua ushairi simulizi ambao ni kipera cha fasihi simulizi katika fasihi ya watoto. Uchunguzi wake umejikita katika utanzu wa ushairi lakini wetu unahusu dhima za hurafa zilizoandikwa vitabuni.

Ruthiiri (2012) alitafiti kuhusu fasihi ya watoto. Alichunguza ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya 5 na ya 6 katika shule za msingi. Uhakiki uliongozwa na nadharia ya kimtindo.

Utafiti unalingana na huu kwa sababu umechunguza kuhusu vitabu vya fasihi ya watoto katika shule za msingi. Tofauti ni kwamba wetu unachunguza dhima, maudhui na mbinu katika hurafa kwa watoto wa darasa la kwanza hadi la nane.

Wood (2014) ametafiti kuhusu hurafa za watoto. Katika maelezo yake amehimiza umuhimu wa hurafa zinazosawiri maudhui ya furaha. Maudhui ya furaha ni kinyume na maudhui ya huzuni yanayosawiriwa katika hadithi za watoto. Maudhui ya kukosa matumaini na kutamausha kupitia wahusika huhuzunisha. Wood anaeleza kupitia maudhui ya furaha watoto huelekezwa maadili bora kuliko maudhui ya huzuni. Wood anaeleza zaidi, hadithi zenye furaha huwapa watoto motisha ya kuziiga tabia za wahusika katika hurafa. Wood ameeleza umuhimu wa hurafa zinazosawiri maudhui ya furaha ambazo ni mwafaka kuelekeza watoto. Tofauti na utafiti huu, unaolenga kuchunguza dhima zote za hurafa kwa watoto zikiwa pamoja na maudhui ya furaha.

Akinyi (2018) amefanya utafiti kuhusu ngano za kifantasia miongoni mwa watoto. Alichunguza na kubaini ya kwamba watoto walifurahi kuishi kwa amani na upendo. Vilevile watoto wana uwezo wa kuhimiza uadilifu. Akinyi (2018) amechunguza ngano za kifantasia lakini utafiti huu umeangalia hurafa ambazo ni za kihalisia.

Utafiti huu umechunguza ya kwamba hurafa katika fasihi ya watoto hutekeleza dhima mbalimbali. Watoto wanaposoma hurafa wanafaidika kwa njia yoyote katika jamii? Majukumu muhimu kwa watoto yamechunguzwa kutokana na dhima, maudhui na mbinu katika hurafa.

Tafiti zimefanywa kuhusu fasihi ya watoto zikichunguza tanzu mbalimbali za fasihi simulizi ya watoto. Kama vile Akoleit (1990) , Gituku (1990) , Alembi (1991), Kairu (2005), Ngugi (2009), Ruthiiri (2012) na Akinyi (2018) . Tafiti hizo zimechangia uchunguzi wa tanzu mbalimbali

katika fasihi ya watoto. Zimechunguza maudhui na mtindo, uhakiki na upokezi wa fasihi ya watoto, usawiri wa wahusika na jinsia tofauti na utanzu wa nyimbo za watoto. Utafiti wetu unachangia umuhimu wa hurafa katika masomo ya watoto wa miaka saba hadi kumi na nne. Hawa ni watoto katika shule za msingi. Pia utafiti umekuwa na malengo ya kuchunguza dhima, maudhui na mbinu zilizotumika katika hurafa kuwasilishia watoto dhima na maudhui.


## 1.7 Misingi ya Nadharia

Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni mbili. Nadharia ya semeotiki na nadharia ya naratolojia. Nadharia ya semeotiki iliasisiwa na Pierce (1977). Anaeleza kwamba nadharia ya semeotiki inaangazia suala la uashiriaji, jinsi kazi zinavyowasiliana na wasomaji na maswali kama maana iliyofasiriwa na kazi ya fasihi. Nayo nadharia ya naratolojia ilihakiki hadithi za watoto kutegemea usimulizi na mbinu zilizotumiwa na waandishi wa hurafa. Prince (2003) ambaye ni mwasisi wa nadharia ya naratolojia amesema usimulizi au uandishi wa kazi ya fasihi hutegemea usanaa wa msimulizi au mwandishi wa hadithi. Wandishi wa hurafa hutumia mbinu mbalimbali kama taharuki, methali, nahau. Jazada, lakabu na nyinginezo ili kueleweka kwa usimulizi wao. Mihimili yote ya nadharia zote mbili imetumika.

### 1.7.1 Nadharia ya Semeotiki

Semeotiki ni neno la lugha ya kiyunani ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo ya makundi fulani. Mielekeo hiyo inahusu jinsi jamii husika zinachukulia maana ya kazi ya fasihi kwa hadhira. Mwasisi wa nadharia hii ambaye ni Pierce (1977) anaeleza ya kwamba kazi ya fasihi huashiria ishara zenye maana kulingana na utamaduni na uhakiki wa msomaji. Mwasisi Pierce (1977) anaeleza ishara hutumiwa kufafanulia vitendo maalumu.

Historia ya nadharia inahusishwa kwa kiasi kikubwa na miaka ya 1970. Wakati huo kulikuwa na mwelekeo mkubwa kuuasi na kuuacha umuundo ambao ulikuwa umetawala wahakiki wa kifasihi katika miaka ya 1960. Uhakiki wa umuundo ulihakiki kazi ya fasihi kulingana na maudhui na sio kwa kuangalia  utamaduni na uhuru wa mhakiki. Pierce (1977) amehusishwa na kielelezo cha ishara kinachohusishwa na pembe tatu Wamitila, (2006). Kielelezo (a) kinachofuata kimetumiwa kuzipa maana hadithi za watoto kulingana na maoni ya utamaduni wa msomaji.




**Kielelezo (a)**: Pembe za kilelezo cha ishara (Wamitila, 2006 :132)

Katika kielelezo (a) Pierce (1977) anaashiria kila ishara huwa na yambwa au kitendwa kinachorejelewa katika akili ya anayefasiri ishara hiyo. Hii inaweza kutazamwa kama ishara ya pili. Kwa mfano, ikiwa mtu anakuonyesha sungura aliyelala mahali fulani, ile ni ishara ya ‘Sungura’ katika lugha yako au tabia ya ujanja au udanganyifu kulingana na utamaduni wa jamii

hiyo. Mihimili ya nadharia ya semeotiki inaotumika katika utafiti inatokana na mwasisi Pierce (1977). Pierce anahimiza jinsi hadithi zina umuhimu katika kazi ya fasihi.

1 Nakidi wa ishara hufanyika katika utamaduni mahususi ambapo mifumo yake inajulikana, inatumiwa na kufahamika na wanajamii waliolelewa katika utamaduni huo maalumu. Hadithi za watoto huwa na ishara ambazo huzingatia utamaduni wa jamii husika katika utafiti wetu.

2 Katika kazi ya fasihi, semeotiki huliangaza suala la uashiriaji na huakiki jinsi kazi hizo zinavyowasiliana na wasomaji. Ujumbe wa hadithi umelengewa kazi ya watoto.

3 Nadharia hii haifasiri tu jinsi tunavyoifasiri kazi ya fasihi tu, bali pia usomaji wetu wa kazi. Msomaji hujiuliza kwa nini kazi ya kifasihi huwa na maana zilizonazo kwa wasomaji wake.

Uchunguzi wa maudhui na dhima katika hurafa unahitaji kuzingatia mihimili yote ya nadharia ili kuchunguza umuhimu wa hurafa kwa watoto. Hata hivyo, nadharia ya pili imetumika ili kuhakiki mbinu za mwandishi au msimulizi wa hurafa.

Nadharia ya pili ni muhimu kwa sababu nadharia ya semeotiki ilitumika kuzipa maana hadithi za watoto na kupata umuhimu wa hadithi kwa watoto kulingana na utamaduni, jinsi kazi ilivyoashiriana na maana anayoipa msomaji. Nadharia ya semeotiki haiwezi kutumiwa pekee kwa sababu usimulizi wa hurafa na jinsi umeandikwa na mwandishi ni muhimu. Kwa hivyo, nadharia ya naratolojia imetumika ili kuchanganua usimulizi na uandishi wa hurafa ulivyotumika kuwasilisha maudhui na dhima kwa watoto. Nadharia ya pili ambayo ni naratolojia ni muhimu katika kazi hii ili kuhakiki usimulizi na uandishi wa mwandishi kupitia mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizo ni za matumizi ya lugha zikiwa methali, tanakali za sauti na tashbihi.

Zingine ni taharuki, picha, nyimbo, majazi, matumizi ya taswira, mbinu ya utangulizaji na uhitimishaji wa hurafa, matumizi ya usemi halisi na sauti ya msimulizi.

### 1.7.2 Nadharia ya Naratolojia

Nadharia ya naratolojia inahusika na simulizi. Kwa mujibu wa Prince (2003) simulizi ni uelezaji wa tukio moja au mengi ya kihalisi au kibunilizi. Nadharia ya naratolojia ina historia inayoeleza ya kwamba ilianza mwaka wa 1966 nchini Ufaransa. Mkondo mmoja wa nadharia hii kulingana na Wamitila (2006) ni kwamba imewekwa msingi na mawazo ya mwanafalsafa wa Kiyunani, Plato ambaye alilinganua usimulizi na udhihirishaji. Genette (1999) alichukua mkondo wa kueleza usimulizi kwa kurejelea mambo matatu. Kwanza, kuelezea kauli ya kisimulizi au kimaandishi au isiyo ya kimaandishi iliyodhamiriwa kulielezea tukio au matukio. Anaeleza dhana hii kama simulizi. Pili, mfano wa matukio halisi au kibunilizi ambayo ni kiini au yanalengwa na usemi fulani. Dhana hii akaeleza kama hadithi au daigesia. Tatu, kuelezea tendo lenyewe la kusimulia au usimulizi, akirejelea dhana hii kama usimulizi.

Kwa mujibu wa Wamitila (2006) mtaalamu wa Kirusi Vladimir Propp alikuwa mwasisi aliyehusishwa zaidi na nadharia ya naratorojia ya kisasa. Propp alichukua mkondo wa kuchunguza hurafa zaidi ya mia moja na kutambua mfuatano maalum na kuwa na majukumu kwa jamii. Propp anayatambua matukio mbalimbali ya hurafa. Matukio ya hurafa ni kwamba hulenga kuelimisha, kuadili na kuburudisha. Jambo muhimu katika nadharia hii ni kwamba matukio fulani yanaweza kuwasilishwa kwa jinsi mbalimbali. Inamhusu Mwana naratolojia kukichunguza kilichosimuliwa, matukio yaliyosimuliwa na usimuliaji wenyewe na njia iliyotumiwa pamoja na ufanisi wake.

Kulingana na waitifaki kama Propp, Plato, Genette na Prince nadharia hii ilichukuliwa kama mtazamo wa jumla kuhusu usimulizi wa aina mbalimbali katika mtindo wa kusimulia na muundo wa vitushi. Prince (2003) aliangalia usimulizi na usanaa wa uandishi wa hadithi katika kazi ya fasihi .

#### 1.7.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Naratolojia

1. Hadithi au simulizi ni mfululizo wa matendo kwa utaratibu jinsi yanavyotukia kiwakati bila kuacha chochote. Prince (2003) ameeleza hadithi kama usimulizi wa mwandishi uliotumia mbinu mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe wa maudhui. Uchanganuzi unazingatia mbinu zilizotumiwa katika hurafa ili kuteua maudhui na dhima kwa watoto.

2. Hadithi hutambwa au husimuliwa kwa njia mbalimbali kwa mfano moja kwa moja (nathari). Pia matukio yanayosimuliwa huweza kusimuliwa baada ya kutokea.

3. Hadithi inachanganuliwa kwa mkabala wa kimtazamo. Mhakiki wa hadithi anapenya kwa kiwango gani kuchunguza hadithi? Hili hujibu swali mkabala wa kimtazamo. Hadithi inasimuliwa kutoka mtazamo wa aina gani? Kuna aina mbili za mkabala wa kimtazamo. Kuna mtazamo wa nje na mtazamo wa ndani. Mtazamo wa nje unaangazia matendo na maneno ya mhusika. Kwa mfano, mbwa alilima (tendo) kwa mtazamo wa ndani unaangazia kile ambacho mhusika anafikiri na kuhisi. Kwa mfano tumbili alifadhaika (hisi). Mitazamo yote ilitumika katika uchanganuzi wa hurafa. Kwa mfano, sungura anaelezwa na msomaji akiwa mlafi kutokana na matendo ya kutaka chakula kingi. Huo ni mtazamo wa nje. Maoni hayo yanatokana na mtazamo wa ndani au mafikira ya msomaji.

4. Sifa ya usemi katika hadithi inachanganua jinsi usemi na mawazo yanavyowasilishwa. Utambaji unaweza kutumia . Mwandishi wa hurafa husimulia au huandika hadithi kwa kutumia usemi halisi au usemi wa taarifa. Usemi uliotumiwa hutumika kujenga tabia za wahusika wa hadithi. Usemi halisi unatumika kuhakiki maudhui na dhima muhimu kwa watoto kutokana na matamshi ya wahusika katika hurafa.

5. Tukio au usemi umerudiwa mara ngapi katika usimulizi ili kupasha ujumbe muhimu. Msimulizi ameeleza na kurudia maneno kwa kiasi gani kama uradidi. Urudiaji unachunguza mbinu ya uradidi iliyotumiwa na mwandishi wa hurafa ili kuwasilisha ujumbe kwa watoto.

## 1.8 Mbinu za utafiti

Utafiti ulifanywa katika maktaba na ulitegemea upekuzi wa nyaraka, vitabu, magazeti, majarida, tasnifu na aina nyingine ya maandishi. Kutokana na upekuzi na uchambuzi wa maandishi, mtafiti aliweza kutafuta habari muhimu zinazohusiana na mada ya utafiti.

### 1.8.1 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999) utafiti wa kimaelezo ni ule ambao hutegemea maelezo katika uwasilishi na uchanganuzi wake. Ufafanuzi wa maelezo hugawanywa katika vikundi kutegemea dhana na vigezo katika maswali ya utafiti. Maelezo yametumika katika uchanganuzi na kuandika matokeo.

### 1.8.2 Mahali pa Utafiti

Mtafiti amesoma vitabu vya watoto, vitabu kuhusu nadharia na majarida na vyote vilivyomsaidia kuandika utafiti huu katika maktaba. Usomaji na upekuzi mwingi wa vitabu ulifanyiwa maktabani.

### 1.8.3 Sampuli Lengwa

Vitabu vya hadithi za watoto kuhusu hurafa vimeteuliwa kimakusudi. Uteuzi wa kimakusudi ni ule wa kuteua sampuli inayotumika pekee. Uteuzi wa vitabu vya watoto kuhusu maudhui yanayofunza watoto maadili mema yamechaguliwa. Maadili haya ni kama uvumilivu, huruma na kuridhika. Wizi, tamaa, udanganyifu unakashifiwa. Maudhui yale yanawafunza na kuelekeza watoto mienendo inayofaa kwa jamii ndiyo yameteuliwa kimakusudi. Uteuzi wa kimakusudi ni mbinu ya kutoa sampuli wakilishi kutokana na idadi kubwa ya watu, au vitu ambavyo haviwezi kuchunguzika vyote pamoja Palinkas (2015). Mbinu hii ilimwezesha mtafiti kupata maudhui katika hadithi za watoto bila kupoteza muda na kuchunguza hadithi za watoto ili kueleza dhima kutokana na hurafa. Pia kuchunguza na kubainisha mbinu zilizotumiwa kuwasilisha maudhui na dhima katika hurafa.

### 1.8.4 Ukusanyaji Data

Data imekusanywa katika vitabu teule. Navyo ni *Ngiri Mgang*a (2010) cha Kariuki *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Mayega. Dondoo kutoka hurafa liliandikwa kuchunguza dhima, maudhui na mbinu muhimu kwa watoto. Mbinu zilizotumiwa kuwasilisha ujumbe wa maudhui kama dhima zilielezwa. Mihimili ya nadharia ya semeotiki ueleza msomaji yeyote wa kazi ya fasihi anabidi kuwa na maana ya kazi ya fasihi kwa walengwa wake. Maudhui yenye majukumu kwa watoto yalidondolewa kwa njia ya maelezo. Kulingana na Pierce (1977) nadharia ya semeotiki husisitiza msomaji wa hurafa anatakiwa kutafsiri maana inayolengewa watoto kwa jamii. Nadharia ya naratolojia huhakiki jinsi usimulizi ulivyosimuliwa au kuandikwa na mwandish. Kama vile matumizi ya lugha, taharuki, uradidi, nyimbo, sauti ya msimulizi, picha na zingine.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (1999), uchanganuzi wa data huenda sambamba na ukusanyaji wa data. Data imepangwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti. Lengo la kwanza lilikuwa kukusanya matini ya kuchunguza dhima kwa watoto. Data kuhusu ujumbu wa maudhui kwa watoto ilidondolewa katika hurafa teule : *Ngiri Mganga, Sungura na Mbwa na Sisimizi Amuua Temb*a. Nadharia ya semeotiki husisitiza ya kwamba hadithi katika kazi ya fasihi zinastahili kuelimisha wasomaji mienendo bora. Mwisho data ilipangwa na kuchunguzwa kuzingatia malengo ya utafiti. Nadharia ya naratolojia huangalia usimulizi wa hadithi; jinsi msimulizi au mwandishi alivyotumia mbinu mbalimbali ili kueleweka na msomaji au hadhira. Kwa hivyo mbinu zilizotumiwa katika hurafa zilichanganuliwa kubainisha umuhimu kwa watoto.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Baada ya ukusanyaji na uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo umefanywa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji huu umehusu kuandika kinathari maudhui kutokana na matini iliyodondolewa katika hurafa. Matokeo ya uchanganuzi wa maudhui ili kupata dhima pia yameandikwa kinathari. Maelezo ya jinsi mwandishi alivyoandika hurafa yalizingatia mbinu mbalimbali zilizotumiwa kuwasilisha dhima kwa watoto. Kulingana na nadharia ya naratolojia, jinsi mwandishi alivyosimulia hadithi ni muhimu ili ieleweke na wasomaji au hadhira. Mbinu zilizotumiwa kuwasilisha maudhui na kuelekeza dhima kwa watoto zilielezwa na kuandikwa kinathari. Maelezo ya matokeo yote yaliandikwa kinathari.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii ni msingi wa utafiti ulioshughulikia usuli wa mada, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada,

misingi ya nadharia, nadharia ya semeotiki, nadharia ya naratolojia, muundo wa utafiti, mahali pa utafiti, sampuli lengwa, ukusanyaji data, upangaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo ya data. Msingi huu ni muhimu katika utafiti. Sura inayofuata imechunguza dhima za hurafa kwa watoto kupitia vitabu teule.

# SURA YA PILI

# DHIMA KATIKA HURAFA KWA WATOTO

## 2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia usuli, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Sura hii imechunguza dhima za hurafa kwa watoto katika vitabu teule. Navyo ni: *Ngiri Mganga* (2010) cha Kariuki *Sungura na Mbwa* (2011*)* cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004*)* cha Mayega. Nadharia ya semeotiki iliyoasisiwa na Pierce (1977*)* imetumika kuchanganua data. Maana ya hurafa huakikiwa kulingana na maana ya msomaji na utamaduni wa jamii husika. katika hurafa za watoto, mwandishi huhimiza kuelimisha mienendo bora katika jamii. Nadharia ya semeotika pia husisitiza ya kwamba kazi ya fasihi inalenga kuwafaidi wasomaji wa vitabu vya fasihi. Kwa hivyo, utendakazi wa hurafa kwa watoto huelekeza dhima ambazo ni muhimu maishani mwa watoto. Dhima mbalimbali zimechanganuliwa kama vile ya kuonya watoto, kuburudisha, kufunza maadili na kuelimisha watoto.

## 2.1 Dhima za Hurafa kwa Watoto

Kwa mujibu wa Ngure (2011) dhima ni wajibu mkubwa au uwezo wa kufanya jambo. Hurafa zina dhima kuu ya kuelimisha jamii. Isitoshe, amesema ya kwamba hurafa ni njia mojawapo ya kufunzia maadili na amali za jamii. Ngugi (2009) na Rosenblatt (1995) wamesema watoto wanaposoma vitabu vyao wanatekelezewa dhima mbalimbali kama kuburudisha na kuelimishwa. Dhima za hurafa ni muhimu katika fasihi ya watoto. Wamitila (2003) ana maoni kuwa hurafa hupendwa sana miongoni mwa hadhira changa na hutekeleza dhima kwa watoto. Kwa mujibu wa Pierce (1977) uchanganuzi uliyobainishwa katika hurafa huthibitisha dhima kwa watoto.

Akifafanua zaidi Pierce (1977) amesisitiza kuwa nadharia ya semeotiki huashiria msomaji wa fasihi kutambua umuhimu wa hadithi kwa jamii.

### 2.1.1 Kuelimisha Maadili

Maana ya kuelimisha kulingana na TUKI (2004) ni kupatia mtu elimu au kufundisha. Hurafa huwasilisha dhima ya kuelimisha madhara kama ya wizi, udanganyifu, uzembe na kuwa na tamaa. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (2011) hurafa huelimisha kwa ujumbe unaotolewa kama kimalizio cha tungo mwisho mwa hadithi. Uchanganuzi unazingatia maana iliyobainishwa na ujumbe wa maudhui kwa watoto. Nadharia ya semeotiki kupitia mihimili yote inasisitiza ya kwamba uhakiki wa kazi ya fasihi unabidi kuwa wa manufaa kwa jamii. Msomaji mtoto anaelekezwa maana ya hurafa inayoelimisha.

Hornby (2012) ameeleza ya kwamba maana ya maadili ni tabia au mienendo inayokubalika na jamii, dini, utamaduni au na wengi kuwa bora au mibaya. Maadili kama mienendo inayokubaliwa na jamii inastahili kuzingatiwa na kuigwa. Mabaya hayafai kutendwa au kuigwa. Maadili ni muhimu kwa jamii. Maadili yanatakiwa kuzingatiwa kulingana na kanuni za jamii. Ngure (2011) na Wamitila (2003) wameeleza ya kwamba dhima muhimu ya hurafa ni kutekeleza dhima ya kufunza maadili. Ngure (2011) ameeleza zaidi na kusema hurafa ni njia ya pekee ya kufundishia watoto maadili na amali za jamii. Hurafa hutekeleza dhima ya kuelimisha maadili kama ilivyo katika *Ngiri Mganga* cha Kariuki (2010):

> Usikate tamaa mke wangu," Chura Kahawia alimtuliza mkewe," na sisi pia, Mungu hatimaye atatujalia watoto wazuri wa kutufaa," "Siku moja Kahawia na mkewe walijaaliwa mtoto wa kiume. Furaha iliyokuwa nyumba hiyo haina kifani usiku huo, Kahawia na mkewe walikoroma na kupiga binja mmoja baada ya mwenzake hadi alfajiri. Walitaka ulimwengu wote upashwe habari hiyo (uk.8).

Kulingana na dondoo chura kahawia alituliza mke wake. Alimwomba asikose matumaini na subira kwani siku moja Mungu atawajalia watoto. Mungu aliwajalia mtoto wa kiume na walifurahi sana. Uashiriaji wa maana ya hurafa hiyo ni muhimu kwa watoto. Maana hiyo ni ya kwamba usomaji unawaelekeza watoto kung'amua umuhimu wa kuwa na subira na matumaini. Kariuki (2010) ameonyesha ya kwamba chura Kahawia walikuwa na subira na matumaini ya kupata mtoto na walijaliwa mtoto baadaye. Maadili ya subira na matumaini yanafunzwa kwa watoto. Hurafa iliyohusu chura aliyeitwa Kahawia na mke wake inadhihirisha siku moja walijaliwa mtoto na kwa kufurahi walipiga mbija hadi alfajiri. Kwa hivyo hurafa hutekeleza dhima ya kuelimisha maadili kama subira na kuwa na matumaini maishani. Jukumu hili pia limebainika katika hurafa ya Kariuki (2010). Amesema:

> Wazo lingine likamjia awapange wanawe namna nyingine ili kuwatia kiwewe ambacho labda kingewavuruga akili na kuwafanya waruke mbele. Alimchukua shoto na kumpanga upande wa kulia wa dada yake labda akimuona dadake upande huo angekosa kwa kurukia na kupinda upande wa mbele. Vilevile kulia akimuona ndugu yake upande ambao ndiyo kawaida yake kurukia, angeelekea mbele. Mambo yalikuwa yamepamba moto, na jamii ya mfalme ilikuwa na hamu ya kujionea lingelotukia. "mko tayari?" Hopa aliuliza jamii ya Kahawia. "Tuko tayari," alijibu Kahawia na mkewe huku wakirudi kwenye umati. "Rukeni" Hopa aliamuru kwa sauti kubwa. Jamii ya mfalme ilingojea kwa matumaini makubwa. Hali ya taharuki na wasiwasii ikitanda kwenye umati. Wana wa Kahawia waliruka ajabu. Umati ulichangamka na mfalme akadhani kuwa jamii ya Kahawia ilikuwa imefanya mazoezi ya muda mrefu. Makofi, nderemo na vigelegele viliendelea kwa muda kwani tukio kama hilo lilikuwa halijawahi kuonekana mashindanoni. Majina ya shoto, kulia na Bakari yalivuma sana katika nchi ya Vyura na kuiletea jamii yao sifa na fahari (Uk.21).

Katika dondoo hili watoto wa vyura Kahawia walitakiwa kuhuhudhuria sherehe ya mashindano ya urukaji. Watoto wote wa jamii ya vyura walitakiwa kuhudhuria mashindano hayo. Chura Kahawia alihangaika jinsi watoto wake watakavyoruka kwa sababu walikuwa na upungufu wa urukaji. Chura Kahawia akaamua kuwapanga watoto wake wote waweze kuruka pamoja. Waliporuka walifurahisha umati na wakashangiliwa mno. Waliibuka washindi. Chura kahawia

alikuwa hana hakika kama watoto wake wangeweza kuruka na kwa mtindo mpya uliovutia umati. Mwishowe wanawe waliibuka washindi.

Watoto wa chura kahawia waliibuka washindi katika mashindano ya urukaji. Watoto hawa walikuwa na upungufu wa urukaji. Hata hivyo, waliporuka wote pamoja waliruka kwa mtindo uliovutia umati na wakaibuka washindi. Watoto wanahimizwa tena katika hurafa umuhimu wa kuzingatia maadili ya subira na uvumilivu. Mwandishi amebainisha kuwa na uvumilivu huleta baraka. Watoto mara nyingi hukosa uvumilivu na ni muhimu kuang'amua ya kwamba uvumilivu una faida. Kujitahidi kutawafanya watoto waibuke washindi kama watoto wa chura Kahawia.Kwa hivyo maadili kama vile uvumilivu na kujitahidi kwa watoto huwa na manufaa. Watoto ni miongoni mwa wanajamii. Kipury (2002) amesema kwamba hurafa hutekeleza dhima ya kuwafunza watoto maadili mema yanayokubaliwa katika jamii. Kupitia hurafa maadili ya wema, huruma, ukarimu, ucheshi na bidii kazini yamejitokeza katika Ngiri *Mganga* cha Kariuki (2010). Mwandishi, katika hadithi *Ngiri Mganga wa Wanyama* amesema:

> Ungemwona akitapatapa kwa furaha baada ya kunusa na kukoroma mara tatu, ungejua kwamba amewahi kuyapata matunda matawi na mizizi ifaayo dawa. Ngiri aliendelea kutafuta viungo huku akiimba wimbo huu.Nusa, koroma, nusa koroma. Nina nini hapa? Matawi, mizizi na matunda viungo dawa kwa walio'ugua (Uk.25).

Kutokana na dondoo, Ngiri mganga wa wanyama, anatapatapa kwa furaha baada ya kupata dawa alizohitaji. Anajua amelitimiza lengo lake la kutaka kuwatibu wanyama wagonjwa. Kariuki (2010), amembainisha Ngiri Mganga kama daktari aliyependa kazi yake. Anasema, aliimba na kutapatapa kwa furaha baada ya kuzipata dawa alizokuwa anatafuta. Dawa hizo alizitumia kuwatibu wanyama wagonjwa bila ya malipo yoyote. Mwandishi anahimiza umuhimu wa watoto kuwa na bidii kazini. Iwe masomoni, kazi za nyumbani na kazi zozote wazifanyazo. Pia inaonyesha umuhimu wa kujali maslahi ya wengine. Hadithi ya *Ngiri Mganga* imeelimisha

umuhimu wa maadili ya wema na huruma. Watoto wanaposoma hadithi hupenda kuiga na kurudia chochote wanachokumbuka kama vile; kuiga wema na huruma wa Ngiri mganga. Watoto wanaelimishwa kuwaonea wenzao huruma, kuwa wakarimu na kuwasaidia wenzao kadiri wawezavyo jinsi Ngiri alivyosaidia wanyama wenzake.

Kariuki (2010), amedhihirisha ya kwamba watoto wanapotimiza malengo yao ya kuwasaidia wenzao wanatakiwa kufurahi. Kuwasaidia wengine kunajitokeza kama jambo muhimu. Watoto kuiga mfano wa Ngiri mganga aliyefurahi kutibu wenzake ni muhimu. Maadili ya huruma na Karimu yanaelimishwa.

Kwa mujibu wa Wamitila (2011) hurafa tangu zamani zilikuwa maarufu miongoni mwa watoto kwa kuwaelekeza maadili bora kama zilivyo hadi sasa. Maelezo haya ya Wamitila yanalingana na matokeo ya kwamba hurafa huelimisha watoto maadili bora kama huruma, wema, ukarimu, ucheshi, furaha na uadilifu.

### 2.1.2 Kuonya

Kulingana na TUKI (2004) kuonya ni kutahadharisha kabla ya jambo baya kutokea au kutendeka. Anayeonywa hujulishwa athari ya kutenda jambo husika. M'Ngaruthi (2008) amesema maonyo ni mawaidha yenye mwongozo. Mawaidha hutokana na uzoefu wenye busara.

Dhima ya kuonya imethibitishwa na mwandishi wa kitabu *Ngiri Mganga*. Kariuki (2010) amewaonya watoto dhidi ya maovu. Maovu haya wakiyatenda kwa siri yanajulikana hatimaye. Ufafanuzi wa dhima hii ya kuonya umeelezwa na Kariuki (2010) katika hurafa *Ngiri Mganga wa Wanyama*. Dondoo lifuatalo linafafanua hivi:

> Bundi hangeweza kuvichukua vikapu kwa sababu ya uzito wake. Hivyo alipaa hewani na kurudi alikomuacha Mganga Ngiri ili kumwarifu. Alipomueleza yaliyotukia, Ngiri,

> alicheka kwa sauti kubwa. "Usiwe na hofu,"alimwambia Bundi, umefanya kazi nzuri sana. Hata kufikia mapambazuko, Tumbili atakuwa angali usingizini." (Uk.34).

Katika dondoo linalotangulia, Kariuki (2010) amesema bundi alipokuwa akivitafuta vikapu vya Ngiri Mganga aliviona. Tumbili alikuwa ameviiba. Ngiri Mganga alimshauri bundi aimbe wimbo wa kumshauri tumbili ayale matunda mekundu ili awe mwerevu. Tumbili kusikia huo wimbo, aliyala upesi. Ndipo akapatwa na usingizi mzito. Ilimbidi sasa bundi kuvichukua vikapu hata ingawa hakuweza kwa sababu vilikuwa vizito. Dawa za Ngiri Mganga zilikuwa humo. Ndipo alipaa hewani ili kumwarifu Ngiri ya kwamba amevipata vikapu vyake vikiwa na Tumbili.

Tumbili alidhani baada ya kuviiba vikapu vya Ngiri vitakuwa vyake milele. Bundi alitumwa na Ngiri kumwambia ayale matunda mekundu ili awe mwerevu. Badala ya kuwa mwerevu alipatwa na usingizi mnono. Mwandishi Kariuki (2010) amewaonya watoto dhidi ya maovu wanaotenda kwa siri. Yote huja kujulikana hadharani. Ukaidi wa tumbili kukataa kuvirudisha vikapu vya Ngiri uliambulia patupu. Pia wizi haufai, kwa sababu mwizi baadaye huadhibiwa na kuaibishwa.

Chimerah na Njogu (2011) wamesema ya kwamba hurafa hudhihirisha tabia za wahusika wanyama ambao hulinganishwa na tabia za wahusika binadamu. Usawiri wa wahusika wanyama unafuata mtindo wa jozi za kilinganuzi ambapo, wahusika wabaya kama Tumbili wanaaibika kwa matendo maovu (Wamitila 2008).

Benton na Fox (1985) wameungwa mkono na Wamitila (2008) ya kuwa watoto wanaposoma hadithi zao hupenda kutenda kama wahusika wenye maadili bora kutegemea tajiriba, umri, uzoefu,na mazingira yao. Wahusika hawa wanatumiwa kuonya watoto dhidi ya kutenda maovu kwa jamii. Kwa hivyo Kariuki (2010) amewaonya watoto dhidi ya kutenda maovu kama kuiba kwa sababu siku moja ujulikana jinsi tumbili alivyopatikana na vikapu vya Ngiri Mganga.

Maudhui ya kuonya yamejitokeza katika *Ngiri Mganga* cha Kariuki (2010). Dondoo lifuatalo limeeleza:

> Tuiuze hii Kabichi mume wangu?" Mke wa Sungura alitoa kauli yake. Tunaweza kulipwa hela nzuri sana eti" (uk.41)… Badala yake walimwona Kiwavi aliyenona kama nguruwe akigagaa mahali hapo. Kaka Sungura aliangua Kilio (Uk. 44).

Kariuki (2010) ameonyesha jinsi mke wa sungura alivyokuwa akimsihi waliuze kabichi ambalo lilitakiwa na wanunuzi wengi. Alimwonya dhidi ya kukataa kuliuza. Sungura alikataa kuliuza kwa sababu alitamani kabichi kubwa sana kuliko zote duniani. Mwishowe sungura alishangaa kumwona kiwavi amekula kabichi lote. Sungura alionywa auze kabichi akakataa mawaidha ya mke wake. Kuwa mkaidi na mwenye tamaa kwake kuliambulia patupu. Kulingana na Pierce (1977) hurafa za watoto huelimisha matarajio mema ya jamii. Watoto wanahitaji kufuata mawaidha na kuonywa kuepukana na tamaa na ukaidi. Wasiwe kama sungura ambaye alipuuza mawaidha na maonyo ya mkewe. Maovu haya mwishowe humfanya mtu kuhangaika. Mara nyingi watoto wanayapuuza mawaidha ya wazazi na walimu wanakuwa wakaidi na kuwa na tamaa nyingi. Ni onyo kwa watoto kuyatilia maanani mawaidha yote wanayopewa. Wahenga hawakukosea waliponena, asiyesikia la mkuu huvunjika guu.Watoto wasipoyachukulia umuhimu mawaidha ya walimu na wazazi watahangaika baadaye

### 2.1.3 Kuburudisha

M'Ngaruthi (2008) amesema kuburudisha ni kustareheka aghalabu kwa vichekesho, muziki na michezo. Vichekesho vinaweza kutegemea msomaji au msimuliwa wa hurafa. Ngugi (2009) amesema hurafa huburudisha watoto kupitia kugusa hisia zao wakafurahi na kucheka; hivyo basi kuwaletea uchangamfu katika maisha. Ngugi (2009) pia ameeleza ya kwamba watoto wanaposoma vitabu vyao wanaweza kutambua raha kutokana na jinsi wahusika walivyoelezwa

na tajiriba wanazopitia. katika kitabu Burudani hujitokeza katika hurafa kupitia maneno ya kejeli, vituko vya hapa na pale au hata nyimbo. Ngure (2011), ana maoni kwamba katika hurafa, jamii au hadhira huwacheka wanyama wanaokubali kuhadaiwa na wanyama wadogo. Pia wasomaji watoto wanawacheka wanyama wanaotenda kinyume cha maadili na kuaibika mwishowe. Ulafi na tamaa pia huchekwa.

Bakize (2014) ameeleza dhima moja ya hurafa ni kuburudisha msomaji wa hurafa au hadhira. Msomaji anachangamshwa kwa kusoma tanzu mbalimbali zilizotumiwa na mwandishi. Tanzu hizi ni kama vipengele vya nyimbo na semi. Katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* ya Mayega (2004) maudhui ya kuburudisha yanajitokeza. Mwandishi anasema:

> Siku moja alfajiri na mapema, kabla wanyama wote hawajaelekea mbugani Sisimizi aliwaomba wamruhusu ili aende kupambana na Tembo. "Ha! Ha! Ha! Ha!" wanyama wote walicheka sana. Jambo hilo liliwashangaza sana. …Sisimizi aliendelea kutamba ndani ya mkonga wa Tembo, Tembo naye aliendelea kubamiza mkonga wake kwenye mti. Hatimaye alidondoka chini na kufa (Uk.11).

Katika dondoo hili, Sisimizi ambaye ni mnyama mdogo alirauka asubuhi siku moja kuomba ruhusa ili akamwuue tembo. Tembo ni mkubwa mno akilinganishwa na sisimizi. Wazo hilo la sisimizi linachekesha wasomaji watoto kama vile wanyama walivyocheka na kushangaa walipoombwa ruhusa na sisimizi kumwuua tembo. Hata ingawa sisimizi ni mdogo alifaulu kumuua tembo. Jinsi Sisimizi alivyoendelea kutamba ndani ya mkonga wa tembo ni njia inayochangamsha watoto. Ujasiri wa sisimizi ambaye ni mdogo sana akilinganishwa na tembo unazua kicheko miogoni mwa wanyama wote. Wanyama wenzake walikuwa wameshindwa kumwangamiza tembo. Burudani kutokana na hurafa huchangamsha na kuchekesha watoto.

Matokeo haya ya watoto kuchekeshwa na kuvutiwa na ushindi wa Sisimizi ambaye ni shujaa aliyeweza kumuua tembo unalingana na mtazamo wa Ngugi (2010) ambaye ameeleza hadithi za watoto huwafurahisha. Wao wanasema watoto wanaposoma hadithi zao huvutiwa na wahusika

jasiri na shujaa. Wahusika hawa wanaweza kuwa wadogo kama sisimizi au mchwa lakini wanaibuka washindi miongoni mwa wanyama wengine. Watoto wakivutiwa na wahusika hawa wanaweza kuiga sifa zao. Sifa za wanyama hawa ni kama vile ushujaa na ujasiri ambazo ni muhimu kwa watoto. Vilevile Katika *Ngiri Mganga* (2010), wasomaji wa hurafa ambao ni watoto wanafurahi na kuburudika wanaposoma kuhusu sherehe ya mashindano ya urukaji ya watoto wa jamii ya vyura. Kariuki anasema:

> Warudie! Warudie!" Umati ulisihi kwa kelele na fujo. "Tunataka warudieeeee!" kwa tabasamu na maringo mengi (uk.21).

Mwandishi katika dondoo hili ameeleza jinsi umati ulivyoshangilia kwa shangwe na nderemo. Walihitaji wana wa chura kahawia kurudia urukaji. Ilikuwa hivyo kwa sababu wana wa chura kahawia waliruka kwa mtindo mpya uliovutia umati. Ndivyo umati wakachangamka na kufurahi.

Pierce (1977) katika mhimili wa tatu ameeleza kutokana na usomaji wa kazi ya fasihi ujumbe muhimu wa maudhui unafaidi msomaji. Katika usomaji wa dondoo hili, watoto wakisoma hurafa wataelewa jinsi wana wa chura kahawia walivyofurahisha umma katika sherehe. Ndivyo wakapiga kelele na fujo wakitaka warudie. Furaha iliyowapata waliohudhuria sherehe, ndiyo inayowapata watoto wanaposoma ya kwamba urukaji wa wana wa chura uliwachangamsha umma mno. Burudani kutokana na hurafa huchangamsha na kuchekesha watoto.

Burudani katika hurafa hujitokeza wakati wanyama wanaotenda kinyume cha maadili hufumaniwa na kuaibishwa (Ngure 2011). Katika kitabu chake Nyakeri (2011), ambacho ni *Sungura na Mbwa* anasema:

> Tafadhali nisameheni ni njaa iliyonifanya kuiba" "Uvivu wako ndio umekuletea njaa", Mbwa alimwambia kwa sauti kali (uk.25).

Nyakeri (2011) katika dondoo linalotangulia amedhihirisha vile sungura alivyokuwa amekosa chakula hadi akaamua kwenda kuiba mahindi ya rafiki yake mbwa. Sungura alikuwa amezoea kuwa mvivu na kuiba chakula. Kufumaniwa kwa sungura akiiba mahindi kunafurahisha watoto wanaosoma hurafa. Ni kinyume cha maadili mema kuiba. Mwizi akishikwa huwa furaha kwa jamii. Matendo ya hila ya sungura yamefikia kikomo. Hilo linachangamsha watoto.

Katika uandishi wake Nyakeri (2011), anapoeleza jinsi sungura alivyofumaniwa kufumaniwa na mbwa akiiba kunazua kicheko. Watoto wanaposoma matini mpya inayosababisha kushindwa kwa mwizi sungura wanavutiwa na wale wapole na wakarimu kama mbwa. Pierce (1977) amesema kwamba nadharia ya semeotiki huhimiza kuvutiwa na kufurahia mienendo ya haki na ukweli. Watoto pia wanafurahia kushindwa kwa wadanganyifu kama sungura. Ngure (2011) ana maoni kwamba watoto hushangilia ushindi wa wapole na pia hufurahia kushindwa kwa walaghai kama sungura. Ucheshi umejitokeza kutokana na usimulizi wa hurafa katika kitabu *Ngiri Mganga*. Kariuki (2010) amesema:

> Halafu aliitana tena kukaingia Mnyama mwingine, na kufuatiwa na wengine. Mganga Ngiri aliwahudumia wote. Baadaye aliwasimulia kisa cha Tumbili na vikapu vyake viwili. Wanyama walicheka karibu kuvunjika mbavu.Walikuwa wanajiandaa kumwomba Ngiri airudie hadithi yake mara ya pili Tumbili alipojitokeza ghafla (uk.36).

Kulingana na dondoo hili Tumbili alikuwa ameiba vikapu vya Ngiri Mganga vilivyokuwa na dawa. Ngiri Mganga aligundua ya kwamba Tumbili ndiye aliyekuwa mwizi wa vikapu vyake. Hata hivyo Tumbili hakuona haya, alienda kwa Ngiri mganga ili ampe dawa. Wanyama waliokuwa wanangojea matibabu kwa Ngiri mganga walikuwa wameelezwa na Ngiri jinsi alivyoviiba vikapu vyake vya dawa. Walipomwona akitaka matibabu kwa Ngiri mganga, walicheka karibu kuvunjika mbavu. Ucheshi kutokana na hadithi pia huchekesha watoto wanaposoma hurafa hiyo. Kwa hivyo ucheshi husababisha burudani kwa watoto. Burudani

inatokana na kejeli zilizotumiwa katika hurafa (M'Ngaruthi 2008). Kariuki (2010) katika *Ngiri Mganga* anasema: "Viko wapi vikapu vyangu sasa?" Ngiri aliuliza kwa mzaha huku akiigiza hasira".

Katika dondoo hili Ngiri Mganga ametumia kejeli. Anamuuliza tumbili kuhusu vikapu vyake ilhali anajua ni yeye alikuwa ameviiba. Kejeli hiyo inachekesha wanyama waliosikia swali hilo. Wanyama walijua tumbili ndiye aliyekuwa mwizi wa vikapu vya Ngiri Mganga. Watoto hata wao wakati wanaposoma kejeli hiyo watachangamka na kufurahi.

Maudhui ya burudani yamejitokeza kupitia furaha inayowapata watoto wanaposoma na kuelewa ya kwamba tumbili ambaye alikuwa mwizi, alihitaji usaidizi wa Ngiri mganga. Mwizi aliyeiba vikapu vilivyokuwa na dawa, hakuona aibu ilhali alifika kwa Ngiri kutibiwa. Wakati huo Ngiri Mganga alimuuliza kama ameviona vikapu vyake vya dawa. Hiyo ilikuwa kejeli iliyozua kicheko. Wanyama walitaka Ngiri arudie kejeli hiyo. Hurafa hutekeleza dhima ya kuburudisha kwa watoto. Kicheko kinachosababishwa na usimulizi katika dondoo hilo, pia huchekesha watoto wanapoisoma hadithi ya Ngiri na tumbili. Nyimbo huashiria furaha na kuendeleza maudhui ya ushindi (M'Ngaruthi 2011). Wimbo katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* unabainisha dhima ya kuburudisha. Wanyama waliimba wimbo ufuatao:

> Shangwe, shangwe, umeliangusha x2, Lilituonea, umeliangusha shangwe, shangwe , umeliangusha x2, Lilikuwa dikteta, umeliangusha (uk.19).

Mayega (2004) amedhihirisha jinsi wanyama walivyorukaruka kwa furaha isiyo kifani wakiimba wimbo wa furaha na ushindi. Ushindi huo unatokana na sisimizi kumuua tembo. Wanyama wanasisitiza maudhui ya ushindi. Ujumbe katika wimbo nikwamba tembo aliyewaonea wanyama na kuwa dikteta ameangamizwa na sisimizi. Shangwe na vigelele wanapoimba ni kwa sababu utumwa wa mfalme Tembo umekomeshwa.

Wamitila (2006) ameeleza ya kwamba semiotiki ni nadharia inayoshugulika na ishara na uashiriaji katika kazi ya fasihi. Kwa hivyo wimbo ni ishara inayosababisha furaha kwa watoto wanapoimba. Wimbo unawafurahisha watoto, ambao wanafurahi na kuimba wakishangilia ushindi. Wanaposoma hurafa wanaimba jinsi wanyama walivyoimba. Kwa hivyo dhima ya kuburudisha inajitokeza kutokana na hurafa. Nyimbo katika hurafa hutumiwa kuashiria maudhui fulani. Ujumbe unapashwa kwa kuimba kama ilivyo katika hurafa *Ngiri Mganga* ya Kariuki (2010), Bundi anaimba:

> Tumbili mwerevu, mwenye busara kula matunda, kula matunda Kula mekundu ya duara. Erevuka, kuwa mwenye busara. Kula mekundu ya duara ( uk.33).

Wimbo huu uliimbwa na bundi ili kupasha tumbili ujumbe wa kuyala matunda mekundu ya duara. Alisisitiza katika wimbo matunda haya yatamfanya awe mwenye busara . Bundi alitaka ayale matunda hayo ili tumbili apate usingizi mnono. Baada ya kulala wangechukua vikapu vya Ngiri ambavyo Tumbili alikuwa ameiba. Umuhimu wa wimbo huu ni kupeleka ujumbe. Bakize (2014) amesema wimbo hutumiwa kupasha ujumbe na kutega makini ya mlengwa. Ujumbe ni kumfanya tumbili ale matunda mekundu. Alikuwa ameanza kulala lakini aliposikia wimbo huo aliamka na kusikiliza kwa makini. Kwa hivyo, licha ya kuwasilisha maudhui ya kutaka ayale matunda mekundu alifurahia wimbo. Watoto wanapotaka kuwasilisha maudhui wanaweza kuimba ili kuvuta usikivu wa walengwa wao. Nyimbo katika hurafa huvutia na kueleza maudhui muhimu.

### 2.1.4 Kuelekeza

Kulingana na Njogu na Chimerah (2011) dhima ya kuelekeza watoto inahusu kuhimizia watoto kutenda yanayotarajiwa kwa jamii kama ukweli na kujali maslahi ya wengine katika jamii.

Matendo yasiokubaliwa ni kama udanganyifu, unafiki, ubinafsi na ulaghai.Watoto huelekezwa tabia zinazokubaliwa kwa jamii.

Watoto wameelekezwa kuepukana na tabia ambazo hazijakubaliwa kwa jamii na kufuata yanayokubaliwa na jamii. Weche (2000) amesema kuwa hurafa zinawafunza watoto kuhusu mienendo inayokubaliwa kwa jamii. Hurafa zinaelekeza mienendo inayotendwa kwa matarajio ya jamii. Mpesha (1995) amesema vitabu vya watoto kama hurafa vinatakiwa kuwafahamisha kuhusu matendo mema ya jamii na kupinga kutenda uovu kwa jamii. Katika kitabu *Sungura na Mbwa* (2011) dhima ya kuelekeza imebainishwa. Mwandishi amesema:

> Itanibidi niende kwa Mbwa usiku wa manane niingie ghalani na kuiba chakula,"alifikiria bila kumwambia mkewe. "Usiku huo, Sungura hakulala, ilipofika usiku wa manane, Sungura alitoka chumbani. Mke wake alipomuuliza alikokuwa akienda alimwambia kuwa alikuwa anatoka nje haja ndogo (uk.15).

Nyakeri (2011) katika *Sungura na Mbwa* ameeleza jinsi sungura alivyopanga kwenda kuiba mahindi ya rafiki yake mbwa. Yeye hakumwambia hata mke wake mipango yake. Mke wa sungura alipomuuliza anatoka wapi alimwambia ya kwamba alikuwa ametoka haja ndogo. Alimdanganya kwa sababu alikuwa anataka kuiba mahindi ya mbwa. Udanganyifu unajitokeza pale sungura hamwambii mke wake ukweli. Alimdanganya anatoka haja ndogo na si kuiba mahindi ya mbwa. Unafiki unapatikana pale sungura anaiba mahindi ya rafiki yake mbwa. Pierce (1977) katika mhimili wa tatu wa nadharia ya simiotiki ameelekeza watoto kutenda matendo mema . Ulaghai na unafiki haufai miongoni mwa watoto. Hilo litawabidi kuepukana na udanganyifu, unafiki, ubinafsi na ulaghai.

## 2.2 Hitimisho

Sura ya pili imechunguza dhima katika hurafa za watoto. kutokana na vitabu teule dhima mbalimbali zimepatikana kuwa muhimu na kuelimisha watoto. Mhakiki wa hurafa hulenga

kubaini kama mtoto ataelimishwa na kuelekezwa. katika dhima ya kuelimisha watoto wamesisitizwa kuwa na maadili yanayokubaliwa kwa jamii. Haya ni kama subira, wema, kuwa na matumaini, ukarimu na busara. Watoto wanaonywa dhidi ya wizi na udanganyifu. Wizi na udanganyifu haufai. Dhima ya kuburudisha ilibainishwa katika hurafa. Hurafa huchekesha wasomaji watoto kutokana na mzaha na kejeli za wahusika. Watoto hufurahia ushindi wa wanyonge na kushindwa kwa wenye kiburi kama tembo. Katika dhima ya kuelekeza watoto wamedhihirishiwa ya kwamba ulaghai na unafiki haufai hata kamwe. Sungura ambaye amekuwa mnafiki wa rafiki yake mbwa ameadhibiwa na kusababisha uhasama baina yake na mbwa. Sura inayofuata inahusu maudhui katika hurafa kwa watoto.

# SURA YA TATU

# MAUDHUI KATIKA HURAFA KWA WATOTO

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imeshughulikia dhima za hurafa kwa watoto. Sura hii imechunguza umuhimu wa maudhui katika hurafa kwa watoto. Maudhui kutokana na hurafa katika vitabu *Ngiri Mgang*a (2010) cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri *na Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Mayega. Nadharia ya semeotiki iliyoasisiwa na pierce (1977) imetumika kueleza umuhimu wa maudhui kwa watoto. Pierce (1977) anaeleza kazi ya fasihi iliyoandikiwa hadhira inabidi kuwasaidia kumarisha maisha yao. Hurafa zina ujumbe unaolenga kuwafaidi watoto, hasa wanaposoma vitabu vyao. Maudhui yaliyochunguzwa ni ya tamaa, wizi, uzembe, utamaduni na dhuluma.

## 3.1 Maudhui

Maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu na hali ya maisha ya wahusika katika fasihi (Senkoro (1982) Njogu na Chimerah (2011). Gatakaa (2012) akifafanua zaidi kuhusu maudhui ameeleza ya kwamba maudhui ni ujumbe muhimu unaojitokeza katika kisa kizima kutokana na kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa Pierce (1977) semeotiki huchanganua ujumbe muhimu unaojitokeza kutokana na usomaji wa kazi ya fasihi. Watoto wanaposoma hadithi hupata maudhui muhimu. Maudhui haya ni kama tamaa, wizi, uzembe, umaskini, utamadun na dhuluma.

### 3.1.1 Tamaa

Wamitila (2003) anasema tamaa ni hamu kubwa ya kupata kitu. Hurafa za watoto huelimisha watoto kuhusu madhara ya tamaa. Wahusika wenye tamaa wameteseka kwa kuwa na hamu

kubwa ya kupata. Dhima ya kuelimisha kuhusu madhara ya tamaa imebainishwa katika hurafa ya *Sungura na Mbwa*. Katika kitabu *Sungura na Mbwa* cha Kariuki (2011) amesema:

> Ulifika wakati ambapo kabichi ya kaka Sungura iliishinda nyumba yake kwa kimo ikawa wanyama wa kijiji hicho, na pia vya mbali, huja kuikondolea macho kwa mshangao. Sungura alijivunia sana kabichi yake."Niuzie hii kabichi," Ndovu aliomba, Nitaifanya kitoweo cha jamii yangu." "Hapana, haiuzwi," Sungura alimjibu."Mimi kwa hii kabichi nitakupatia ng'ombe wawili" Fisi alijaribu bahati yake. "Haitawezekana" Sungura alijibu kwa kejeli. Labda ukirudi baada ya siku kadhaa nitaweza kukupatia mbegu chache kwa ng'ombe huyo mmoja" (Uk.42)… Walipofika shambani walipigwa na butwaa. Mlikuwa hamna kabichi hata chembe. Badala yake walimwona kiwavi aliyenona kama nguruwe akigagaa mahali hapo. Kaka Sungura aliangua kilio, kweli mtaka yote hukosa yote (Uk.44).

Katika dondoo hili Sungura amebainishwa kama mwenye tamaa. Tamaa yake imebainika wakati alipanda kabichi na alitamani sana kabichi kubwa kuliko zote duniani. Alikuwa na tamaa na alikataa kuwauzia wanyama waliotaka kulinunua, kama Ndovu. Mwishowe hilo kabichi lililiwa na kiwavi na likaoza lote. Sungura kwa kuwa na tamaa ya kutaka kabichi kubwa zaidi alikataa kuliuza kabichi. Alipoenda kuliangalia siku iliyofuata alikuta kiwavi amelikula lote. Mipango ya Sungura iligonga mwamba. Angekubali kuliuza kabichi hangeenda hasara. Kwa sababu ya tamaa ya kutaka kuwa na kabichi kubwa kuliko lingine lote ulimweguni sungura alikosa kila kitu. Hivyo kuhimiza madhara ya tamaa na uchoyo. Watoto pia wanaelimishwa kuhusu madhara ya kupuuza mawaidha kwa sababu ya tamaa. Tamaa ya sungura na matokeo yake inaashiria watoto umuhimu wa kuepukana na tamaa. Kwa hivyo ni muhimu watoto kuepukana na tamaa na uchoyo kwani unaleta madhara.

Wakiunga mkono ya kwamba hurafa huwa na ujumbe mwishoni mwa hadithi, Njogu na Chimerah (2011) wamesema ya kwamba ujumbe unaotolewa mwisho mwa hadithi za watoto huwa na ujumbe unaoelimisha kama "tamaa mbele mauti nyuma." Kumaanisha tamaa husababisha hasara. Sungura alitamani kuvuna kabichi kubwa kuliko zote duniani. Alikataa

kuliuza na mwishowe kiwavi akalikula lote. Kwa hivyo watoto wanaposoma hadithi ya *Sungura na Kabichi* wanapata ujumbe unaohimiza tamaa husababisha hasara.

Katika *Ngiri Mganga* maudhui kuhusu tamaa yamejitokeza. Katika hadithi ya *Ngiri Mganga* Ngiri anamuonya fisi dhidi ya ulafi. Naye fisi hakusikia bali aliendelea kula kwa tamaa. Mwishowe alipatwa na mchafuko wa tumbo. Alienda kupewa dawa na Ngiri. Kumaanisha tamaa yoyote iwe ya chakula au vyovyote vile mwisho husababisha hasara. Adhabu hii inabainishwa hivi:

> Mara tu nitakapomaliza hii nyama, nitakujia matibabu; fisi alisema huku mashavu yamefurishwa na nyama. "Chunga sana usije ukavimbiwa na tumbo hasa, "Ngiri alimtahadharisha na kwenda njia zake (uk.26) " Ulinionya nitahadhari mchafuko wa tumbo na sasa ninao (uk.35)

Kutokana na dondoo hili fisi ameonywa dhidi ya tamaa na Ngiri lakini hakusikia. Alikula nyama nyingi na mwishowe akapatwa na mchafuko wa tumbo. Kwa hivyo tamaa husababisha hasara. Pia watoto wanahimizwa dhidi ya tamaa. Kutokana na tamaa ya fisi, alikula nyama nyingi kupita kiasi. Mwishowe akaumwa na tumbo. Watoto wanatolewa ujumbe ya kwamba kula chakula kupita kiasi kunaweza kusababisha mchafuko wa tumbo. Maudhui juu ya madhara ya tamaa ya yamejitokeza pia kupitia hurafa ya *Sisimizi Amuua Tembo* ya Mayega (2004) amesema:

> Kuanzia siku hiyo tembo akajinyakulia ufalme wa wanyama wote. Ndipo Tembo alipotangaza amri ya kuwataka wanyama wote kumletea chakula kila siku. Nao wanyama wote walitekeleza amri hiyo. Hatimaye jambo hilo likawachosha. (uk.11).

Kulingana na vile tembo alitamani chakula kutoka kwa wanyama kila siku, wanyama hawakufurahia. walichoshwa kumpelekea chakula kila wakati. Wanyama walikutana kwa siri na kukata shauri kumuua Tembo. Mwandishi amedhihirisha ya kwamba wanyama hawakufurahia kumpelekea tembo chakula kila siku. hakustahili kuhitaji chakula kutoka kwao kila siku. Hilo ni

dhihirisho ya kuwa mwenye tamaa. Baadaye wanyama waliamua kumuua. Katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* ya Mayega (2004) amesema ya kwamba:

> Hatimaye jambo hilo liliwachosha. Wakakutana kwa siri na kukata shauri kumuua mfalme Tembo ili waondokane na utumwa huo (uk.11).

Katika dondoo linalotangulia ni dhahiri kuwa mfalme tembo alipangiwa kuuawa kwa sababu ya tamaa. Alitamani chakula kutoka kwa kila mnyama. Wanyama hawakufurahia tamaa ya tembo. Kulingana na maelezo ya dondoo maudhui katika hurafa huwa na ujumbe kwa watoto. Ujumbe huo ni kwamba tamaa huwa na madhara.

### 3.1.2 wizi

Kwa mujibu wa *Kamusi sanifu* (2004) wizi ni kuchukua kitu cha mtu mwingine kwa siri bila ya ruhusa au haki. Wizi haukubaliki na jamii yoyote. Wizi huwa na madhara. Katika kitabu *The Law of Kenya* Tudor (1986) ameeleza ya kwamba kuiba ni kuvunja sheria kama inavyoelezwa katika kifungu cha 63:63,1 wizi ni utumiaji wa hila kuchukua chochote bila haki ya kukimiliki au kuwa na idhini ya mwenyewe. Seheme ya 275 inatueleza adhabu ya wizi. Aliyepatikana na hatia ya wizi huhukumiwa kifungo cha miaka mitatu au adhabu nyingine yoyote kulingana na kitu kile aliiba na hali ilivyokuwa wakati wa wizi huo. Katika kitabu *Sungura na Mbwa* cha Nyakeri (2011) dondoo lifuatalo linabainisha maudhui ya wizi.

> Hata wewe umekuja hapa kuiba?" Panya alimuuliza, Sungura alinyamaza kimya (uk.20) … Kumbe ni wewe umekuwa ukituhangaisha?" Sungura alipoangalia nje, alimwona Mbwa ameyaweka tayari meno yake makali. "Shuka mara moja," Mbwa aliamrisha.

Nyakeri (2011) amesema kwamba Sungura alipanga kuiba mahindi ya rafiki yake mbwa.

Alikuwa akiiba siku nyingi lakini siku moja alishikwa. Alishikwa na baadaye akaadhibiwa. Aliaibishwa na kutangazwa yeye ndiye mwizi. Alionywa dhidi ya kukaribia kwa mbwa. Urafiki

wa mbwa na sungura haukudumu. Katika kitabu *Sungura na Mbwa* uamuzi wa korti ya wanyama ni kama ufuatao:

> Korti ya wanyama ilikaa kusikiliza kesi kati ya Sungura na Mbwa.Wanyama waliamua kuwa Sungura alipe chakula alichokuwa ameiba. Pia, waliamuru kuwa baada ya kulipa chakula hicho,Sungura asiruhusiwe kukaribia kwa Mbwa. Urafiki wao ukaishia hapo (uk.25).

Dondoo hili limedhihirisha wizi husababisha aibu, uhasama na kugharimu malipo ya chochote kilichoibiwa. Maudhui ya wizi huwa na ujumbe ya kwamba watoto kuiba kunasababisha madhara baya. Sungura aliendelea kuiba lakini siku moja alishikwa. Watoto wakisoma hurafa watafahamu sungura aliiba mahindi ya mbwa na alfumaniwe na mwenye mahindi. Kwa hivyo watoto wanaonywa dhidi ya wizi.

### 3.1.3 Uzembe

Kulingana na Miruka (2011) uzembe ni hali ya kufanya kazi bila makini au ugoigoi. Uzembe huwa na matokeo mabaya. Miruka (2011) ameeleza kuwa wenye bidii na wanaofanya kazi kwa makini bila uzembe husifiwa na jamii. Wenye bidii na wanaofanya kazi kwa makini bila ugoigoi wanaepukana na ufukara. Kwa hivyo jamii yoyote inaelimisha uzembe haufai maishani ya kila mtu. Katika *Sungura na Mbwa (*2011) maudhui ya uzembe yamejitokeza

Mwandishi amesema: `

> Kwa upande mwingine Sungura alikuwa ni mnyama mvivu. Alipenda kulala sana.Wakati wanyama wengine walikuwa wakilima yeye alikuwa akilala. Alilala sana mpaka mchana (uk. 1).

Katika dondoo linalotangulia sungura ni mnyama mvivu asiyependa kufanya kazi. Hakulima kama wanyama wengine. Alipenda tu, kulala mpaka mchana. Kutokana na uvivu wake watoto wake walikosa chakula. Ndipo Nyakeri (2011) katika *Sungura na Mbwa* anasema hivi:

> Sungura na jamii yake waliendelea kuishi maisha ya kubahatisha. Hawakwenda kutayarisha shamba ili wapande chakula. Mwezi ulipita. Chakula alichokuwa amemwibia Mbwa kilikwisha. Ilibidi Sungura arudi kwa Mbwa kuiba tena. Alitumia mbinu kama zile za kwanza na kuiba chakula kingi (uk.22).

Kulingana na Nyakeri (2011) sungura alikataa kufanya kazi. Hakutayarisha shamba ili apande. Kutokana na uvivu wake aliishi maisha ya kubahatisha. Uzembe wake ulimfanya akose chakula cha watoto wake. Alifikiria kwenda kuiba mahindi ya mbwa. Alipokuwa anaiba alifumaniwa akiiba na mwenye mahindi ambaye ni mbwa. Uzembe unasababisha ukosefu wa chakula. Pia uvivu ulimfanya sungura akaibe mahindi ya mbwa ili watoto wake wapate chakula. Kutokana na ujumbe wa maudhui katika dondoo hilo, msomaji anang'amua ya kwamba uzembe husababisha njaa na wizi. Mwishowe uzembe ulimfanya sungura kuwa maskini. Hayo ndiyo madhara ya uvivu. Watoto wanaposoma hadithi *Sungura na Mbwa* wanapata ujumbe kuwa uvivu kama wa sungura ulimfanya kukosa chakula. Wanahimizwa kutenda kinyume cha tabia za sungura.

### 3.1.4 Umaskini

Umaskini kulingana TUKI (2004) ni ukosefu wa mahitaji muhimu maishani. Mahitaji haya ni chakula, mavazi, nyumba na usalama. Maana ya kuadili ni kutenda haki na ukweli. Hurafa inabainishi ya kwamba mtu mwenye bidii hutajirika. Kumaanisha miongoni mwao watoto wanaotia bidii kazini bila shaka huepukana na umaskini. Maudhui ya umaskini yameelezwa katika katika hurafa, Nyakeri (2011) amesema:

> Watoto wake walianza kukonda kama ngonda kwa kukosa chakula. Watoto wenyewe walikuwa wameparara na pia walionekana wenye kudhoofika sana kimwili (Uk.4).

Nyakeri (2011) ameonyesha jinsi watoto wa sungura walianza kukonda kwa kukosa chakula. Sungura alikuwa mvivu na hakupenda kufanya kazi. Watoto wake walidhoofika kimwili na kuparara. Mwandishi anadhihirisha umaskini wa sungura ulisababishwa na uvivu wake. Maudhui ya umaskini yanaeleza ujumbe ya kwamba muhimu yanayojitokeza ni muhimu watoto kukataa

uvivu na kutia bidii kwa kazi zozote wanazofanya. Hii ni kwa sababu umaskini huwapata wavivu kama familia ya sungura. Umaskini huwapata wazembe na wasiopenda kutia bidii kazini kama familia ya sungura. Umaskini kama huo wa sungura unatokana na uzembe.Watoto wakisoma hurafa watapata ujumbe wa maudhui kwamba uvivu husababisha umaskini.

Watoto wakikosa malezi mema na chakula huathirika kiafya na kimwili. Wanakuwa wanyonge. Watoto kama hao huonyesha ufukara. Nyakeri (2011) amebainisha ya kwamba watoto wa sungura walianza kukonda na kuparara. Kuonyesha umaskini unaotokana na uzembe wa sungura na familia yake. Nyakeri (2011) amehimiza watoto watie bidii kazini wasifuate mfano wa sungura na familia yake. Watoto wamehimiziwa ujumbe wa maudhui unaoeleza ya kwamba kukataa kufanya kazi kunasababisha umaskini kama ule uliwapata sungura na familia yake.

### 3.1.5 Utamaduni

Utamaduni unahusu mila, jadi, desturi ya mavazi, matumizi ya mali asili, nyimbo, tabia na miiko, dini, maadili na maisha ya jamii kwa jumla (Miruka 2011). Katika hurafa maudhui muhimu kwa watoto hujitokeza. Senkoro (1982) ameeleza ya kwamba kutokana na fasihi maudhui mbalimbali kama vile ya utamaduni yanapitishwa. Watoto hufaidika kutokana na hali ya maisha ya wahusika au ujumbe wa jumla wa hurafa. Katika Ngiri Mganga, maudhui ya utamaduni yamejitokeza. Kariuki (2010) amesema:

> Muda si mrefu, kapu la pili la mganga lilijaa matunda, matawi na mizizi ya kila aina. Mizizi mingine ilikuwa minene na mifupi. Mingine ilikuwa mirefu na nyembamba (uk.27).

Kariuki (2010) amesema ya kwamba Ngiri Mganga ambaye alikuwa daktari wa wanyama alijishugulisha na utafutaji wa dawa. Dawa alizokuwa akitafuta ni mali asili na za kimila. Nazo ni matunda, matawi na mizizi za kienyeji. Hizo ni dawa za kiutamaduni za kiafrika. Kariuki

anadhihirisha utamaduni muhimu wa kutumia mali asili kama dawa. Ngiri alitegemea mizizi,matawi na matunda kutayarisha dawa za kuwatibu wagonjwa. Maudhui ya kuhifadhi utamaduni yanawatolea watoto ujumbe wa kuchukulia umuhimu wa dawa za kienyeji kama zilivyotumiwa na Ngiri kutibu wanyama wenzake. Dawa hizi hata sasa hutumika na ni muhimu kwa sababu zinawatibu wagonjwa.

Maoni ya Hunt (1994) yamelingana na matokeo ya uchanganuzi wa maudhui ya utamaduni yanayohimizia watoto dhima ya kuzingatia mila na desturi za jamii. Hunt (1994) ameeleza ya kwamba hadithi za watoto huandikwa zikiwa na lengo la kufundisha watoto kuhusu matarajio ya jamii na utamaduni husika.

Miruka (2011) ameeleza kuwa utamaduni unahusu desturi na maisha ya kila siku ya jamii. Desturi hizo ni kama kuwa na baraza la kitamaduni ambalo linahukumu na kuadhibu wanaotenda kinyume cha sheria za mila na desturi za jamii. Kulingana na M'Ngaruthi (2008) mabaraza ya kitamaduni yalitekeleza shughuli kama vile kuzipatanisha jamii, kulinda utamaduni, kuadhibu wakosaji, kutoa ushauri na kulinda maeneo yenye umuhimu wa kitamaduni. Katika jamii ya Wameru M'Ngaruthi (2008) amesema baraza la kitamaduni linaitwa Njuri Ncheke. Maudhui ya utamaduni yamejitokeza katika *Sungura na Mbwa* cha Nyakeri (2011). Dondoo lifuatalo linaeleza.

> Korti ya wanyama ilikaa kusikiliza kesi kati ya Sungura na Mbwa. Wanyama waliamua kuwa sungura alipe chakula alichokuwa ameiba. Pia, waliamuru kuwa baada ya kulipa chakula hicho, Sungura asiruhusiwa kukaribia kwa mbwa. Urafiki wao ukaishia hapo (uk. 25).

Dondoo linalotangulia limeeleza ya kwamba wanyama walikuwa na baraza la utamaduni ambalo liliitwa korti ya wanyama. Kazi ya korti hiyo ni kusikiliza kesi na kuhukumu mkosaji au kumwadhibu. Sungura alikuwa ameiba chakula cha mbwa. Alipatikana na hatia na akapewa

adhabu. Aliambiwa alipe chakula chote alichokuwa ameiba cha Mbwa na akaambiwa asikaribie kwa Mbwa.

Kulingana na Nyakeri (2011), dondoo kuhusu baraza la kitamaduni linatekeleza jukumu muhimu ya kuadhibu wanyama wanaotenda kinyume cha maadili. Kila jamii husisitiza umuhimu wa kutumia mifumo ya kisheria kutatua shida zao. Watoto husoma hurafa ili kuelewa tamaduni kwa jamii na kuzihifadhi (Brooks na Huck 1979). Watoto wanaposoma jinsi sungura alivyohukumiwa na kuadhibiwa kutokana na matendo yake, wanaelewa mila na desturi za jamii na kuepukana na yanayosababisha adhabu. Mila na desturi huzingatia amani miongoni mwa wanajamii. Kwa hivyo kutokana na ujumbe wa maudhui ya utamaduni katika hurafa, watoto wanahimizwa umuhimu wa kuhifadhi na kuzingatia utamaduni.Maudhui yafuatayo pia yanafaidi watoto wanaposoma hurafa.

### 3.1.6 Dhuluma

Njogu na Chimerah (2011) wameeleza ya kwamba dhuluma inahusu unyanyasaji, uonevu na matendo yasiyo na haki. Katika uhakiki wa kazi ya fasihi ya watoto kuna uwezekano wa maudhui ya dhuluma. Dhuluma ni kinyume cha matarajio yanayokubaliwa na jamii. Dhuluma hujitokeza mara nyingi katika uongozi. Katika hurafa wanyama wanaweza kudhulumiwa na kiongozi wao ambaye ni mnyama mwenzao. Katika Hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* ya Mayega (2004) imesema:

> Kuanzia siku hiyo Tembo akajinyakulia ufalme wa wanyama wote. Ndipo Tembo alipotangaza amri ya kuwataka wanyama wote kumletea chakula kila siku. Nao wanyama walitekeleza amri hiyo. Hatimaye jambo hilo liliwachosha. Wakakutana kwa siri na kukata shauri kumuua mfalme Tembo ili waondokane na utumwa huo. Lakini kila aliyenyemelea Tembo na kujaribu kupambana naye aliuawa kikatili sana.Siku moja alfajiri na mapema, kabla wanyama wote hawajaelekea mbugani Sisimizi aliwaomba wamruhusu ili aende kupambana na Tembo. “Ha! Ha! Ha! Ha!”wanyama wote walicheka sana. Jambo hilo liliwashangaza sana. …Sisimizi aliendela kutamba ndani ya mkonga wa

> Tembo, Tembo naye aliendelea kubamiza mkonga wake kwenye mti. Hatimaye alidondoka chini na kufa (Uk.11).

Kutokana na dondoo hili tembo alijinyakulia ufalme wa wanyama wote. Tembo aliwadhulumu wanyama wenzake. Alitaka wanyama wote wamletee chakula kila siku. Wanyama walitii amri lakini jambo hilo liliwachosha. Wanyama waliamua kuasi na kupanga kumuua Tembo. Tembo alikuwa na nguvu ndiposa hakuna aliyeweza kupambana naye. Sisimizi ambaye alikuwa mnyama mdogo aliomba ruhusa ya kupambana na tembo. Wanyama walicheka mno,lakini alifaulu kumwangamiza Tembo.

Dhuluma imesababishwa na tembo. Anajifanya kiongozi wa wanyama wengine kwa sababu ana nguvu kuliko wao. Licha ya kujifanya kiongozi aliwataka wanyama wote wamletee chakula kila siku. Kwa hivyo aliwanyanyasa. Wanyama hawakufurahi na utumwa huo, walipanga njama ya kumuua, lakini wote walishindwa isipokuwa sisimizi. Mwishowe mfalme tembo aliyesababisha dhuluma aliangamia.

Mayega (2004) amesisitiza dhuluma haifai kamwe miongoni mwa watoto. Unyanyasaji wa watoto na kuwanyima haki hakufai. Hata watoto wanaweza kujiokoa kutokana na dhuluma na kunyimwa haki. Sisimizi ni mdogo lakini ndiye aliyewaokoa wanyama wenzake kutokana na utumwa wa Tembo. Wamitila (2010), amesema mwandishi wa hurafa huwa na mtazamo wa kuwapevusha wanajamii na kuwafanya wazindue na kujiokoa kutokana na utumwa. Watoto wakizinduka wanaelimishwa kupinga dhuluma na kusababisha mapinduzi. Pia wanapata uhuru wa kujua haki zao na kujitetea.

### 3.2 Hitimisho

Sura hii imekuwa na lengo la kubainisha maudhui kwa watoto katika hurafa. Data ya maudhui imedondolewa katika hurafa na kuchanganuliwa ili kudhihirisha ujumbe muhimu kwa watoto. Nadharia ya semeotiki ililenga kufafanua ujumbe wa maudhui muhimu kwa watoto.

Maudhui ya umaskini yamesawiriwa katika hurafa.Hayo yamedhihirisha ujumbe kwamba watoto wataepukana na umaskini wakitia bidii kazini.Umaskini hudhihirishwa na ukosefu wa chakula kama watoto wa sungura.Watoto wanahimizwa kuwa na mienendo inayokubaliwa kwa jamii. Maudhui ya tamaa, wizi na uzembe yanaujumbe kwamba watoto wajitenge na tamaa, wizi na uzembe. Tabia hizo hazifai katika jamii.

Maudhui ya utamaduni yamebainishwa. Maudhui haya yamefafanua mila na desturi za jamii zinazostahili kuigwa. Watoto wamehimizwa kufuata mila na desturi za jamii na sheria za utamaduni husika. Watoto wanasisitizwa kuwa na amani na kuonelea dawa za kiyenyeji umuhimu ambazo zinatibu magonjwa hata sasa.

Maudhui kuhusu dhuluma yamekuwa na ujumbe ya kwamba unyanyasaji na ukosefu wa uadilifu uliotendewa wanyama na mfalme tembo ulisababisha kifo chake. Maudhui haya yameelekeza watoto kukataa kunyimwa haki na ukweli. La muhimu ni kwamba hata ingawa watoto ni wadogo wanaweza kutumia njia mbalimbali kupata haki na ukweli.Watoto wanaiga mhusika sisimizi ambaye ni mdogo lakini alipata mbinu ya kuwaokoa wanyama wenzake kutokana na dhuluma ya tembo. Sura inayofuata imeshughulikia mbinu katika hurafa zilizotumika kuwasilishia watoto dhima na maudhui.

# SURA YA NNE

## MBINU ZILIZOTUMIKA KUWASILISHA DHIMA NA MAUDHUI

### 4.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia imechanganua maudhui ya hurafa katika vitabu teule kwa watoto. Lengo la sura hii ni kudhihirisha mbinu ambazo zimetumiwa katika hurafa kupitishia watoto dhima na maudhui. Matini kutoka hurafa za watoto katika vitabu teule ndiyo data. Nadharia ya naratolojia husisitiza umuhimu wa mbinu zinazotumiwa na msimulizi au mwandishi wa hurafa. Mbinu hizo humwezesha mwandishi kuwasilisha ujumbe kwa njia inayofaa kutokana na maudhui ya hurafa na kuelekeza dhima kwa watoto. Prince (2003) ambaye ni mwasisi wa nadharia hii husisitiza wasimulizi wa hurafa mara nyingi hutumia mbinu kama taharuki, methali, tanakali za sauti, mianzo na miishio ya hadithi, tashbihi, usemi halisi, nyimbo, ukariri na zingine kama mbinu katika usimulizi wa hadithi.

### 4.1 Mbinu

Kwa mujibu wa M'Ngaruthi (2008) mbinu ni uwezo wa msimulizi au mwandishi kupata picha kamili ya kazi ya fasihi. Simpson (1997) amesema mbinu inayofaa ya kisasa ni ile inayomwezesha msomaji kuelewa kutokana na ustadi wa uzoefu. Msokile (1993) amesisitiza mbinu ni kazi ya kisanaa ya mwandishi katika kazi ya kifasihi ambazo mhakiki atatakiwa azitambue na kuzifafanua; baadhi ya mbinu hizi ni tamathali za usemi, matumizi ya takriri, methali, misemo na nahau na taharuki. Guantai (2002) ameelezea mbinu kama usanaa wa msimulizi au mwandishi wa hadithi. Mbinu rejeshi, kinaya, nyimbo, sauti ya msimulizi, jazanda na tashbihi ni baadhi ya mbinu katika hadithi. Crystal (1997) anasema ya kwamba wataalamu wengi wana mitazamo tofauti ya maana ya mbinu katika fasihi mmoja wao akiwa Wesley, ambaye anaeleza mbinu kama usanaa wa mwandishi au msimulizi.

### 4.1.1 Mbinu ya Taharuki katika Hurafa

Msokile (1993) amesema taharuki ni hali ya kusisimua hadhira iliyokusudiwa kutokana na hamu kubwa ya kutaka kujua nini kilitokea baadaye. Hali hii hujengwa kwa makusudi na msanii ili kuifanya hadhira iendelee kusubiri lile litakalotokea. M'Ngaruthi (2008), amesema mbinu ya taharuki humfanya msimuliwa kuachwa katika hali ya kutaka kusimuliwa zaidi. Maswali fulani huachwa bila kutatuliwa au kusimuliwa kikamilifu. Msimulizi au msomaji wa hadithi hubaki akiwa na hamu ya kujua zaidi. Hamu ya msomaji inaongezeka. Madumulla (2009) amemweleza msanii mzuri kuwa ni yule anapanga kazi yake kiasi kwamba tukio moja linasababisha jingine na kusababisha kujenga hamu ya msomaji ya kutaka kuendelea kujua litakalotendeka. Hali hiyo ndiyo anasema ni taharuki.

Wamitila (2010) amesema mbinu hii ya taharuki ni kanuni moja inayotawala fasihi ya watoto. Anaeleza zaidi, ya kwamba ni mbinu inayokuwa na mvutano au mgogoro ambao unatokana na mvutano miongoni mwa wahusika. Watoto wanakuwa na hamu ya kutaka kujua litakalotokea kutatua migogoro katika hadithi. Watoto wanakuwa na hamu ya kusoma zaidi na kuelewa mwishoni nani ataibuka mshindi. Nadharia ya naratolojia inahimiza usimulizi wa hurafa katika kazi ya fasihi unahitaji kusmuliwa kwa kuzingatia mbinu kama taharuki ili kuwapa wasomaji motisha wa kuendelea kusoma hadithi. Katika *Ngiri Mganga* mbinu za taharuki zimetumika.

> "Usijali, mzee kahawia alimjibu. Tutajaliwa mtoto mwingine ambaye bila shaka atakuwa Chura kamili ataruka kama sisi na vyura wengi. Halafu atawafundisha ndugu na dadake jinsi ya kuruka wakielekea mbele." (uk. 12).

Taharuki inajitokeza pale wasomaji wana hamu ya kutaka kujua kama mtoto atakayezaliwa wa tatu wa Chura kahawia atakuwa na kasoro ya urukaji kama jinsi alivyokuwa kifungua mimba na

wa pili kuzaliwa. Watoto wanaposoma hurafa hii wanakuwa na hamu ya kutaka kujua litakalotokea.

Msimulizi anawatia wasomaji watoto hamu ya kujua kama mzee chura kahawia na mkewe watajaliwa mwana anayeweza kuruka kama vyura wengine. Hamu hii inatokana na sababu ya kwamba mwana wa kwanza kuzaliwa hakuruka kama vyura wengine, alipojaribu kuruka alielekea kushoto badala ya mbele. Wa pili pia alipozaliwa, alikuwa na kasoro, na alipojaribu kuruka alielekea kulia. Wa tatu pia alipozaliwa alikuwa anaruka akielekea nyuma badala ya mbele. Taharuki katika hadithi hii ni kuwatia watoto hamu ya kutaka kuendelea kusoma hadithi ili kufikia mwisho. Kwa hivyo uzoefu wa watoto katika usomaji huwafanya wakuze lugha. Katika *Ngiri Mganga* cha Kariuki (2010) anaeleza:

> Hali ya taharuki na wasiwasi ilitanda kwenye umati. *Wana wa kahawia* waliruka ajabu. Shoto aliruka upande wa kushoto Dada yake kulia aliruka upande wa kulia, wakipitana angani…… makofi, nderemo na vigelegele viliendelea kwa muda kwani tukio kama hilo lilikuwa *halijawahi kuonekana* mashindanoni (uk. 21).

Mwandishi ametumia mbinu ya taharuki. Umati walingojea kwa hamu ya kutaka wana wa chura kahawia kuendelea kuruka. Ndiyo Kariuki (2010) anasema “hali ya taharuki na wasiwasi ilitanda kwenye umati”. Mwandishi amejenga taharuki kwa msomaji kutaka kujua jinsi watoto wa chura kahawia watakavyoruka kwa sababu walikuwa na kasoro na hawakuwa wanaruka kama vyura wengine.

Kariuki (2010) ametumia taharuki katika hurafa inayoburudisha na kuelimisha watoto. Anaeleza makofi, nderemo na vigelegele viliendelea kwa muda. Kudhihirisha furaha kwenye umati. Pia watoto wanaposoma hurafa hiyo watakuwa wanaburudika jinsi umati unavyofurahia.

Wana wa chura kahawia walikuwa na upungufu wa urukaji lakini hata hivyo waliibuka washindi. Walishinda kwa sababu walipangwa waruke wote pamoja.Walipoanza kuruka waliruka kwa

mtindo uliovutia umati tofauti na wengine. Hurafa hii ni muhimu kwa sababu watoto wanapewa motisha ya kufaulu maishani hata ingawa wana upungufu wa mwili au kasoro fulani maishani.Watoto wanakuwa na uwezo wa kuwa  na matumaini na subira.Hayo ni maadili muhimu kwa watoto. Dhima inayobainishwa katika hurafa.

Taharuki imetumiwa katika *Ngiri Mganga* ukurasa wa 23-37. Mbinu hii inajitokeza pale bundi anapogundua tumbili ndiye aliyeiba vikapu vya Ngiri. Msomaji anapatwa na hamu ya kutaka kujua kama tumbili atakubali kumrudishia au ni nini itakayotokea mwishowe. Kariuki  katika *Ngiri Mganga*  (2010)  anaposimulia hurafa ya kiwavi na kabichi anasema:

> Tuiuze hii kabichi mume wangu?" Mke wa sungura alitoa kauli yake. "Twaweza kulipwa hela nzuri sana eti" "hapana," kaka sungura alipinga. "Tukingoja kidogo tu, tutakuwa na kabichi kubwa zaidi ulimwenguni kote (uk. 41)... "Niuzie hii kabichi," Ndovu aliomba,nitaifanya kitoweo cha jamii yangu."Hapana, haiuzwa,"sungura alijibu ( uk.42).

Taharuki inajitokeza pale msimulizi anawatia wasomaji wa hurafa hamu ya kutaka kuendelea kusoma zaidi ili wajue kama Sungura alifanikiwa kuvuna kabichi kubwa kuliko zote ulimwenguni.

Kariuki (2010) ameelezea watoto ujumbe  kwamba kaka Sungura ni mwenye tamaa, anayetaka kupanda na kuvuna kabichi kubwa kuliko zote duniani. Watoto wanaposoma hurafa hiyo wana hamu ya kutaka kujua kama Sungura alivuna kabichi kubwa kuliko zote ulimwenguni kama vile alivyotaka. Usomaji wa kuzingatia hatua kwa hatua kwa watoto ili mwishoni wajue matokeo kunawaburudisha watoto. Kwa hivyo, taharuki huwapa watoto motisha ya kutaka kusoma ujumbe wa hurafa na kutekeleza dhima ya  kuwachangamsha.

Katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* Mayega (2004) ameandika hadithi kwa hali inayozua taharuki miongoni mwa watoto.Mayega anasema:

> Wakakutana kwa siri na kukata shauri kumuua mfalme Tembo ili awaodokane na utumwa huo.Lakini kila aliyemsongelea Tembo na kujaribu kupambana naye aliumwa kikatili sana.Siku moja alfajiri na mapema, kabla wanyama wote hawajaelekea mbugani, Sisimizi aliwaomba wamruhusu ili aende kupambana na Tembo. “Ha! Ha! Ha!”Wanyama wote walicheka sana. Jambo hilo liliwashangaza sana ( uk.12).

Taharuki inatokea pale wanyama wanataka kujua kama sisimizi atamuua tembo au atashindwa. Watoto pia wanaposoma hurafa hiyo watakuwa na hamu ya kutaka kuendelea kusoma ili wajue kama Sisimizi atamuua tembo au atashindwa.Hali ya taharuki imefika kilele pale Sisimizi anawaomba wanyama wenzake wamkubali amuue tembo. Baada ya kuwasihi kwa muda mrefu walikubali. Kila mnyama alitaka sana kuona mgogoro na vita baina ya tembo na sisimizi. Wanyama wanaburudika kushuhudia sisimizi akimuua Tembo kutumia ujanja na kuingia ndani ya mkongo wa tembo. Hivyo basi, mbinu ya taharuki inamwezesha mwandishi kuwatia hamu watoto kuendelea kusoma hurafa.

### 4.1.2 Matumizi ya Methali katika Fasihi ya Watoto

M’Ngaruthi (2008) amesema methali ni mali na amali ya jamii. Ndiposa zinapotumika, maneno yanayotumiwa yanaeleweka na kutokana na jamii husika. Matumizi yake hutegemea uhifadhi wake na tajriba ya watumizi wake. Asili ya neno methali ni neno ‘mithili’, yaani ‘fananisha kitu na kingine’, hivyo basi, methali hutumiwa kutolea ujumbe fulani kwa njia ya mfananisho. Maana yake, ni sawa na semi nyinginezo, huwa imefichika. Methali hasa ni kifungu cha maneno yanayotumiwa pamoja kisanii, kwa njia ya kufumba au kupigia mfano jambo fulani. Huchukua maana ndefu na pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa. Ni muhtasari wa ujumbe wa kisanii wenye maana pana iliyokubalika na jamii husika. Miruka (2011) ana maoni kuwa methali inahusu utamaduni na pia ni mali ya jamii husika. Simiyu (2011) anaeleza methali ni semi fupi zinazosheheni fumbo juu ya ukweli wa maisha ya binadamu na huwa na umbo maalum. Simiyu (2011) ameongezea kwamba methali huwa na lugha teule inayoteuliwa kwa ustadi mkubwa.

Lugha hii teule hujumuisha sitiara, tashbihi, taswira, maswali na balagha, takriri, mchezo wa maneno na tanakali za sauti. Methali huwa na maana fiche. Maana wazi hupatikana kutokana na maneno yaliyotumika moja kwa moja. Maana fiche hupatikana kutokana na matumizi ya methali husika.

Msokile (1993) amesema methali ni kazi ya sanaa ya kifasihi inayotumia mafumbo kwa kawaida semi zote zina hekima ndani yake. Ubora wa hekima hiyo hutegemea muktadha hali ambapo methali hutumika. Methali pia ina kazi ya kufurahisha, kutisha, kuonya na kadhalika. Waandishi hutumia methali na ni jukumu la mhakiki kuzitambua.

Kwa mujibu wa Wamitila (2010) Methali ni msemo wa kijadi au kimapokeo unaoeleza uzoefu fulani wa kijamii katika muundo uliofungika na ule unaobainika na kukumbukika. Pia methali ni semi muhimu katika lugha na kiungo kikuu katika matumizi ya lugha.Methali ni mbinu inayotumiwa kuwasilisha ujumbe au kuelimisha jinsi mwandishi wa hurafa angependa kwa wasomaji au wasikilizaji wa hadithi yake. Methali zinapotumiwa kupasha habari huwa na nia ya kurekebisha tabia zinazofuata maadili ya jamii. Salami, (1998) amesema mwandishi anazitumia kuipa hadithi yake muhtasari. Katika mwisho wa hadithi ujumbe unahimizwa kwa njia ya methali. Ameeleza zaidi Salami (1998) ya kwamba methali zinatumiwa kurembesha hadithi na kupamba lugha inayotumiwa na mwandishi. Prince (2003) ambaye ni mwasisi wa nadharia ya naratolojia anasema waandishi wengi wa hurafa hutumia mbinu ya methali kama semi katika matumizi ya lugha ili kuelimisha na kukuza lugha.

Kulingana na M’Ngaruthi (2008) tofauti ya methali na tamathali za usemi ni kwamba methali za

Kiswahili zimejaa ufananisho. Jambo hili huzipa sura mbili sehemu ya wazo na ile ya ufananuzi wake. Kama vile haba na haba, hujaza kibaba. Methali huwa na mdundo wa kimuziki ambapo huwa na vina na mizani. Sifa ya wazo na jibu, pia hupatikana katika mashairi ya mandhuma.

Methali zina muundo wa kishairi. Kwa mfano "Asiyesikia la mkuu, huvunjika guu" na "Asiyefunzwa na mamaye, hufunzwa na ulimwengu." Kila methali ina mizani nane katika kila sehemu.Mizani zote ni kumi na nane kwa kila methali. Methali hupambwa na tamathali za usemi na kujenga taswira ifaayo; baadhi ya tamathali hizo ni: takriri, taswira, tashbihi, istiari / sitiari, tashihisi na nahau.

Katika *Sungura na Mbwa*, Nyakeri (2011) ametumia mbinu ya methali; "Kikulacho ki nguoni mwako." Maana ya kikulacho ni kitu kile kinakusumbua. Nguo ni ile unavaa ambayo iko na wewe. Matumizi yake ni kitu kikusumbuacho hakiko mbali nawe, kama kiroboto au kunguni kikaribu na mwili wako au ndani ya nguo yako. Methali hii ilitamkwa na Panya alipomkuta Sungura akiiba mahindi ya Mbwa. Panya alishangaa kwa sababu Sungura alijulikana kama rafiki wa Mbwa. Methali hii imetumiwa na mwandishi wa *Sungura na Mbwa* katika ukurasa wa 22. Methali hii inamaanisha yule anayeweza kukutendea jambo baya si mwingine isipokuwa yule anayekujua na kukufahamu vyema. Matumizi yake kama ilivyotumiwa ni kwamba paka anamfahamu Sungura kama rafiki wa Mbwa ilhali yeye ndiye anampata usiku wa manane akiiba mahindi ya rafiki yake mbwa. Mbwa alikuwa rafiki wa Sungura. Sungura alimsaidia mara nyingi na mahindi. Umuhimu wa methali hii ni kuwaonya watoto kuhusu kujua ya kwamba rafiki wako anayekujua ndiye anaweza kukudhuru. Elimu inayopitishwa kuhusu rafiki, ambaye mtoto anastahili kujichunga naye asimdhuru jinsi sungura alivyomwibia mbwa mahindi. Pia methali hii ina umuhimu wa kuhimiza maadili mema kwa watoto. Panya alikuwa na lengo la kumkera

sungura alipomuuliza nilikuwa nafikiri wewe ni rafiki wa mbwa, kumbe "kikulacho ki nguoni mwako." Tabia ya sungura inakashifiwa.

Methali "siku za mwizi ni arobaini". Maana ya mwizi ni yule anayeiba. Akiiba ataendelea kwa muda hadi siku ya arobaini. Inamaanisha mtu yeyote anayefanya maovu kwa siri akidhani haonekani, siku moja hugunduliwa na kufumaniwa. Mwandishi wa *Sungura na Mbwa* (2011) katika ukurasa wa 25 ametumia methali hii alipokuwa anaandika vile Mbwa alivyomwambia Sungura alipompata akiiba mahindi yake. Mbwa alimwambia siku zake arobaini zimefikia mwisho. Ujumbe unaotolewa ni umuhimu wa kutoiba kwa sababu siku moja utapatikana. Mtoto anaonywa dhidi ya wizi. Kuiba hakukubaliwi kwa jamii. Sungura anapofumaniwa akiiba, msomaji anachangamka na kutaka kujua zaidi litakalotokea. Watoto katika usomaji wangemuunga mkono Mbwa na hawangependa sungura aendelee na wizi.

Methali nyingine, "akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki." Maana ya dhiki ni shida au taabu. 'faa' nayo ina maana ya saidia. Anayekusaidia wakati wa shida ndiye rafiki. Ni methali katika *Sungura na Mbwa* (2010) ukurasa wa 6 ambapo sungura aliitamka alipokuwa anamshukuru Mbwa kwa kumsaidia na chakula. Methali hii inamaanisha yule anayekusaidia wakati wa shida ndiye mwandani wako. Mbinu hii imetumiwa na mwandishi kumweleza jinsi sungura alivyojifanya rafiki wa mbwa kwa sababu alimsaidia kwa chakula. Sungura alikuwa katika shida ndipo akaenda kuomba mbwa chakula. Umuhimu wa methali hii ni kuonyesha tabia ya mbwa. Mbwa alikuwa mwenye huruma na rafiki wa kweli wa sungura. Methali hii imeelezwa kwa watoto.

Wao wanastahili kugundua anayekusaidia wakati unahitaji msaada ndiye rafiki wa mtu wa kweli. Pia watoto wanatakiwa kusaidiana wakati wana shida. Hivyo kuhimiza mbinu ya kuelimisha maadili mema katika jamii miongoni mwa watoto.

Methali nyingine ni, "chelewa chelewa utakuta mwana si wako." Maana ya kuchelewa ni kukawia. Ukikawia utakuta mwana ni wa mwingine si wako. Hiyo ni maana ya juu. Maana fiche ni kwamba ukichelewa kutenda jambo muhimu kwa wakati unaofaa unaweza kukosa kulifanya tena. Methali hii imetumiwa na Kariuki katika Ngiri *Mganga* (2011) ukurasa wa 39. Methali hiyo inamaanisha kwa lolote mtu angependa kulifanya anastahili kulifanya bila kupoteza muda. Mbinu hii ya methali inatumika katika kuwasilisha maudhui ya kuelimisha. Tamaa ya sungura inasisitizwa kwa watoto wanaosoma hurafa. Sungura alikuwa anataka mkewe akanunue mbegu zitakazoshinda zingine zote. Alitaka mke wake aharakishe kwenda sokoni. Ndipo akamwambia "chelewa chelewa utakuta mwana si wako."

Kariuki (2010) pia ametumia methali "asiyesikia la mkuu huvunjika guu", Maana ya asiyesikia ni yule anakataa kufuata mawaidha. Mkuu ni yeyote mwenye busara anayepeana mawaidha. Guu ni mguu katika hali ya ukubwa. Kuvunjika kuna maana ya mguu kuumia. Katika *Ngiri Mganga* ukurasa wa 35. Methali hii inamaanisha yule ambaye hazingatii mawaidha ya wenye busara au wazazi mwishowe huumia. Mwandishi ametumia mbinu hii ya methali ili kuwasilisha busara ya daktari Ngiri pili anakashifu tamaa ya fisi. Ngiri alimwonya dhidi ya mchafuko wa tumbo kwa kula ovyo ovyo lakini hakusikia. Ndivyo akatoa funzo kwa watoto, ya kwamba ni vizuri kuzingatia maagizo ya wale wenye busara.

"Ukipenda donda, penda na usaha wake," ni methali nyingine ambayo imetumiwa katika *Ngiri Mganga* katika ukurasa wa 17. Maana ya donda ni jeraha kubwa katika mwili ambalo halijapona

kwa muda mrefu. Usaha ni ute wa rangi ya manjano iliyopauka unaotunga katika vidonda au majipu. Maana ya juu ni kama umependa jeraha ambalo halijapona kwa muda mrefu hautaweza kuchukia usaha wa hilo jeraha. Mke wa chura anamsihi mumewe asiwachukie watoto wake kwa sababu hawawezi kuruka kama vyura wengine. Anamtuliza na kumwambia wao ni kama donda ambalo halijapona kwa wakati mrefu. Hata ingawa halijapona itawabidi pia wakubali usaha wa donda hilo. Watoto ni wao hata ingawa hawawezi kuruka kama vyura wengine itawabidi wawakubali kama watoto wao. Methali hii inawahimizia watoto wajikubali jinsi walivyo. Chochote Mungu anachokupa huwa na sababu zake.

Methali, “haba na haba hujaza kibaba” imetumiwa. Maana ya haba ni kidogo au kwa uchache. Kibaba ni mkebe mdogo. Maana yake ni ukiweka kiasi kidogo cha kitu kila mara mwishoni utakuwa na akiba kubwa. Kariuki (2010) katika ukurasa wa 25 ametumia mbinu hii. Maana ya methali hii ni kidogo kidogo mwishowe huwa kingi na kujaza kibaba. Ngiri aliitamka methali hii wakati alipokuwa kazini akitafuta dawa za kutibu wanyama. Methali hii inatumiwa kutia moyo na kuhimiza watoto kufanya kazi kama Ngiri alivyokuwa na furaha. katika hali hiyo ya kazi aliona ameikamilisha. Methali hii ni muhimu kutia watoto moyo wa kufanya kazi yoyote ile. Huo ni ujumbe unaoashiria maadili bora ya jamii. Ngiri alijishughulisha na utafutaji wa dawa za miti. Watoto pia wanahimizwa kuhifadhi mali asili ya Kiafrika kama vile dawa za miti jinsi Ngiri alivyofanya.

### 4.1.3 Matumizi ya Nahau katika Fasihi ya Watoto

Msokile (1993) ana maoni ya kuwa nahau ni semi ambazo hutumiwa na mwandishi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi. Nahau zinatumiwa pia kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha. Ngure (2011) amesema

nahau ni misemo iliyojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambayo huwa imesetiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno yayo hayo katika matumizi yake ya kawaida.

Guantai (2002) amesema ya kwamba nahau ni mafungu ya maneno yaliyopewa maana maalum na jamii. Nahau hutumika kwa njia ya kupamba kazi ya fasihi kama hurafa za watoto. Nahau pia hutumiwa na wasanii na wazungumzaji kuyakazisha maelezo yao.

Nahau hutumiwa kuelezea mbinu za matumizi ya lugha ambazo kimsingi zinahusisha ukiushi wa aina fulani ambapo neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi (Wamitila 2010). Katika fasihi ya watoto mbinu hii ni muhimu kukuza lugha. Pia ni mbinu inayotumiwa na mwandishi kupamba lugha.

Nahau "walipigwa na butwaa," imetumiwa na Kariuki (2010) katika *Ngiri Mganga* ukurasa wa 44. Maana ya pigwa ni kupatwa na. Butwaa ni mshangao. Maana fiche ya neno piga ni kupatwa na. Kumaanisha sungura alipatwa na mshangao. Nahau inawasilisha ujumbe ya kwamba sungura alishangaa kugundua kiwavi alikuwa ameila kabichi yake yote.

Vile alivyofikiria atakuta kabichi hakuipata hata chembe. Nahau nyingine iliyotumiwa na Kariuki

(2010) katika ukurasa 44 ni "aliangua kilio" nahau hiyo imetumiwa pale sungura amekuta kabichi yake imeliwa na Kiwavi. Maana yake katika muktadha huu ni kwamba sungura alilia kwa sauti ya juu alipokuta hamkuwa na kabichi. Aliudhika sana na kujuta kwa nini hakuivuna kabichi mapema. Sungura anaangua kilio kwa sababu ya tamaa. Ndivyo watoto wanaposoma hurafa wanapata funzo ya kwamba tamaa huwa na madhara.

Nahau "alijikaza kisabuni" imetumiwa na mwandishi wa Sungura *na Mbwa* ambaye ni Nyakeri

(2011) katika ukurasa wa 20. Maana ya kujikaza ni kujitahidi. Sabuni nayo hutumiwa kufulia kuogea au kusafisha vitu. Nahau hii inamaanisha alitia bidii sana. Sungura alikuwa ameyaiba mahindi mengi na mazito ya Mbwa. Alikuwa amelemewa kuyabeba lakini alijitahidi kwa lolote lile kuyabeba . Ndiyo Nyakeri (2011) akasema "alijikaza kisabuni". Watoto wanaposoma hurafa *Sungura na Mbwa* watajifunza maana ya nahau hii. Hivyo kukuza lugha.

Nahau "Shingo upande," imetumiwa na Kariuki (2010) katika *Ngiri Mganga.* kwa Mujibu wa TUKI (2004) maana ya shingo ni sehemu ya mwili inayounganisha kichwa na sehemu nyingine za mwili. Maana ya upande ni kutokuwa karibu. Maana ya shingo upande ni kukubali bila kupenda. Sungura alikuwa amemtuma mke wake amnunulie mbegu za kupanda kubwa ambazo hazina mfano mwingine. Baada ya mke wake kuzikosa alinunua zile alizopata. Sungura hakuridhika. Kwa hivyo alizichukua bila kupenda au shingo upande. Umuhimu wa nahau hii ni kuwafunza watoto kuelewa maana yake. Pili ni kupamba lugha kama mwandishi alivyoandika. Tatu ni mwandishi kuashiria tamaa ya Sungura

### 4.1.4 Ukariri

Kulingana na Guantai (2002) takriri ni kule kurudiarudia maneno au sauti kwa kusudi la kusisitiza. M'Ngaruthi (2002) ameeleza takriri ni urudiaji wa neno, silabi, sauti au wazo kwa lengo la kusisitiza jambo. Ngure (2011) akieleza zaidi amesema takriri ni tamathali inayohusika na urudiaji wa neno ili kusisitiza ujumbe. Ukariri hujitokeza kwa wingi katika nyimbo ili kutilia mkazo ujumbe unaopashwa na mhusika katika hurafa. Hurafa Ngiri *Mganga* ya kariuki (2010) katika ukurasa wa 31ametumia tamathali ya ukariri kama ifuatavyo: "Vikapu viko hapa. Vikapu vikapu. Vikapu viko hapa. Ni vyangu milele".

Ukariri umetumiwa pale Tumbili ameimba wimbo akirudia maneno kadhaa. Amerudia neno "vikapu" mara tatu na neno "viko" mara mbili. Pia neno "hapa" amerudia mara mbili. Msimulizi anataka kusisitiza ya kwamba Tumbili ndiye aliyeiba vikapu vya Ngiri lakini hataki kuvirudisha.

Ukariri umetumiwa katika maneno "ni vyangu milele", kumaanisha vikapu alivyoiba kutoka kwa Ngiri, hataki kurudisha. Tumbili alikuwa akiimba akitumia ukariri ili apashe bundi ujumbe maalum; ya kwamba ni yeye ana vikapu vya Ngiri na amevifanya viwe vyake milele. Ukariri ni muhimu kwa sababu ni mbinu moja muhimu inayoweza kutumiwa na watoto ili kusisitiza ujumbe muhimu au wazo kuu la habari yoyote. Ukariri husababisha uelewaji na huondoa tashwishi yoyote. Kama vile bundi alipata hakika ya kwamba tumbili ndiye aliyeiba vikapu vya Ngiri.

Katika hurafa ya *Sungura na Mbwa* Nyakeri (2011) ametumiwa ukariri katika ukurasa wa 14. Nyakeri anasema, "Watoto wake wadogo walikuwa wakilia. Woi mama! Woi mama! Tunakufa njaa! Woooi mama! Tunakufa njaa! Waliendelea kulia kila mara. Wanasisitiza ujumbe kwa mama yao. Maneno "Woi mama!" yametumiwa mara mbili. Maneno yaliorudiwa ndiyo ukariri. Nyakeri amedhihirisha mbinu ya ukariri. binu hii inatilia mkazo maudhui ya umaskini ya familia ya Sungura (Nyakeri 2011). Watoto wanaposoma hurafa hiyo wataelewa kwa urahisi ujumbe kuhusu kilio cha watoto wa sungura kwa sababu ya njaa. Wataelewa kwa sababu urudiaji wa maneno huondoa tashwishi yoyote kuhusu ujumbe unaopashwa.

### 4.1.5 Tanakali za Sauti

Kwa mujibu wa Bakize (2014) tanakali za sauti hueleza sauti au jinsi kitendo fulani kilivyotendeka. Mbinu hii husaidia mtoto kuelewa hali fulani na kupata picha ya maelezo. Tanakali za sauti huchangamsha mtoto na pia huvuta makini yake. Mbinu hii pia huwa pambo la

lugha. Msokile (1993) amesema ya kwamba tanakali ni neno ambalo likitamkwa huiga sauti ya kitu. M'Ngaruthi (2008) ameeleza maneno haya ambayo huiga sauti kuashiria jambo limetendeka hutumiwa kutilia mkazo jinsi kitu kilivyo. Prince (2003) ameeleza ya kwamba tanakali za sauti hutumiwa na wasimulizi wa hurafa ili kutilia mkazo au kujenga picha kamili ya kitu, kitendo au jambo linaloelezwa.

Tanakali za sauti "Ha!Ha!Ha!Ha!" zimetumiwa na Mayega katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) katika ukurasa wa 5. Simba alicheka kicheko kikubwa kujivunia nguvu yake. Mwadishi anataka watoto waelewe vile Simba alicheka. Mbinu hii husisitiza kicheko cha simba ili watoto wapate picha kamili ya msimulizi. Watoto pia huburudika na huiga hicho kicheko. Mayega tena katika ukurasa wa 5, anaeleza jinsi simba alivyonguruma. Anasema, simba alianza kunguruma, "Ngruu! mm! mm!" Sauti inayotolewa na simba anaponguruma inaonyesha ukali wake. Ujumbe kwa watoto ni kwamba sauti yoyote inayotamkwa kwa nguvu na nzito huashiria ukali (Mayega 2004).

Tanakali za sauti, " Ta ! Ta ! Ta ! Ta !" zimetumiwa katika *Sungura na Mbwa* (2010) katika ukurasa wa 21 Nyakeri alitumia tanakali ya sauti alipotaka kuonyesha mahindi aliyoiba sungura yalikuwa mazito mno. Mwandishi anasema, "Alibeba gunia moja la mahindi mpaka msituni na kulificha. Gunia lenyewe lilikuwa zito sana. Lakini alijikaza kisabuni. Alitititirikwa na jasho kama maji akitembea na gunia hilo mgongoni. Ta! Ta! Ta Ta!" Kusisitiza vile Sungura alivyokanya na hakupenda kuyaachilia mahindi. Mwandishi anabainisha tabia za sungura ambazo hazikuzingatia maadili ya jamii. Watoto kupitia ujumbe huo wanaonywa dhidi ya tabia za Sungura ambazo ni kinyume na maadili ya jamii.

#### 4.1.6 Matumizi ya Tashbihi katika Hurafa

Kulingana na Msokile (1993) tashbihi ni mojawapo wa tamathali za usemi zinazotumiwa na waandishi wa fasihi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana, mtindo na pengine sauti katika maandishi. M'Ngaruthi (2008) na Guantai (2002) wameeleza tashbihi ni ulinganisho wa moja kwa moja wa vitu viwili au zaidi vilivyo na sifa sawa kwa kutumia vilinganishi. Vinavyotumika sana ni mithili ya, kama, sawa na, na kama vile. Mbinu hii imetumiwa na waandishi wengi wa hurafa za watoto ili kukuza lugha kwa watoto. Maelezo zaidi ya kufananisha hali au kitu husababisha uelewaji wa usomaji au usimulizi wa hadithi.

Tashbihi, "Sungura amefurahi kama kibogoyo aliyepata meno" imetumika katika *Sungura na Mbwa* katika ukurasa wa 13. Mwandishi anaonyesha jinsi sungura alivyojawa na furaha kama kibogoyo aliyemea meno. Kibogoyo ni mtu ambaye hana meno au ana meno machache. Wakati anapata meno anajawa na bashasha. Tashbihi hiyo ilitumiwa na Nyakeri (2011) alipokuwa akieleza vile sungura alifurahi baada ya kupewa chakula na mbwa. Furaha iliyompata Sungura inalinganishwa na ile kibogoyo anajawa nayo baada ya kupata meno. Mwandishi anasisitiza haja aliyokuwa nayo ya chakula kwa watoto wanaosoma hurafa. Pia anataka waelewe tashbihi inayotumika kufananisha furaha. Watoto wanakuza lugha kwa matumizi ya tashbihi hiyo.

Nyakeri (2011), katika *Sungura na Mbwa* ukurasa wa 3 ametumia tashbihi "kukonda kama ng'onda." Alisema, "watoto wa sungura walianza kukonda kama ng'onda". Kukonda ni kuwa wembamba. Ng'onda ni samaki aliyepasuliwa sehemu mbili na kuanikwa juani. Tashbihi hiyo imetumiwa na mwandishi kufananisha kuathirika kwa watoto wa sungura wakawa wembamba kama ng'onda. Watoto watasoma tashbihi hiyo na kulinganisha kukonda kwa watoto wa sungura na samaki mdogo aliyekaushwa juani.

Katika ukurasa wa 11 wa *Sungura na Mbwa* (2011) tashbihi "mbwa ana bidii kama ya mchwa" imetumiwa na Nyakeri. Tashbihi hiyo ilisemwa na mke wa sungura alipokuwa anamwambia Sungura. Kilichomfanya aitamke ni kwa sababu walikuwa wanaenda kumwomba mbwa chakula. Walipofika walikuta ghala la mbwa limejaa chakula kingi. Ndiyo sungura akauliza pahali mbwa anatoa chakula hicho kingi. Mke wa sungura alimjibu mbwa ana bidii kama ya mchwa. Mke wa sungura anafananisha bidii ya mbwa kama ile ya mchwa ambaye ni mdogo lakini anaweza kujenga kitu kikubwa kwa bidii. Watoto wanaposoma hurafa wataelewa jinsi mbwa anajitahidi kufanya kazi kwa bidii jinsi mchwa anavyofanya. Umuhimu wa mbinu hii ni kumpa sifa mbwa. Aliyesifu bidii ya mbwa ni mkewe sungura kuonyesha anafanya kazi juu chini na ndiyo sababu mbwa na familia yake wana chakula kingi kwa ghala. Watoto wanahimizwa watie bidii kazini kama mbwa au mchwa. Watoto ni wadogo kama mchwa lakini kwa kutia bidii kazini wanaweza kufanya kazi kubwa. Dhima ya kuelekeza watoto bidii kazini inawasilishwa.

Mwandishi wa hurafa *Kiwavi na kabichi* katika *Ngiri Mganga* ( 2010*)* ametumia mbinu ya tashbihi kuonyesha picha ya kiwavi aliyekula kabichi ya sungura. Katika ukurasa wa 44, Kariuki anaeleza ukubwa wa Kiwavi. Anasema, "Badala yake walimuona kiwavi aliyenona kama nguruwe akigaagaa mahali hapo." Kumaanisha kiwavi alikuwa amekula kabichi ya sungura hadi akawa mkubwa kupindukia. Kariuki (2010) ameeleza jinsi kiwavi alivyokula kabichi hadi akawa mnono na anamlinganisha na nguruwe. Nguruwe ni mnyama mnono ambaye anaweza kukula na kuwa mnono kupita kiasi. Orwell (2011) ana maoni ya kuwa nguruwe anaweza kunona hadi akafikia ratili mia tatu na hata kuona vigumu kuona kwa macho yake madogo. Anasisitiza jinsi kiwavi alivyokuwa mkubwa baada ya kula kabichi ya sungura yote. Kwa kutumia tashbihi watoto wanapata picha ya jinsi alivyokuwa mnono.

Tashbihi imetumika katika *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) ukurasa wa 6. Mayega (2004) anasema, "Kisha kwa kasi kama umeme alimrukia punda milia na kumchana vipande vipande, halafu aliuliza, "Nani anabishana na mimi?" Tashbihi hii imetumiwa kuonyesha vile Simba alitumia nguvu zake kwa wanyama wengine. Punda milia alijiringa ana uwezo wa kupigana na wanyama wote. Simba alitaka ajue ya kwamba hana nguvu kuliko yeye. Kwa hivyo simba alimrukia Punda Milia na kumchana vipande vipande. Mwandishi amelinganisha haraka aliyoitumia kumrukia punda milia na ile ya umeme. Anaonyesha vile simba alivyomchana Punda milia bila kupoteza muda. Kasi ni kumaanisha haraka. Umeme una maana ya miale ya mwanga inayoonekana kabla ya radi ambayo hutokeza kwa haraka mno. Haraka hiyo inalinganishwa na ile Simba alikuwa nayo kumchana Punda milia. Watoto wanapata picha kamili na kuelewa Simba alianza kupambana na punda milia bila kupoteza muda. Kwa hivyo katika usomaji wa hurafa watoto watapata ujumbe wa mwandishi. Wakipata ujumbe wanaweza kuzitumia tashbihi kukuza lugha.

### 4.1.7 Matumizi ya Taswira katika Hurafa

Kwa mujibu wa Guantai (2002) taswira ni mbinu inayotumiwa na mwandishi ili kuwezesha msomaji kumithilisha hali fulani na kuelewa kwa undani zaidi. Mwandishi anaweza kutumia maneno kutusawiria picha ya hali hiyo mawazoni mwetu. M'Ngaruthi (2008) amesema taswira ni mbinu ya sanaa inayotumiwa na msimulizi wa hadithi ili kumwezesha msomaji kupata picha kamili ya kinachosimuliwa. Maelezo mazuri humpa mhusika sura ya mandhari, wahusika, sauti au mlio fulani au vitendo vya kutisha. Njogu na Chimerah (2011) wamesema taswira ni picha ya maono inayomjia mtu akilini mwake. Watoto wanaposoma hurafa wanaweza kuona, kusikia, kuonja, kunusa, kupenda, au kuchukizwa au kudharau kilichosawiriwa kutegemea nguvu za taswira zilizotumika.

Taswira imetumiwa na Nyakeri katika Sungura *na Mbwa* (2011). Katika ukurasa wa 18 mwandishi anaeleza jinsi sungura alivyokalia gogo. Anasema, "Kulikuwa na gogo ambalo lilikuwa karibu na mti mmoja mkubwa. Sungura aliamua kulikalia kwa muda. Mwandishi ametumia taswira ya gogo ambalo linaonekana. Wakati mtoto anaposoma hurafa, akilini mwake anaweza kuona taswira zilizotumiwa kama vile gogo lililokaliwa na sungura na sauti aliyoisikia ikitoka chini ya gogo. Picha inajengeka akilini mwa watoto na kuelewa ujumbe wa mwandishi. Taswira hurahisisha kuelewa hurafa kwa watoto.

Taswira nyingine imetumiwa na Nyakeri (2011) katika ukurasa wa 24. Kuhusu mbwa na wanawe. Mbwa na watoto wake walikaa chonjo wakimngojea mwizi atakayeingia kuiba mahindi yao. Mwandishi ameandika "Mara alipoingia ghalani, alishangaa kuwaona watoto wa mbwa wamemwelekeza kucha zao." Picha hii inajengeka akilini mwa watoto wanaposoma hurafa. Hakuna mwizi angetoroka bila kushikwa kwa jinsi walivyojipanga.

Katika *Ngiri Mganga* (2010) ukurasa wa 32, mwandishi ametumia taswira ya jinsi Ngiri alivyopatwa na usingizi baada ya kufanya kazi alichoka mno. Ndipo akaelezwa "Ngiri alifungua jicho moja kwanza, kisha akalifungua la pili. Alikuwa kama aliyefunikiwa na blanketi,

Hakuliona hata pua lake gizani." Taswira hii ya Ngiri kulifungua jicho moja halafu akafungua lingine ni taswira inayojengeka akilini mwa watoto wanaosoma hurafa. Watoto wanaelewa vile Ngiri alichoka baada ya kufanya kazi. Alikuwa amefanya kazi mchana kutwa. Mwandishi angependa watoto waelewa na wapate habari Ngiri alifanya kazi kwa bidii iliyomfanya achoke na kupata usingizi mnono. Kuonyesha Ngiri alikuwa daktari mwenye bidii kazini. Kutia bidii kazini ni muhimu kwa watoto kama vile Ngiri alivyofanya.

### 4.1.8 Ukuzaji wa Lugha

Wamitila (2003) katika amesema ya kwamba dhana ya lugha hutumiwa kuelezea mfumo wa sauti nasibu zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana kuwasiliana. Wahigi (2003) akieleza kuhusu lugha anasema lugha hutumia maneno ambayo hutumika tunapowasiliana katika maisha yetu ya kila siku.

Maneno haya yanatakiwa kupangwa kwa utaratibu maalum ili yaweze kuleta maana kamili. Collie na Slater (2010) wamekiri kuwa fasihi ya watoto hukuza lugha kwa watoto hasa wanaposoma vitabu vya hadithi za watoto kwa wingi. Vitabu kama hivi ni kama hurafa za watoto ambazo huwa na maudhui ya lugha yanayotekeleza dhima ya kufunza watoto lugha. Kwa hivyo vitabu hivi huwawezesha kuwa na umilisi wa msamiati mwingi. Kwa mfano, mtoto aliye na msamiati mwingi huweza kujimudu katika mazungumzo na kujieleza kikamilifu. Watoto wanaposoma hurafa hufaidika kwa kukuza lugha. Ngugi (2010) amesema kwamba watoto husoma ili waweze kupata uzoefu na kuelewa umbo la lugha.

Watoto wanaposoma vitabu vyao wanatambua matumizi mbalimbali ya lugha kupitia wahusika katika hadithi na baadaye kupata maarifa ya matumizi ya lugha ambayo yatawasaidia kujieleza vilivyo. Wahiga (2003) anasema lugha inayotumika katika hadithi za watoto inastahili kuwa nyepesi ili mtoto aweze kujifunza kwa urahisi na hatimaye kumjenga katika kutumia lugha hiyo. Kahigi (1995) amesisitiza ya kwamba lugha nyepesi ni sentensi sahili ambazo huundwa kwa maneno rahisi na kitenzi kimoja.

Katika *Sungura na Mbwa* cha Nyakeri (2011) mwandishi amefaulu kuwafunza watoto msamiati mbalimbali. Katika ukurasa wa kwanza (1) aya ya pili, anasema: “Kwa upande mwingine, sungura alikuwa ni mnyama mvivu. Alipenda kulala sana”. Kutokana na dondoo Nyakeri (2011)

ametumia maneno ambayo ni rahisi kueleweka kwa watoto wanaposoma. Mtoto anaposoma "sungura alikuwa ni mnyama mvivu", atang'amua maana ya "uvivu". Kulingana na dondoo, mtu anayependa kulala kila wakati bila kufanya kazi huelezwa kama mvivu, kwa hivyo inakuwa rahisi mtoto kung'amua maana ya "mvivu" kama mnyama asiyependa kufanya kazi. Sungura alipenda tu kulala.

Kutokana na *Sungura na Mbwa* (2011) sentensi inayofuata imeelezwa na mwandishi jinsi watoto wanapoisoma watang'amua maana. Katika ukurasa wa nane Nyakeri anasema: "Chakula kilichoiva, sungura alipakua na kuwagawia watoto wake". Katika usemi huo, Nyakeri ametumia sentensi sahili. Sentensi sahili au nyepesi ni ile ambayo ina kitenzi kimoja pekee na huwa rahisi kung'amua maana, kwa mfano, "Sungura alipakua chakula". Maana ya msamiati "alipakua", unaeleweka kwa urahisi na watoto kwa sababu mtoto anafahamu baada ya chakula kuiva kinatiwa kwa sahani. Hicho ndicho kitendo kinachotangulia kula. Kumaanisha msamiati "kupakua" hunaeleweka na watoto kwa urahisi. Msomaji mtoto huelewa msamiati kutokana na lugha nyepesi iliyotumika katika hurafa.

Ukuzaji wa lugha kwa watoto pia kunatokana na usomaji wa hurafa. Hurafa huwa zimeandikwa kwa kuzingatia sarufi sahihi. Wahiga (2003), amesema sarufi ndiyo uti wa mgongo wa lugha. Kwa hivyo watoto wanahitaji uzoefu wa lugha sanifu ili kukuza lugha. Jukumu hili linadhihirika katika kitabu cha Mayega (2004). Anasema:

> Simba alicheka sana. "Ha! Ha! Ha! Ha!" Kisha akasema, "Bwana Chui, acha kuonea vijana wadogo wadogo. Hebu niangalie mimi". Baada ya kusema hayo, Simba alianza kunguruma, "Ngruuu! Mm! Mm! mnanipata lakini?" aliuliza (Uk. 5).

Dondoo la hapo juu linatokana na mwandishi ambaye amefuata kanuni za lugha. Ameakifisha kwa kufungia maneno aliyoyatamka simba. Ameweka alama za mtajo. Baada ya sentensi

ameweka kikomo. Sentensi zimeanza kwa herufi kubwa. Alama ya mshangao imetumika. Kiulizi kimewekwa baada ya kuuliza swali. Kanuni za ngeli zimezingatiwa kwa mfano katika Ngeli ya (A-WA) ambayo, upatanisho wa kisarufi huzingatia nomino zote za viumbe vyenye uhai katika hali yake ya kawaida huingia katika ngeli hii kwa vile huchukua viambishi -a- na -wa- (Wahiga 2003). Ni dhahiri katika dondoo la hapo juu mwandishi ametumia upatanisho wa kisarufi kuendeleza ngeli. Anasema, “Simba alicheka”, “Vijana wadogo wadogo”. Kwa hivyo viumbe wenye uhai katika hali ya umoja huchukua kiambishi -a- na katika hali ya wingi huchukua kiambishi -wa-. Kutokana na dondoo hilo, Mayega (2004) ametumia lugha sanifu ambayo ikisomwa na watoto watapata uzoefu wa lugha sanifu na kwa hivyo kukuza lugha.

### 4.1.9 Nyimbo katika Hurafa

Kwa mujibu wa Ngure (2011) wimbo ni utungo ulio na mdundo na mahadhi na unaweza kuimbika. Miruka (2011) ameeleza ya kwamba nyimbo ni mbinu inayotumiwa na msimulizi wa hadithi ili kuwasilisha maudhui au dhima kwa wasomaji. Kwa mujibu wa M’Ngaruthi (2008) nyimbo ni maneno yanayotamkwa kwa sauti ya kuvutia na kwa mahadhi ya kupendeza. Guantai (2002) ana maoni ya kuwa nyimbo ni mbinu inayotumiwa na mwandishi kuwasilisha ujumbe. Pia hisia za ndani kabisa za mhusika anayeimba. Kulingana na Bakize (2014) msimulizi wa hadithi akiwasimulia watoto hadithi na kuona wanasinzia itambidi aimbe na kuwaomba waitikie wimbo. Akieleza zaidi Bakize (2014) amehimiza ya kwamba uimbaji wa wimbo huchangamsha watoto na wanafurahia midundo ya nyimbo. Nyimbo pia hutumika kusisitiza, kupitisha ujumbe muhimu na kufunzia maadili zinapotumiwa katika hadithi za watoto kama hurafa. Prince (2003) amesisitiza usimulizi unaburudisha watoto waliokuwa wakisoma hurafa wakianza kuimba wimbo. Kwa mfano katika ukurasa wa tano 5 wa kitabu *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) Mwandishi ameandika wimbo huu:

> Shangwe, Shangwe, umeliangusha x2 lilituonea, limeliangusha Shangwe, Shangwe umeliangusha x2 lilikuwa dikteta, umeliangusha (uk. 19).

Wimbo huo uliimbwa na wanyama waliotawaliwa na mfalme tembo. Aliwadhulumu na kuwatesa wanyama wenzake. Sisimizi alijitolea kumuua na kweli alifanikiwa. Umuhimu wa wimbo huu ni kuwasilisha maudhui ya kuburudisha. Wanyama wanaimba wakishangilia. Pia watoto wasomapo hurafa watashangilia. Dhima ya kuelimisha pia inasisitizwa. Mtoto anaposoma hurafa anagundua nguvu za mwili hazifai kuwatesa wenzake mwishowe unaweza kuangamia kama vile Mfalme Tembo alivyoangamizwa na sisimizi Mayega (2004). Watoto pia wanahamasishwa kukataa maovu yanayoangamiza. Hivyo ndivyo wanyama walivyofanya. Dhima ya kuadili ni dhima ya kutenda haki na ukweli. Dhima hii pia inawasilishwa. Tembo ameuawa na sisimizi kwa sababu alikuwa dikteta. Kumaanisha wanyama wamepiganiwa haki na ukweli na sisimizi ambaye ni mnyama mdogo. Wimbo huu upitisha ujumbe wa kuadili ambayo ni dhima ya kuelekeza watoto kupigania haki na ukweli. Wimbo umetumiwa kama mbinu na Nyakeri (2011) katika kitabu chake *Sungura na Mbwa*. Katika ukurasa wa 22 ni kama ufuatao:

> Mama, mama weee! Baba, baba weee! Tunakufa njaa, tunakufa njaa! Matumbo yanauma, mama weee! Tuokoe jamani weee!! (uk.22).

Wimbo huo uliimbwa na watoto wa sungura. Nyakeri (2011) amesema watoto wa sungura waliimba wimbo kuonyesha vile walikuwa na njaa kupindukia. Hawakuweza kuvumilia ndiyo wakawasumbua wazazi wao kwa kuimba. Wimbo huu ni muhimu katika hurafa ya sungura na mbwa. Umuhimu wake ni kudhihirisha madhara ya uvivu na uzemba. Tabia zinazoenda kinyume na maadili ya jamii husababisha njaa. Watoto wanafundishwa kutia bidii na kuchukia tabia za Sungura. Maelezo haya yanahimizwa zaidi na msimulizi, Nyakeri (2011) anapoandika wimbo ulioimbwa na kasuku katika kitabu hicho hicho *Sungura na Mbwa.*

> Mvivu rafiki ya njaa, wooi! Alalaye njaa ni mvivu, woooi! Nguvu za mtu ndicho chakula, woooi! (uk. 7)

Kasuku ndiye aliyeimba wimbo huo kupitisha ujumbe kwamba familia ya Sungura haina chakula kwa sababu ya uvivu wao. Kasuku anaimba chakula kinatokana na kutia bidii kazini. Wimbo huo ulirudiwa mara nyingi na Kasuku. Nyakeri (2011) ameeleza jinsi watoto wa Sungura walivyovutiwa na huo wimbo. Wimbo uliwalenga watoto wa Sungura wanaolala njaa kwa sababu ya kukataa kufanya kazi. Mbali na kukashifu uvivu. Wimbo huu unawachangamsha watoto wanapouimba. Umuhimu mwingine wa wimbo huu ni kuhimiza sifa ya ndege ya kupasha ujumbe. Aina ya ndege aliyetumiwa na mwandishi ni kasuku. Ndiye anaimba wimbo. Mwandishi wa kitabu *Ngiri Mganga* amewasilisha dhima ya kuburudisha kupitia wimbo ulioimbwa na Ngiri. Katika ukurasa wa 25. Ngiri aliimba hivi:

> Nusa, koroma, nusa koroma. Nina nini hapa? Matawi, mizizi na matunda viungo dawa kwa walio ugua (uk. 25).

Wimbo huo uliimbwa na Ngiri alipokuwa anatafuta dawa za kutibu wanyama. Alikuwa ananusa na kukoroma kuhakikisha ndizo anahitaji.   Wimbo huo umesisitizwa na mwandishi kwa sababu Ngiri ameuimba tena katika ukurasa wa 26. Umuhimu wa wimbo huu ni kuwasilisha furaha iliyomjaa Ngiri kazini. Wimbo unachangamsha watoto wasomaji. Wimbo pia unatilia mkazo umuhimu wa ujumbe wa kuhifadhi utamaduni wa Kiafrika. Guantai (2002) amefafanua ya kwamba wimbo huwa na nia ya kupasha ujumbe na hisia za mwimbaji. Ujumbe muhimu kwa watoto ni jinsi dawa za kitamaduni zinatumika kutibu wagonjwa. Dawa zinatokana na mali asili, matawi, mizizi na matunda. Bakize (2014) ana maoni ya kwamba wimbo huimbwa kwa lengo la kuonyesha hisia za furaha. Ngiri anaimba kutokana na furaha aliyonayo anapofanya kazi yake. Wimbo unaashiria tabia ya Ngiri ya kupenda kazi yake. Huo ni ujumbe kwa watoto wazipende kazi zote wafanyazo.

Kariuki (2010) katika Ngiri *Mganga* ametuamia mbinu ya wimbo kupasha ujumbe baina ya Bundi na Ngiri. Nyimbo hizo ni kama zifuatazo katika ukurasa wa 30 na 31. Bundi aliimba, "Vikapu viko wapi? Vikapu vikapu. Vikapu viko wapi? Na mwizi aliyeviiba?" (uk.30).

Bundi aliimba wimbo huu akiuliza aliyevichukua vikapu vya Ngiri ni nani. Alikuwa na nia ya kutaka kujua mwizi wa vikapu. Ndiyo anauliza mwizi wa vikapu ni nani. Wimbo huu ni muhimu katika hurafa *Ngiri, Mganga wa Wanyama*. Katika hurafa hii Kariuki anabadilisha njia yake ya kuandika. Kwa mujibu wa M'Ngaruthi (2008) na Bakize (2014) nyimbo huchangamsha wasomaji wa hurafa wanazoziimba. Kwa kutumia mbinu ya wimbo anataka watoto wanaosoma hurafa waimbe wimbo. Hivyo basi watoto kufurahi na kuchangamka. Bundi kwa kuimba akiuliza vikapu vya Ngiri vilipokuwa, ni njia ya kufanya uchunguzi. Njia hii inafaulu. Kwa hivyo wimbo unatumiwa kupasha habari. Tumbili anaposikiliza wimbo huu pia anajibu kwa njia ya wimbo ndiyo Kariuki (2010) amesema Tumbili aliimba hivi: "Vikapu viko hapa. Vikapu vikapu. Vikapu viko hapa. Ni vyangu milele".

Wimbo huo uliimbwa na tumbili alipokuwa anamjibu bundi kama ni yeye aliiba vikapu vya Ngiri. Kumaanisha yeye ndiye aliyeviiba vikapu. Mbinu ya wimbo ikawa inawasilisha habari bila kuudhi yeyote. Tumbili alikubali yeye ndiye ana vikapu kwa urahisi sana. Tumbili katika ukurasa huo huo (31) aliurudia wimbo. Aliimba na kukubali yeye ndiye ana vikapu. Njogu na Chimerah (2011) wamesema ya kwamba nyimbo huimbwa kueleza ujumbe muhimu kwa hadhira. Umuhimu wa kuimba wimbo tena ni kuhimiza ujumbe unaopashwa kuhusu vikapu.

Bundi aliambiwa na Ngiri Mganga amshauri tumbili ayale matunda mekundi. Ngiri alijua tumbili angeyala matunda mekundu yaliyomo vikapuni angelala fo!fo!fo!. Ndiyo bundi akaimba tena katika ukurasa wa 33:

> Tumbili mwerevu, mwenye busara. Kula matunda, kula matunda. Kula mekundu ya duara. Erevuka, kuwa mwenye busara. Kula mekundu ya duara (uk. 33).

Wimbo huu uliendelea kuimbwa na bundi baada ya kugundua tumbili ndiye aliyeiba vikapu vya Ngiri Mganga. Alitaka akule matunda mekundu yatakayomfanya alale kwa siku mbili bila kuamka. Katika wimbo huu kuna uelewano baina bundi na tumbili. Tumbili alikubali ujumbe wa wimbo na kukula matunda mekundu. Kwa hivyo wimbo unatumiwa kupasha ujumbe muhimu (M'Ngaruthi 2008). Athari ya wimbo inajitokeza pale tumbili amedanganywa na kuimba yeye ndiye ana vikapu vya Ngiri Mganga. Ni njia ya ujanja inayotumika na bundi ili Ngiri avipate vikapu vyake. Ngiri alijua tumbili akilala baada ya kuyala matunda mekundu wangevichukua vikapu vyake. Bundi aliurudia huo wimbo mara nyingi. Tumbili alifurahia wimbo na bila kupoteza wakati aliyala matunda mekundu. Baada ya kuyala matunda alishikwa na usingizi wa ghafla. Ngiri alivichukua vikapu vyake bila tumbili kujua. Nyimbo hizo kutoka kitabu *Ngiri Mganga* (2010) zimetumiwa kuwasilisha maadili kama uerevu, uvumilivu na kukashifu wizi.

Tabia zinazofuata kanuni za maadili ya jamii zinahimiziwa watoto. Ubinafsi wa tumbili unakashifiwa.

### 4.1.10 Matumizi ya Picha katika Hurafa kwa Watoto

Kwa mujibu wa Bakize (2014) picha ni michoro au vielelezo vinavyotumiwa kutunga na kuwasilisha fasihi ya watoto. Anafafanua zaidi na kusema mbinu ya picha huvutia watoto wanaposoma hadithi. Watoto wakisoma maandishi wanahusisha na michoro au picha zilizochorwa kuyaeleza.

Cass (1967) anasema picha na vielelezo katika vitabu vya watoto vinastahili kutumiwa ili watoto wanaposoma waelewe ujumbe wa hadithi wanazosoma. Anamaoni ya kwamba picha katika hadithi za watoto hushikilia makini katika usomaji wao. Rangi zinazovutia huwafanya watoto

wavutiwe na kile wanachosoma. Mwandishi anatumia picha pamoja na maandishi kwa sababu Picha pia hubeba ujumbe muhimu unaotokana na maandishi. Kwa hivyo picha hurahisisha kuelewa kwa maandishi katika vitabu vyao.


Mara nyingi wandishi wa vitabu vya watoto huchora picha zinazoelezea tabia za wanyama jinsi wanavyoonyesha. Tembo anaonyesha kuwa na uwezo na nguvu. Wanyama wadogo kama sisimizi, wanaashiria ujanja katika kutenda mambo makubwa. Ndege wanawaeleza wakiwa na uwezo wa kupeleka ujumbe na kutafuta suluhisho. Kwa hivyo kila mnyama katika hurafa huelekeza tabia maalumu ya mnyama huyo.



**Kielelezo 1:** Tembo na Sisimizi (Mayaga 2004:14)

Katika *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) picha imechorwa katika ukurasa wa 14 (Kielelezo 1). Picha hiyo imechorwa mnyama mkubwa kuliko wanyama wote ambaye ni tembo na sisimizi


ambaye ni mdogo kupita kiasi. Watoto wanalinganisha nguvu ya tembo na sisimizi na kucheka kwa sababu sisimizi alifaulu kumuua mfalme tembo. Ujumbe katika hadithi unalingana na ujumbe wa picha Mayega (2004) katika ukurasa wa 17 amesema, "Sisimizi alitamba ndani ya mkonga wa tembo na kumuua". Kwa hivyo watoto wakitazama picha wanaelewa vile walivyosoma kwa urahisi. Sisimizi ni mnyama mdogo sana akilinganishwa na wanyama wenzake. Watoto wanachangamka kupindukia kumwona tembo anayengoa miti akiuawa na sisimizi.



**Kielelezo 2:** Picaha ya Kiwavi aliyekula Kabichi ya sungura (Kariuki 2010:43).

Picha ya kiwavi katika ukurasa wa 43. Katika *Ngiri Mganga, 2010* (Kielelezo 2) imechorwa kiwavi ambaye ni mnene kupita kiasi. Amechorwa akigaagaa mahali kabichi ya sungura ilikuwa. Picha hiyo ina rangi nyekundu na manjano ambazo ni rangi zinazopendwa na watoto. kwa hivyo

zinawavutia wanapotazama vile kiwavi amekula kabichi ya sungura na kugaagaa pahali hiyo kabichi ilikuwa. Kariuki (2010) amesema, “badala ya kuona kabichi walimwona kiwavi aliyenona kama nguruwe akigaagaa mahali hapo”. Ujumbe waliosoma katika hurafa unalingana na wa picha kiwavi ameila kabichi yake hadi akanona kama nguruwe. Kiwavi amechorwa akiwa mnono sana. Watoto wanaburudika kwa kuitazama hiyo picha inayobeba ujumbe wa kiwavi kula kabichi yote na kunenepa kama nguruwe. Hakuna kabichi tena. Picha hiyo inavuta makini kwa watoto wanaposoma hurafa.




**Kielelezo 3:** Wana wa Chura Kahawia katika mashindano ya urukaji (Kariuki 2010:20)

Katika *Ngiri Mganga* (2010), ukurasa wa 20, picha ya wana wa chura kahawia imechorwa. Watoto wa chura kahawia wanaonekana wakiruka. Picha ni ya rangi nyekundu, kijani kibichi na manjano. Rangi hizo huvutia watoto na kupenda kujua zaidi kinachoendelea katika picha.

Ujumbe wa picha unatokana na maandishi wanayosoma katika hurafa. Kariuki (2010) anasema, “wana wa chura Kahawia waliruka ajabu”. Kuonyesha picha inaeleza zaidi kuhusu walilosoma. La muhimu ni jinsi wana wa chura kahawia walivyoruka kwa mtindo uliovutia ilhali ya kuwa na upungufu wa urukaji. kwa kutazama picha watoto wanaondoa uchovu kwa kuchangamka.

Picha katika hurafa *Sungura na Mbwa* (2011) imechorwa katika jalada. Sungura na mbwa wanaonekana. Sungura anabeba kikapu kilichojaa mahindi. Ghala la chakula li mlango wazi. Sungura amevaa shati ya rangi nyekundu na nyeupe lakini ya mbwa ni ya rangi nyeupe na bluu. Kikapu ni cha rangi ya bluu, nyeupe na nyekundu. Rangi zilizopakwa picha zinavutia watoto. Watoto watakuwa makini kuelewa picha na kuwa na hamu ya kusoma hurafa hiyo. Baada ya kuburudika na picha watapenda kusoma kujua mengi kuhusu sungura na mbwa.




**Kielelezo 4:** Picha katika jalada ya *Sungura na Mbwa* (Nyakeri 2011)

### 4.1.11 Lakabu katika Hurafa kwa Watoto

M’Ngaruthi (2008) na Guantai (2002) wameeleza dhana ya lakabu kama jina ambalo mtu hupewa au kujipa mbali na jina lake la kawaida. Jina hili aghalabu hunuiwa kumpa mtu sifa fulani au kulificha jina lake halisi. Lakabu hunuiwa kumsifu, kumkashifu, kusema kwa mafumbo au hata kejeli; kutokana na sifa nzuri au mbaya ya mtu ama umbo la mtu wenye kasoro fulani. Wamitila (2010) amesema mbinu ya lakabu inamrahisishia msomaji kazi ya kuwaelewa wahusika wanaopatikana katika kazi inayohusika. Prince (2003) ana maoni kwamba hii ni mbinu ya upenyezi wa mwandishi katika kazi ya kifasihi, hasa kwa kuliteua jina fulani mwandishi anamwelekeza msomaji kwenye tathmini au uelewaji fulani maalum. Katika hurafa za watoto mbinu hii hutumika na waandishi.

Katika *Ngiri mganga (2010)* lakabu zinajitokeza katika ukurasa wa 10. Lakabu “shoto” ni jina ambalo mtoto wa chura kahawia alipewa aliposhindwa kuruka kuelekea mbele kama vyura wengine. Badala ya kuelekea mbele aliruka akielekea upande wa kushoto. Marafiki wake wakaanza kumwita “shoto” likiwa ndilo jina lake.

Lakabu “Kulia” ni jina mtoto wa pili wa chura kahawia aliitwa na marafiki wake. Pia, mtoto wa pili alipewa lakabu hiyo ‘kulia’ aliposhindwa kuruka mbele kama vyura wengine. kila mara alipojaribu kuruka alielekea upande wa kulia. Lakabu “bekii” ni jina aliloitwa mtoto wa chura kahawia wa tatu. Alipozaliwa pia yeye alishindwa kuruka, alipojaribu kuruka alielekea upande wa nyuma badala ya mbele. Nafasi ya lakabu katika hurafa kama vile nadharia ya naratolojia inavyoeleza ni jinsi usimilizi wa hadithi unavyoeleweka kwa urahisi. La muhimu ni kuwawezesha watoto kuelewa wahusika wa hadithi wanazosoma. Wakielewa wahusika watapata ujumbe wa maudhui kwa njia rahisi.

### 3.1.12 Mianzo na Miishio ya Hurafa kwa Watoto

Prince ( 2003) ambaye ni mwasisi wa nadharia ya naratolojia anaeleza ya kwamba msimulizi wa hurafa hufuata fomula katika mianzo na miishio ya hadithi. Fomula hiyo huwa utaratibu unaowasilisha uelewaji baina ya hadhira au wasomaji na msimulizi. Miruka (2011) amesema hurafa hutanguliwa kwa mbinu maalum ambayo huwa makubaliano baina ya msimulizi na hadhira. Msimulizi anaomba ruhusa ya kusimulia hurafa na hadhira inaitikia kusikiliza.

Kabira na Adagala (2002) wana maoni ya kwamba mbinu moja ya usimulizi inayotumiwa katika hadithi za Afrika kama hurafa ni ya mianzo na miishio ya hadithi. Msimulizi anawatayarisha hadhira kwa kuwafanya wafikirie katika nyakati za zamani. Msimulizi anapomaliza usimulizi anawajulisha "hadithi imeishia hapo". Kulingana na Ngure (2011) mianzo na miishio ya hadithi ni mbinu inayotumiwa na msimulizi kuwa na uhusiano na hadhira yake. Anawatayarisha kuanza kufikiria katika ulimwengu wa zamani ambapo ukweli wa hadithi ulitokea. "Hapo zamani za kale" kama mbinu ya kuanza hadithi za watoto hasa hurafa hufanana. Nyingi hutumia fomula ya fasihi simulizi. Uhitimishaji ni msingi muhimu kwa hadithi nyingi za watoto, zina mielekeo ya kimaadili au ya kufunza. Huelekea kutoa "funzo" au adili fulani kwa njia bayana (Wamitila 2012). Hurafa nyingi katika fasihi ya watoto huanza kwa kuwatayarisha wasomaji au hadhira. Msimulizi au mwandishi huwapeleka katika nyakati za zamani. Katika ulimwengu wa ubunifu na maajabu (Bukenya na wengine 2007). Utaratibu wa kuanza na kumalizia hurafa huwatayarisha hadhira ya watoto kupokea maudhui ya hurafa na kuelekezwa dhima kama maadili bora. Kwa sababu hiyo Prince (2003) katika nadharia ya naratolojia anaeleza kwamba hurafa huandikwa au husimuliwa kwa fomula maalum.

#### 4.1.12.1 Mianzo ya Hurafa katika Fasihi ya Watoto

Hurafa *Kiwavi na kabichi* katika *Ngiri Mganga* ukurasa wa 38, imeanza kwa njia hii: " Hapo zamani za kale paliondokea kaka sungura mroho sana." Mbinu hiyo ya kuanza inampeleka msomaji mtoto kwa wakati wa zamani ambapo lolote lingetokea. Msimulizi anawaandaa kwa kuelewa maajabu na maelezo ya kubuni kuhusu sungura ambaye alikuwa mroho sana.

Hurafa *Sungura na Mbwa* iliyoandikwa na Nyakeri (2011) imeanziwa kwa njia hii : " Hapo kale paliishi marafiki wawili." Jinsi ya kuanza hurafa huwatayarisha hadhira. Watoto wanaosoma kitabu wanaandaliwa kuelewa maajabu yaliyotokea wakati hawakuwa wamezaliwa. Wanaandaliwa kufikiria yaliyotendeka na kuyakubali kwa sababu hawakushuhudia ulimwengu huo. Mwandishi Mayega katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) imeaanzia hivi, "Hadithi hadithi! Hadithi njoo, uongo njoo. Utamu kolea" (uk.1)

Watoto wanaandaliwa hata kuyasikia masimulizi ya kweli na yasiyo ya kweli. La muhimu ni kufurahia na kuipokea hadithi. Kwa hivyo njia zote za kutangulia hurafa zina maana ya kumhadaa msikilizaji au msomaji wa hurafa iliyoandikwa.

#### 4.1.12.2 Miishio ya Hurafa katika Fasihi ya Watoto

Mwisho wa hurafa mara nyingi huwa methali. Kwa mfano katika kitabu *Ngiri Mganga,* Kariuki (2010) ameishia hurafa *Kiwavi na kabichi* kwa methali. "Kweli mtaka yote hukosa yote." Maana yake ni mwenye tamaa kila wakati huambulia patupu. Sungura alitaka kabichi kubwa kuliko zote duniani na mwishowe akaikosa yote. sungura angekubali kuiuza kabichi kwa wateja waliotaka kuinunua haingeliwa na kiwavi. Alikataa kuiuza kwa sababu alitaka iwe kubwa kuliko ile haijawahi kuonekana. Ujumbe wa hurafa umehitimisha hadithi kwa methali. Uchanganuzi kulingana na nadharia ya naratolojia unaelekeza dhima ya kuelimisha maadili na kuonya dhidi

ya tamaa kwa watoto. Watoto wanafunzwa mwenye tamaa mwishoye hukosa vyote. Dhima ya kuburudisha imesisitizwa. Watoto wanafurahia sungura kukosa kabichi kwa sababu ya tamaa yake

Mbinu ya miishio ya hurafa huelekeza maadili bora kwa watoto katika jamii.Watoto wameonywa dhidi ya wizi, tamaa, ulaghai na mengine. Mwandishi wa hurafa anamaliza hurafa kwa kuwatoa wasomaji kutoka ulimwengu wa ubunifu na maajabu kwa ulimwengu wa kisasa (Bukenya na wengine 2007). Nyakeri (2011) katika hurafa *Sungura na mbwa* anamaliza hadithi kwa kueleza kwa nini mbwa kila wakati huwa chonjo akimngoja mwizi. Mwizi huyo anaelezewa kuwa ni sungura aliyefumaniwa akiiba mahindi yake. Ngure (2011) amesema fomula za kumalizia hadithi kama hurafa, zimelengewa kuwarejesha wasikilizaji kutoka kwenye ulimwengu wa ubunifu na maajabu na kuwapeleka katika ulimwengu halisi. Nyakeri (2011) katika hurafa *Sungura na Mbwa* ukurasa wa 26 amehitimisha hurafa jinsi ifuatavyo:

> Tangu siku hiyo, Sungura na Mbwa wakawa maadui. Mbwa aliendelea kuchunga wezi wasiingie kwake au kwa majirani kuiba. Hata sasa, usiku amsikiapo mtu, Mbwa hufikiri ni Sungura na kuanza kuonya kuwa kuna mwizi. (uk.26).

Kuligana na jinsi Nyakeri (2011) alivyomalizia hurafa ni dhahiri kwamba watoto wakisoma watajua ukweli ya kwamba zamani mbwa na sungura walikuwa marafiki. Miishio ya hurafa huwatayarisha watoto kujua ukweli wanaoshuhudia sasa. wametolewa kutoka ulimwengu wa ubunifu wa maajabu na kubainisha uhalisia wa jinsi Mbwa kila wakati huwa anawalinda wezi. Huo ndio ukweli unaonekana na watoto hata siku ya leo. Watoto wanaelekezwa udaganyifu na wizi haufai kwa sababu ndio ulisababisha uhasama baina ya mbwa na sungura. Huo ndio ukweli unaowasilishiwa watoto.

### 4.1.13 Matumizi ya Usemi Halisi katika Fasihi ya Watoto

Kwa mujibu wa Rothlin (2001) usemi halisi ni mbinu ya kisanaa inayotumiwa na wasimulizi wa hadithi za watoto na huwa ni maneno yatamkwayo na mtu mwenyewe au mhusika na huwa ushahidi wa tabia za mhusika. Pia anaeleza, umuhimu wa mazungumzo hutegemea usemi halisi. Nikolojeva, (2002) amesema mhusika anapewa sifa na tabia zake kulingana na jinsi anavyoongea na jinsi wengine wanavyosema kuhusu yeye. Mbinu hii huburudisha wasomaji watoto. Wanafurahia kusikia jinsi wahusika walivyosema, kuliko kila wakati kuelezwa na msimulizi. Nadharia ya naratolojia inaelekeza ustadi wa mwandishi katika kujenga wahusika (Prince 2003). Mwandishi anajenga wahusika kwa matamshi yao ili kurahisisha kuwasilisha ujumbe kutokana na hurafa kwa watoto.

Usemi halisi uliotamkwa na sungura katika *Sungura na Mbwa* ukurasa wa 17 : "Kisirani, kumbe bado, unanifuata? Mungu wangu niokoe!". Sungura alijiambia akitoka shimoni pole pole. Ujumbe wa ubinafsi wa sungura unabainisha sungura alikuwa anaenda kuiba mahindi ya mbwa. Alikutana na mbwa mtu usiku wa manane akienda kuiba. Watoto wanaposoma hurafa wanachukia tabia za sungura. Usemi katika ukurasa wa 41 ulisemwa na Sungura. Usemi huu umedondolewa katika kitabu *Sungura na mbwa* (2011) Ni kama ufuatao:

> Rafiki mwema mbwa, naomba unisaidie chakula. Watoto wangu wana njaa," alimwambia mbwa kwa sauti yenye hisia za majonzi "chakula katika shamba langu kililiwa chote na wanyama wengine juzi juzi tu," alidanganya mbwa (uk.4).

Nyakeri (2011) amempa sungura nafasi ya kudanganya mbwa. Alisema chakula chake kililiwa chote na wanyama wengine. Sungura anatumia tabia za hila kuomba mbwa chakula. Mwandishi anawasilisha ujumbe ya kwamba sungura ana tabia zinazovuruga amani miongoni mwa wanajamii. Kwa mujibu wa Nyakeri (2011) sungura anapenda vitu vya bure bwerere. Maneno

aliyotamka sungura mwenyewe katika uemi halisi ni dhihirisho ya tabia ya udanganyifu wa sungura. Hata ingawa mbwa alimsaidia sungura kwa chakula alifanya hivyo shingo upande kwa sababu aliona yeye ni mzembe.

Usemi halisi ulisemwa na mbwa katika ukurasa wa 13 wa kitabu *Sungura na* Mbw*a* (2011) ni kama ifuatavyo: “Hii ndio mara ya mwisho kukusaidia. Ni lazima ujikaze kulima shambani. Usiwategemee wengine, unasikia?” Umuhimu wa usemi huu ni kukashifu uzembe wa sungura ambao hauzai matunda. Watoto wanaposoma hurafa *Sungura na Mbwa* (2011) wanapendezwa na tabia za Mbwa za upole, huruma na bidii kazini.

Semi halisi pia zimetumika katika *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) Katika ukurasa wa 1 mwandishi ametueleza vile Nyati alivyosema, Anasema, “mmeuona ukali wangu? Nani anaweza kufanya namna hiyo?” Umuhimu wa usemi huu ni kuhimiza jinsi waliojidai wana nguvu walivyotesa wengine. Huyu ni nyati aliyeanzia kutesa wanyama wenzake. Katika kitabu hicho pia, chui anaelezwa akitumia usemi: “ Huo ni mchezo mdogo sana.” Alijitokeza akasema, “Hebu niangalieni mimi,” Usemi huu unahimiza jinsi wanyama wenye nguvu walivyoendelea kuwadhulumu wenzao. Mwingine aliyetumia usemi halisi kuonyesha nguvu zake ni simba. Katika hurafa *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) simba alisema, “ Bwana chui, acha kuonea vijana wadogo wadogo, hebu niangalie mimi,” kumaanisha yeye anajihisi ndiye ako na nguvu kuliko wanyama wote. Semi hizi zinawasilisha maudhui kuonyesha hatari ya dhuluma. Baadaye watatafuta mbinu za kupata suluhisho hata ingawa ni wadogo kwa umri na miaka. Pia watajiepusha na dhuluma. Katika *Ngiri Mganga* ukurasa wa 32 mwandishi ametumia usemi halisi ufuatao:

> Hivi vikapu vimeshonwa vizuri sana. Navitaka viwe vyangu," Tumbili alijibu , "Nimetamani vikapu kama hivi kwa muda mrefu sana. Isitoshe, haya matunda ninayamezea mate," "Usiniambie kuwa unaweza kula matunda hayo!" Bundi alisema kwa mshangao. " Siyo lazima niyale mimi naweza kutupa vyote vilivyomo. Hii ni takataka tu! (uk.32).

Usemi ulionenwa na mhusika tumbili na bundi ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe. Ujumbe huo unahusu vikapu vya Ngiri. Bundi ameyaelewa mafikira ya tumbili (Mwizi wa vikapu). Bundi ametumiwa na mwandishi kama mhusika muhimu wa kupeleka ujumbe. Bundi ni muhimu katika usemi huu kwa sababu ndege wote katika hadithi huwa ishara ya kuwezesha mawasiliano. Pia ndege wanatumiwa kuharakisha ujumbe kwa mlengwa. Mwandishi anawasilisha maudhui ya kuelimisha watoto. Mwizi kila wakati hufumaniwa na hujulikana.

Tumbili anafumaniwa kutokana na usemi halisi alionena yeye mwenyewe (kariuki 2010). Amesema yeye ndiye ana vikapu vya Ngiri na anavitaka viwe vyake. Habari hii inachangamsha wasomaji watoto na pia mhusika Ngiri na bundi. Usemi huo unawaonya watoto dhidi ya wizi na ulaghai. Kwa mujibu wa Kariuki (2010) mwizi anaendelea kuiba lakini siku moja hujulikana kama vile Tumbili alijulikana kama mwizi wa vikapu.

### 4.1.14 Sauti ya Msimulizi katika Fasihi ya Watoto

Prince (2003) ambaye ni mwasisi wa nadharia ya naratolojia anasema msimulizi wa hadithi anaweza kuwa na hadhira wanaomsikiliza au wanaosoma vitabuni. Msimulizi huwa na nafasi ya kuongeza au kupunguza kile anachokiandika. Nafasi ya msimulizi wa hurafa ndiyo sauti ya msimulizi. Kwa mujibu wa Prince (2003) msimulizi huwa na nafasi ya kuwaeleza wahusika wake jinsi anavyotaka ili kuwasilisha maudhui kwa wasomaji wake. Akieleza zaidi Prince anasema hurafa nyingi huandikwa kwa msimulizi kutumia nafasi ya tatu. Wamitila (2010) akiunga Prince (2003) mkono amesema ya kwamba msimulizi au sauti ya msimulizi inaweza kuwa katika nafasi ya kwanza (mimi), nafasi ya pili (wewe) au nafasi ya tatu (yeye). Msokile

(1993) amesema hata ingawa nafasi ya msimulizi huwa katika nafasi ya kwanza , ya pili na ya tatu ,wasimulizi wengi husimulia hadithi katika nafasi ya tatu. Akieleza zaidi, Msokile anasema nafasi ya tatu huwa na kiambishi "a" au mofimu {a} katika hali ya umoja na kiambishi "wa" au mofimu {wa} katika hali ya wingi. Jina lingine la nafasi ya tatu ni nafsi ya tatu.

Prince (2003) ameeleza ya kwamba katika hurafa nyingi za watoto msimulizi huwa katika nafsi ya tatu (yeye). Mofimu {a} katika hali ya umoja na {wa} katika hali ya wingi ndio zinatumiwa. Umuhimu wa nafsi hii ya tatu (yeye) ni kumwezesha msimulizi kuwa nje ya ulimwengu wa hadithi kwa namna inayomwezesha kutoka sehemu moja hadi nyingine. Pili ni kupenya kwenye mawazo au akili za wahusika wanyama. Kulingana na nadharia ya naratolojia usimulizi huwa unahusishwa na mtazamo wa nje.

Sauti inayosimuliwa katika vitabu teule iko katika nafsi ya tatu (yeye). Kwa mfano hurafa *Ngiri Mganga wa Wanyama* (2010*)* ukurasa wa 23, msimulizi anasema "Ngiri alikuwa mtia bidii sana kwa kazi zake." Sauti ya msimulizi inatambulika pale ambapo Kariuki (2010) amesema Ngiri alikuwa mtia bidii sana kwa kazi. Mofimu {a} imetumiwa kuonyesha nafsi ya tatu umoja katika neno "-a-likuwa". Sauti ya msimulizi katika nafsi hiyo inampa Kariuki (2010) nafasi ya kumweleza mhusika Ngiri jinsi atakavyoeleweka na watoto kama mnyama mwenye bidii kwa kazi yake. Mwandishi anamsifu mhusika Ngiri vile anavyotaka ili kuwasilisha ujumbe kwa watoto wanaosoma hurafa.

Katika hurafa *Ngiri Mgang*a (2010) sauti ya msimulizi nafsi ya umoja imetumika. Mwandishi katika ukurasa wa 33 anasema, "tumbili alikaa kitako na kumsikiliza bundi." Mofimu {a} pia imetumiwa katika hali ya umoja kutokana na neno "-a-likaa." Kariuki ameeleza hali ya tumbili

baada ya kusikia wimbo. Anahimiza kwa watoto wanaosoma hurafa vile wimbo ulivuta makini ya Tumbili.

Mifano kutoka kitabu *Sisimizi Amuua Tembo* ukurasa wa 10: Wanyama wengine kuona vile alivyotendewa simba walikunja mikia yao kuonyesha adabu zao kwa tembo." Neno "wanyama" lina kiambishi wa- ambacho ni sauti ya msimulizi nafsi ya tatu hali ya wingi. Pia hali ya umoja imetumiwa kwa neno "a-livyotendewa." Mayega (2004) amepenya kwenye wahusika na kuonyesha vile Simba alishindwa kupigana na Tembo. Katika hali hiyo Tembo akajipatia ufalme wa wanyama. Kutokana na sauti ya msimulizi inayomwezesha kutawala akili na mafikira ya wahusika ili kuwaeleza, Mayega anaeleweka kwa urahisi na watoto wanaosoma hurafa vile tembo alijipatia uongozi.

Katika *Sungura na Mbwa* mwandishi ametumia usimilizi katika nafsi ya tatu. Ameandika, "Sungura na jamaa yake waliendelea kuishi maisha ya kubahatisha". Kiambishi wa- katika neno "Wa-liendelea" ni neno linaashiria nafasi ya tatu hali ya wingi. Mofimu wa- imetumiwa katika ukurasa wa 12. "Mbwa alifungua mlango akawaona sungura na mkewe wakiwa…" Nafsi ya tatu wingi katika neno "wa-kiwa" imetumiwa. Nyakeri atasema lolote analotaka kuhusu sungura na familia yake ili kupasha ujumbe kwa watoto vile wataelewa jinsi walivyokuwa. Katika neno " -a-lifungua" . Msimulizi amesimulia kwa nafsi ya tatu umoja. Kiambishi -a- kama mofimu kimetumiwa. Nafsi hii ya tatu umoja na wingi iliyotumiwa inamwezesha mwandishi kupenya kwa njia yoyote katika kuwaeleza wahusika wanyama na kwa kufanya hivyo dhima na maudhui yanajitokeza kwa watoto.

## 4.2 Hitimisho

Sura imekuwa na lengo la kuchunguza na kudhihirirsha aina za mbinu zinazotumika katika hurafa kwa manufaa ya watoto. Hurafa huwasilisha maudhui na dhima kwa watoto kwa njia ya usimulizi. Nadharia ya naratolojia imetumika kuchanganua usimulizi uliotumiwa katika hurafa. Nadharia hiyo pia hueleza mwandishi hutumia mbinu mbalimbali ili kuwezesha kuwasilisha ujumbe wa maudhui na kuchanganua dhima kwa watoto.

Mbinu ya taharuki katika kuwasilisha maudhui na dhima kwa watoto imepatikana kuwapa watoto motisha ya kuendelea kusoma hurafa. Watoto wanapovutiwa huwa na hamu ya kutaka kuendelea kusoma. Dhima ya kuimarika katika usomaji, ukuzaji wa msamiati na lugha sanifu inaelekezwa kwa watoto.

Watoto wanapopata hamu ya kutaka kuendelea kusoma hurafa wanagundua ujumbe wa maudhui. Ujumbe huo huelekeza dhima ya ushindi wa wanyama wadogo kama sisimizi kumuua fisi. Methali imebainisha maudhui ya kuelimisha, kuonya, maadili bora na ukuzaji wa lugha. Methali huelimisha maadili ya kutia bidii kazini na kutokosa matumaini.

Kupitia hurafa usanaa wa mwandishi kutumia mbinu za kukuza lugha kama nahau, ukariri, tanakali za sauti, tashbihi na matumizi ya taswira ulichangia kurahisisha kueleweka kwa ujumbe wa maudhui kama vile wandishi wa hurafa wanavyotaka kuwasilisha kwa watoto. Watoto wanaposoma hurafa wanaongeza msamiati na kupata uzoefu wa usanifu wa lugha.

Matumizi ya nyimbo katika hurafa yamebainishwa kama njia ya kuwaburudisha watoto. Watoto wanapoimba nyimbo katika usomaji wanachangamka na kufurahia. Nyimbo zimepatikana kuwasilisha hisia na ujumbe wa furaha, ushindi au huzuni. Matokeo ya uchanganuzi wa picha

katika hurafa yamethibitisha kwamba picha hubeba ujumbe wa maudhui na huelekeza dhima muhimu kwa watoto. Picha ya tembo inaonyesha uwezo na nguvu. Sisimizi, nyuki na mche wanaashiria ujanja katika kutenda mambo makubwa.

Mbinu ya mwandishi ya kutumia Lakabu katika hurafa huwa na nia ya kuelekeza wasomaji watoto tathmini au uelewaji fulani maalum. Watoto wanarahisishiwa kuwaelewa wahusika wa hurafa kutokana na tabia zao. Utaratibu wa kuanza na kuhitimisha hurafa ni mbinu ya mianzo na miishio ya hurafa. Utaratibu huu unarahisisha kuendeleza maudhui ya hurafa na kuhitimisha hadithi kwa watoto. Mwanzo hutekeleza dhima ya kuwatayarisha watoto kupokea hurafa. Kuhitimisha kunawatayarisha watoto kuelewa kwa hali halisi ya maisha jinsi mtoto anavyoshuhudia wakati wa sasa. Miishio kama "...hivyo ndivyo sababu mbwa na sungura hadi sasa ni adui na hawaonani" au "Hiyo ndiyo sababu mbwa anakaa akibweka hadi leo akitafuta mwizi wa mahindi yake ambaye ni Sungura." Matumizi ya usemi halisi ni usanaa wa mwandishi kurahisisha watoto kuelewa wahusika wa hurafa. Usemi halisi wa mhusika mwenyewe hudhihirisha tabia kutokana na matamshi yake mwenyewe. Watoto wanachunguza malengo ya wahusika bali na kuelezwa na mwadishi. Kwa njia hiyo maudhui ya hurafa na ujumbe kwa watoto yanaeleweka.

Sauti ya msimulizi inathibitisha kwamba mwandishi huwa na uhuru wa kupenya na kuwaeleza wahusika wake vile anavyopenda. Hurafa kwa wingi hutumia nafsi ya tatu, umoja na wingi. Mwandishi anapoeleza -a- aliiba au -wa- waliiba. Anatumia kiambishi -a- katika hali ya umoja au kiambishi -wa- katika hali ya wingi. Kwa hivyo sauti ya msimulizi kutokana na hurafa ni muhimu katika kuthibitisha maudhui na dhima zilizoelekezwa kwa watoto. Sura inayofuata ni kuhusu muhtasari wa kila sura, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Utafiti ulijikita katika kuchunguza dhima, maudhui na mbinu zilizotumika kuwasilishia watoto dhima na maudhui. Hurafa zimechanganuliwa katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Vile vimetumika ni *Ngiri Mganga* (2010*)* cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimiz*i *Amuua Tembo* (2004) cha Mayega. Utafiti ulinuia kuafiki malengo matatu. Kubainisha dhima za hurafa katika fasihi ya watoto, kudhihirisha maudhui ya hurafa kwa watoto na kuthibitisha mbinu zilizotumiwa katika hurafa kuwasilishia watoto dhima na maudhui. Ili kufanikiza malengo hayo nadharia ambazo zimeongoza utafiti ni mbili. Nadharia ya semeotiki ilitumika kuchanganua dhima na maudhui muhimu kwa watoto. Nyingine ni nadharia ya naratolojia kwa kupitia mbinu za usimulizi zilizotumiwa kuhakiki hadithi. Wandishi wa hurafa wanatumia mbinu mbalimbali ili kuwasilisha ujumbe wa hadithi kwa watoto.

## 5.1 Muhtasari wa Matokeo

Sura ya kwanza imeshughulikia mambo muhimu katika utafiti huu. Yaliyoangaziwa ni usuli, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili imelenga kubainisha dhima za hurafa katika fasihi ya watoto. Dhima ya kuelimisha watoto kuhusu maadili yanayokubaliwa na jamii. Watoto wameelimishwa kuwa na subira na matumaini, wema, huruma, ukarimu, bidii na ucheshi kazini jinsi Ngiri mganga alivyojitokeza. Matokeo ni kwamba hurafa huelimisha watoto ya kwamba tabia za wahusika wanyama kama Ngiri huvutia na zinastahili kuigwa na watoto. Hurafa zimebainisha dhima ya kuonya watoto

dhidi ya udanganyifu na unafiki. Matokeo ni kwamba ukweli kila wakati ugunduliwa. Watoto wanahimizwa kuzingatia haki na ukweli. Isitoshe dhima ya kuburudisha kwa watoto kutokana na hurafa imebainishwa. Matokeo ni kwamba kutokana na usomaji wa hurafa watoto huchangamka na hufurahia kejeli, kinaya, ucheshi wa wahusika wanyama na ushindi wa wanyonge. Dhima ya kuelekeza watoto kuhusu matokeo ya ubinafsi, unafiki, udanganyifu imefafanua ya kwamba watoto wanatakiwa kutenda mema yanayoleta umoja na amani kwa jamii. Watoto wanahimizwa kutenda kinyume cha matendo ya sungura.

Sura ya tatu imelenga kuchunguza maudhui yaliyobainishwa katika hurafa. Maudhui yamedhihirisha ujumbe unaoelimisha na kufunza watoto. Katika hurafa maudhui ya tamaa yamebainishwa. Ujumbe katika maudhui haya ni kwamba watoto wasiwe na tamaa kwa sababu inaweza kuwafanya wakose kila kitu jinsi sungura alivyokosa. Maudhui ya wizi katika hurafa yamekuwa na ujumbe ya kuwa tumbili na aliaibika kwa sababu alijulikana kama mwizi wa vikapu vya Ngiri vya dawa. Ujumbe huo unalenga kuonyesha watoto kuiba ni kubaya. Uzembe na umaskini katika hurafa ni maudhui yanayotolea watoto ujumbe ya kwamba kukataa kutia bidii kwa kazi yoyote kunaweza kusababisha umaskini. Sugura alikataa kufanya kazi hata ya kulima na akawa maskini ambaye alikosa hata chakula cha familia yake. Kwa hivyo watoto wasiwe wazembe na waepukane na umaskini.

Matokeo ya sura yamebainisha maudhui ya utamaduni yamepatikana katika hurafa. Maudhui haya yanasisitiza watoto kuhifadhi tamaduni za jamii. Mila na desturi za jamii zinazosababisha amani. Pia watoto huelekezwa kuthamini mali asili kama matawi, matunda na mizizi kama dawa muhimu zinazotibu.

Hali kadhalika maudhui ya dhuluma yalipatikana katika hurafa yakihimiza umuhimu wa kupinga unyanyasaji na kupigania haki. Hata ingawa hurafa zinalenga watoto wanafundishwa kwa mbinu mbalimbali kushinda jinsi sisimizi alivyoshinda.

Sura ya nne ililenga kuonyesha mbinu zilizotumiwa na wandishi wa hurafa kupitisha maudhui na dhima kwa watoto. Mbinu hizi ni taharuki, methali, nahau, ukariri, tanakali za sauti, matumizi ya tashbihi, matumizi ya taswira, nyimbo, picha, lakabu, mianzo na miishio ya hurafa, matumizi ya usemi halisi na sauti ya msimulizi.

Ni wazi kwamba mbinu ya taharuki inapotumiwa na mwandishi katika hurafa huwapa watoto hamu na motisha ya kutaka kuendelea kusoma hadithi. Wototo wanaposoma hurafa wanausoma ujumbe wa maudhui unaowaelimisha na kuwaonya.

Ilibainika ya kwamba mbinu ya ukuzaji lugha ilitumika katika hurafa. Watoto wanajifunza matumizi ya lugha, uzoefu wa lugha sanifu na kupata ustadi wa kusoma hadithi. Ilipatikana ya kuwa methali, nahau, ukariri, tanakali za sauti, tashbihi na taswira zilitumika katika hurafa ili kukuza lugha kwa watoto. Sentensi sahili zilizotumiwa katika hurafa na maneno yanayoeleweka na watoto katika hurafa husaidia kujenga uzoefu wa lugha.

Nyimbo zinatumiwa kama mbinu ya kupasha ujumbe muhimu. Watoto wanaposoma hurafa wanapata ujumbe muhimu. Imebainika kuwa watoto wanapoimba jinsi wimbo umeandikwa katika hurafa wanachangamka na kuburudika. Imedhihirika kwamba wimbo husisitiza ujumbe muhimu kwa watoto kutokana na maudhui ya hurafa. Ujumbe huo unaweza kuwasilisha hisia za huzuni au furaha kulingana na nia ya mwandishi.

Imebainika ya kwamba picha zimetumika na ili kuwasaidia watoto kuelewa ujumbe wa maudhui. Picha huwa zimechorwa kuhusu maelezo ya maudhui kwa hivyo watoto wanapotazama picha watalinganisha kile walisoma na wanachoona kinafanyika katika mchoro. Watoto wanavutiwa na kuburudika kutokana na picha wanazotazama. Kwa mfano, picha ya Tembo akiwa mkubwa akilinganishwa na sisimizi inawashangaza watoto jinsi Sisimizi alivyoweza kumwangamiza Tembo. Rangi zilizopakwa picha huwa zinavutia. Hili lilidhihirisha ya kwamba watoto wanapendezwa na rangi nyekundu, manjano, bluu na nyeupe. Picha huashiria maana muhimu kwa watoto. kama sisimizi, nyuki na mchwa wanajulikana kwa kuwa wadogo lakini wanatenda mambo makubwa. Kwa hivyo kila picha katika hurafa urahisisha uelewanaji baina ya msomaji na mwandishi. Picha hurahisisha watoto kupata maudhui ya hurafa.

Imedhihirika ya kuwa lakabu hutumiwa na ili mtoto anaposoma hurafa aelewe kuhusu tabia za wahusika. Hii ni kwa sababu majina ya lakabu hupewa wahusika wa hurafa kulinganana na tabia zao. Majina hayo wanaweza kupeanwa na wengine au wandishi.

Mianzo na miishio ya hurafa ni mbinu inayotumiwa na wasimulizi wa hurafa. Msimulizi anaanza usimulizi kwa kuomba hadhira ruhusa na wanakubali. Hiyo ndiyo sababu wanaanza kwa kusema "hadithi hadithi," hadhira inajibu "hadithi njoo". Kwa kusema hivyo katika hurafa msomaji mtoto anashiriki kwa kukubali kusimuliwa.

Msimulizi pia anawapeleka wasomaji watoto katika nyakati za kale, anawambia "hapo zamani za kale" Watoto wanatayarishwa kwa wakati hawakuwa wamezaliwa na wanakubali maajabu ya hadithi jinsi ilivyo. Katika miishio ya hurafa, watoto wanajulishwa ukweli wa yaliyomo yale wanayaona. Kwa mfano, mbwa anakaa akibweka akiona mgeni yeyote kwa sababu anafikiria mgeni ni sungura aliyemwibia mahindi yake.

Imepatikana ya kwamba usemi halisi husaidia watoto kuelewa ujumbe wa maudhui wanaposoma hurafa. Ujumbe unaolengewa watoto hueleweka rahisi. watoto wanaposoma hurafa uelewa sifa za wahusika katika usemi halisi uliotamkwa na wahusika. Unafiki na ulaghai wa sungura unajulikana kutokana na matamshi yake mwenyewe. Anamdanganya mbwa ya kwamba chakula chake chote kiliibwa na wezi. Alisema hivyo ili mbwa amsaidie kwa chakula. Sungura alipewa chakula lakini pia aliendelea kuiba mahindi ya mbwa. Alifumaniwa akiwa anaiba na mbwa mwenyewe.

Maudhui ya dhuluma yanaeleweka na watoto kwa matumizi ya semi halisi zilizotamkwa na wanyama. Watoto wanaposoma hurafa wanakubali tembo ni mwenye dhuluma kwa wanyama wengine kutokana na usemi wake mwenyewe. Matamshi ya tumbili mwenyewe yanaonyesha watoto wanaosoma hurafa ya kwamba yeye ndiye mwizi. Hilo linatokana na jinsi alivyosema ya kwamba vikapu ni vyake milele.

Imedhihirika kwamba usemi halisi uliotumiwa na mwandishi wa hurafa unasababisha kicheko kwa watoto wanaosoma hurafa. Kugunduliwa kwa mwizi tumbili kunazua kicheko. Mwizi wa vikapu vya Ngiri amejitangaza yeye mwenyewe. Usemi halisi huwa muhimu katika utambuzi wa sifa za mhusika tumbili kwa wasomaji watoto.

Matokeo ya kuchunguza mbinu ya sauti ya msimulizi katika hurafa ni kumfanya msomaji mtoto wa hurafa kuelewa wahusika. Sauti ya msimulizi nafsi ya tatu humpa mwadishi uhuru wa kuwaeleza wahusika wake vile anavyotaka. Kwa hivyo ujumbe wa maudhui ataueleza vile utaeleweka na wasomaji wa hurafa. Kwa hivyo matumizi ya sauti ya msimulizi humpa msimulizi au mwandishi nafasi ya kueleweka na watoto wanaposoma hurafa.

Sauti ya msimulizi nafsi ya tatu humpa mwandishi uhuru wa kuendeleza ujumbe wa maudhui ya hurafa vile anavyotaka. Jinsi sungura alivyoiba chakula cha mbwa inaeleweka na watoto kutokana na maelezo ya mwandishi. Kwa hivyo sauti ya msimulizi urahisisha kueleweka kwa maudhui yanayodhihirisha dhima kwa watoto.

## 5.2 Mahitimisho

Utafiti umegundua ya kwamba hurafa zinawasilisha dhima ya kuelimisha watoto kuwa na maadili yanayokubaliwa kwa jamii. Maadili haya ni subira, wema, ukarimu, ucheshi, furaha, na kuwa na matumaini. Hurafa huelimisha watoto kuepukana na maovu kwa jamii. Utafiti umebainisha hurafa huwa na dhima ya kuonya watoto ubaya wa kudanganya kwa sababu hurafa zimebainisha ukweli baadaye hujitokeza. Utafiti umedhihirisha hurafa huburudisha watoto wanaposoma hadithi. Wanaposoma wanatambua raha kutokana na jinsi wahusika walivyoelezwa na mbinu za ucheshi zilizotumiwa na wandishi wa hurafa. Hurafa huelekeza watoto kuwa waminifu kwa marafiki zao si kama jinsi sungura alivyokuwa rafiki mnafiki wa mbwa.

Maudhui ya tamaa na wizi yamebainishwa katika hurafa yakihimiza ujumbe kwamba watoto wasitamani vitu vya wenyewe na kuiba. Hurafa zimedhihirisha uzembe wa sungura ulimfanya kuwa maskini. Watoto wanasisitizwa kuwa wenye bidii kwa lolote wanalotakiwa kufanya ili kuepukana na umaskini.

Utafiti umebainisha maudhui ya utamaduni. Husisitiza mila na desturi za jamii ni muhimu kuzingatiwa na watoto. Hayo ni pamoja na kuchukulia umuhimu wa dawa za kiyenyeji. Utafiti umechangia ya kwamba maudhui ya dhuluma huimiza watoto kukataa dhuluma na unyanyasaji na kutetea haki.

Utafiti umechangia kwa kubainisha ya kwamba katika fasihi ya watoto mbinu mbalimbali hutumika katika hurafa kubainishia watoto dhima na maudhui. Katika hurafa mbinu ya taharuki, methali, nahau, ukariri, tanakali za sauti, matumizi ya tashbihi, matumizi ya taswira, nyimbo, lakabu, mianzo na miishio ya hurafa, matumizi ya usemi halisi na sauti ya msimulizi zimetumika. Zimetumika kubainisha dhima na maudhui muhimu kwa watoto.

Hurafa zimebainishwa kuwa na manufaa kwa watoto. Zina dhima, maudhui na mbinu zinazotumiwa kupitishia watoto ujumbe. Utafiti una manufaa kwa wizara ya elimu inaoyoshughulikia masomo ya watoto hasa kuhusu fasihi. Vilevile utafiti umechangia pakubwa kuonyesha umuhimu wa hurafa katika fasihi ya watoto. Jambo ambalo litawafanya wandishi kuandika vitabu vingi kuhusu hurafa.

### 5.3 Mapendekezo kwa Tafiti zijazo

Utafiti huu umeshughulikia maswala ya dhima za hurafa katika vitabu *Ngiri Mganga* (2010), *Sungura na Mbwa* (2011) na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004). Malengo ya utafiti yamekuwa kuchunguza dhima za hurafa kwa watoto, pili kubainisha maudhui ya hurafa kwa watoto na tatu kuthibitisha mbinu za hurafa zilizotumika katika usimulizi. Bali na hivyo kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika fasihi ya watoto. Utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu dhima za hurafa katika tanzu zingine katika fasihi ya watoto. Hizi ni kama bembelezi, nyimbo na semi. Pia utafiti unaweza kufanywa kwa kutumia nadharia nyingine bali na ya semeotiki na naratolojia zile zimetumika katika utafiti huu. Hali kadhalika utafiti unaweza kufanywa kuhusu hurafa za watoto za wandishi wengine bali na *Ngiri Mganga* (2010) cha Kariuki, *Sungura na Mbwa* (2011) cha Nyakeri na *Sisimizi Amuua Tembo* (2004) cha Mayega.

## MAREJELEO


Akinyi, D.O. (2018). *Ufasiri wa Ngano za Kifantasia Miongoni mwa Watoto wa Shule za Msingi*: Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa).

Alembi, E. (1991). *Oral an Analysis of Style and Social Significance of the Abanyole Children's Oral Poetry*. M.A. Thesis Kenyatta University. (Unpublished).

Bakize, L.H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Nairobi: Moccony Printing Press.

Benton, M & G. Fox (1985). *Teaching Literature: Nine to Fourteen.* New York: Oxford University Press.

Brooks, E. (1979). *Language and Thinking in School.* New York: Rinehert and Winston.

Bukenya, A.S. (1997). *Oral Literature: A Senior Course.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Cass, J.E. (1967). *Literature and the Young Child*. London: Longman Group Ltd.

Collie, J, & S, Slater. (2010). *Literature in the Classroom: A Resourse Book of Ideas and Activites.* Cambridge: Cambridge University.

Crystal, D, (1997). *The Cambridge Encyclopaedia of Language*. Cambridge: Cambridge University Press.

Farsi, S.S. (1979). *Swahili Sayings from Zanzibar.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Finnegan R. (1970). *Oral Literature in Africa.* Oxford: Oxford University Press.

Gatakaa, G. (2012). *Uhakiki wa Maudhui Teule katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa. Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu cha Nairobi. Haijachapishwa.

Genette, G. (1999). *Narrative Discourse: An Esssay in Method*. Ithaca: Cornell University Press.

Gituku. N. (1990). "*Maigizo ya Kienyeji wa Watoto Nchini Kenya*". Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Guantai, J.G. (2003). *Mwongozo wa Kilio cha Haki.* Nairobi: Acacia Publishers.

Holder, H. (1981). *Aesops Fables*. Chicago: Vicking Press.

Hornby, A.S. (2012). *Oxford Advanced Learner`s Dictionary*. Oxford: Oxford University Press.

Huck, C.S. (1979). *Children Literature in the Elementary School (3rd ed).* New York: Holt and Winston.

Hunt, P. (1994). *An Introduction to Children`s Literature*. Oxford: Oxford University Press.

Kabira, M.W (2002*).* *Kenyan Oral Narratives: A Selection*. Nairobi: East African Educational Publishers LTD.

Kahigi, K.K. (1995). Lugha katika Vitabu vya Watoto katika, *Kioo cha Lugha*. Dar es salaam: TUKI. Kur. 24-27.

Kariuki, E. (2010). *Ngiri Mganga,* Nairobi: Phoenix Publisher Ltd.

Kairu, W.M. (2005). *Uhalisia wa Mtindo wa Ken Walibora katika fasihi ya Watoto*. M.A. Thesis Kenyatta University Nairobi. (Haijachapishwa).

Kipury N. (2002) *Oral Literature of the Maasai*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Kipury, K. (1983). *Oral Literature of Maasai.* Nairobi: Heinemann Publishers.

M'Ngaruthi, T. K. (2008). *Fasihi Simulizi na Utamaduni*. Nairobi: Autolitho LTD.

Madumulla, J.S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Dar es salaam: Mture Education Publishers Ltd.

Mayega, P.B. (2004). *Sisimizi Amuua Tembo.* Nairobi: Mvule African Publishers.

Mbiti, S.J. (2011). *African Religious and Philosophy*. Nairobi: East African Educational publishers.

Miruka, O. (2011). *Encounter with Oral Literature.* Nairobi: East African Publishers.

Mpesha, N. (1995). Children's Literature in Tanzania*: A literary Appreciation of Its Growth and Development.* PhD Thesis, Kenyatta University. (Haijachapishwa).

Msokile, M, (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi,* Dar es salaam: TUKI.

Mugenda, O. & A.G. Mugenda. (1999). *Research Methods Quantitative & Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Ngugi, P. (2009). *Language and Literary Education*: *The state of childrens`s Literature in Kiswahili in Kenya*. Saarbrucken. Lambert academic Publishing.

Ngugi, P.M. (2010). "*Nafasi ya Ubunifu katika Mchezo wa Watoto wa Michongoano". Katika kioo cha Lugha*. Juz. 8, Kur. 67-79.

Ngugi, P.M. (2011). *Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya katika Kioo cha Lugha*. Juz. 9, Kur. 84-94.

Ngure, A. (2011). *Fasihi Simulizi.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Nikolajeva, M. (2002). *The Rhetoric of Character in Childrens Literature*. London: The Scare Crow Press, Inc.

Njogu, K. & R. Chimera. (2011). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: English Press Ltd.

Nyaga, D. (1997). *Customs and Traditions of Meru*. Nairobi: East African Publishers.

Nyakeri, F. (2011). *Sungura na Mbwa*. Nairobi: Marimba Publishers Ltd.

Okhoba, E. (1995). *Style and meaning of Abamarachi Children's Oral Poetry*. M.A Thesis Kenyatta University. (Unpublished)

Orwell, G. (2011*). Shamba la Wanyama*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Palinkas, L. A., Horwitz, S. M., Green, C. A., Wisdom, J. P., Duan, N., & Hoagwood, K. (2015). Purposeful Sampling for Qualitative data Collection and Analysis in Mixed Implementation Research. "*Administration and Policy in Mental Health and Mental Health Services Research"*, *42*(5), 533-544. 05 January 2019.

Pierce, C. (1977). *Semiotics and Signific: The Correspondence between Charles. S. Pierce and Lady Victoria Welby.* Indiana: Indiana University Press.

Prince. G. (2003). *A Grammar of Stories.* The Hague: Mouton Publishers.

Propp, V. (1968). *Morphology of the Folktale*: Austin: University of Texas Press.

Rosenblatt, L. (1995*). Literature as Exploration.* New York: The Modern Language Associatio of America.

Rothlin, B. (2001). *The Stylistics and Novel: A Stylistic Analysis of some Aspects of Emily Bronte's Wuthering Heights*. Diplomarbeit, University of Vienna.

Salami, Y.K, (1998). "*Yoruba Proverbs as a Mechanism for Social Regulation*." In C. Ulrike. (Eds). *Swahili Forum* 56. Institute fur Afrikanistik. Koln: University Zu Koln .147 – 161.

Senkore, F. K. (1982). *Fasihi*. Dar es saalam: Dar es saalam Press and Publishing Centre.

Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi, Kwa Shule Vyuo na Ndak*i. Mwanza: Serengeti Publishers.

Simpson, P. (1977). *Language Through Literature. An introduction.* London and New York: Routedge.

Smith, R. W. (1832). *The Thirteen Moral Fables of Robert Hernyson. A modernized Edition*. Maitaland club publishers.

Tucker, N. (1981). *The Child and the Book: Apsychological and Literary Exploration*. Cambridge: Cambridge University Press.

Tudor, J. (1986). *The Law of Kenya, An Introduction Cases and Statutes.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

TUKI. (2004). *Kamusi Ya Kiswahili Sanifu*. Dar es salaam: Oxford University Press.

Wahiga, G, (2003). *Sarufi Fafanuzi ya Kiswahili.* Nairobi: Longhorn Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi naNadharia.* Nairobi: Nairobi Focus.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi, Simulizi na Andishi*. Nairobi: English Press Publishers.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanizi Ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Daisy Printers (K) LTD.

Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Video Mulwa Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2011). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: English Press.

Wamitila, K.W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix.

Weche, M. (2000). *Children's Literature as an image Forming Force. A case Study of Ezekiel Alembi's Books*. M.A. Thesis Kenyatta University.


Wood, J, (2014). Fables with Happy Endings more likely to Inspire Honesty in Kids. *Psych Central news*. https://psychcentral.com/news/2014/06/21/fables-with-happy-endingsmore-likely-to-inspire-honesty-in-kids/71529.html. 03 October 2019.

## VIAMBATANISHO


**Kielelezo 1:** Tembo na Sisimizi (Mayaga 2004:14)



**Kielelezo 2:** Picaha ya Kiwavi aliyekula Kabichi ya sungura (Kariuki 2010:43).



**Kielelezo 3:** Wana wa Chura Kahawia katika mashindano ya urukaji (Kariuki 2010:20)



**Kielelezo 4:** Picha katika jalada ya *Sungura na Mbwa* (Nyakeri 2011)

